**18 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Arobaini na Nane – Tarehe 18 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Arobaini na Nane.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni kipindi cha Maswali. Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale aulize swali lake.

Na. 613

### Uhakiki wa Wastaafu Ngazi ya Wilaya

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, lini uhakiki wa Wastaafu utafanyika wilayani badala ya mkoani kama ilivyo sasa, ili kuwaondolea usumbufu wa kusafiri umbali mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anawakilishwa na Mheshimiwa Geophrey Pinda. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wastaafu wanapata huduma bora, Mifuko ya Pensheni imeboreshwa, mifumo yake ya TEHAMA ambayo imesaidia kurahisisha uhakiki kwa wastaafu kwa kutumia alama za vidole. Maboresho hayo yamewezesha wastaafu kujihakiki kwa kutumia simu janja *(Smartphone)* bila kufika katika Ofisi za Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastaafu ambao hawana simu janja, uhakiki unaendelea kufanyika katika Ofisi za Mifuko zilizoko Mikoani na Wilayani na wale wenye changamoto za kiafya huhakikiwa kwa kufuatwa nyumbani kwao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yanayoonesha namna gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi inavyowajali watumishi hasa ambao wametumikia Taifa hili kwa weledi mkubwa. Kwa maana hiyo, sina swali la nyongeza ila ninaendelea kuipongeza Serikali kwa juhudi hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una *comment*? Tunashukuru.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya,

Mbunge wa Meatu, aulize swali lake. Nina mashaka hayupo, kwa niaba yake, Mheshimiwa Swai.

Na. 614

**Kupandisha hadhi Zahanati ya Mwabuzo kuwa Kituo cha Afya**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Mwabuzo - Meatu kuwa Kituo cha Afya?

**MWENYEKITI:** Majibu, Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kupandisha hadhi vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi baada ya kukidhi vigezo mbalimbali ikiwemo idadi ya watu na ukubwa wa eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mwabuzo yenye Zahanati ya Mwabuzo inakidhi vigezo vya kuwa na kituo cha afya kwa kuwa ina eneo la ekari 12 na idadi ya watu 13,483 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu na kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati zenye vigezo kote nchini ikiwemo Kata ya Mwabuzo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kwa niaba ya Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu amesema ameridhika na majibu ya Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri una *comment* ya kusema?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninampongeza sana Mheshimiwa Leah Komanya, pia Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali kwa niaba yake. Hii ni kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ujenzi wa zahanati zaidi ya 1,300, vituo vya afya zaidi ya 400, hospitali za halmashauri zaidi ya 129 na kazi inaendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mvomero ina zahanati zaidi ya 10 ambazo ni chakavu sana na za muda mrefu ikiwemo Zahanati ya Kijiji cha Nyandila. Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuzikarabati ama kujenga mpya katika vijiji hivi kwenye zahanati hizi ambazo ni za muda mrefu na zimechakaa sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba zipo zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri chakavu kongwe ambazo zinahitaji aidha ujenzi mpya au ukarabati wa majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Jonas Zeeland kwamba kwanza, Serikali ilishaainisha vituo vya afya na zahanati zote kongwe na hospitali za halmashauri zote kongwe na tumeshaanza ukarabati kwenye hospitali za halmashauri kongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tumeshakarabati zaidi ya hospitali kongwe 98. Hivi sasa tunaendelea na hospitali za halmashauri kongwe 50. Baada ya hapo tutakwenda kukarabati vituo vya afya chakavu 203 ambavyo tumeviainisha na tutafika

kwenye ukarabati wa zahanati chakavu. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zahanati hiyo tutakwenda kuikarabati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajenge, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Baadhi ya vijiji katika Jimbo la Mwibara vimeanza kujenga zahanati zao. Je, ni lini Serikali itashirikiana na hivyo vijiji, ili kukamilisha zahanati hizo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuunga mkono juhudi za wananchi katika ujenzi wa zahanati. Nitumie nafasi hii niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mwibara, kwanza kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya, kutenga maeneo na kuanza, kuchanga michango na nguvu zao katika ujenzi wa maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi huu uliopita Serikali imeshapeleka fedha zaidi ya shilingi 17,600,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 346 ya zahanati zote nchini. Zahanati hizi ambazo zimepelekewa fedha hii ni zile zahanati ambazo zimeanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kajege kwamba, Jimbo la Mwibara pia limepata fedha wiki mbili zilizopita kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma. Pia Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha maboma katika zahanati pote nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa Serikali imeweka vipaumbele kwenye

maeneo ambayo vituo vya afya vya mkakati kutokana na wingi wa watu na sisi tumeleta maombi kwa Kata ya Matui na Dongo, nini kauli ya Serikali kuhakikisha wananchi hawa kwamba, vituo hivi vitakuwa vya kipaumbele katika siku zijazo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kiteto ni moja ya majimbo yenye eneo kubwa kijiografia, pia lenye uhitaji mkubwa wa vituo vya afya. Ndiyo maana tangu mwaka 2021 mpaka sasa Mheshimiwa Rais amepeleka fedha nyingi katika Jimbo la Kiteto baada ya Mheshimiwa Olelekaita kutoa hoja za wananchi na Serikali sikivu ikapeleka fedha na vituo vimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Jimbo la Kiteto kwamba, Serikali inatambua uhitaji wa vituo vya afya katika kata hizo alizozitaja na kata nyingine za kimkakati, na tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinajengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Bado tupo Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini aulize swali lake.

Na. 615

**Hitaji ila Shule Watoto wenye Mahitaji Maalum Morogoro Vijijini**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Watoto wenye Mahitaji Maalum katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa watoto wenye mahitaji maalum kupata afua stahiki kwa kuzingatia hali yao ya ulemavu. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha shule kuwa jumuishi, kuboresha vitengo, kujenga hosteli, kutoa vifaa maalum na vifaa saidizi na ruzuku ya chakula kwa watoto wote wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa hosteli ya watoto wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Mvuha. Vilevile, Halmashauri inaelekezwa kukamilisha hosteli hiyo ili ianze kutumiwa na watoto wenye mahitaji maalum wa Shule za Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa watoto wenye mahitaji maalum.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwenye, matokeo ya Sensa ya Mwaka 2023 Halmashauri ya Morogoro imeonesha kwamba, tuna watoto 243 ambao wanahitaji mahitaji maalum ya elimu; wenye uoni hafifu wapo 97, wenye ukiziwi wapo 28 na wenye matatizo ya akili wapo 68; na wenye matatizo ya viungo wapo 50 ambao jumla ni 243.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idadi kubwa ya watoto hao, halmashauri imeshatenga eneo kwa ajili ya kupata Shule Maalumu ya Watoto hao. Shule ya Mvuha ni shule ambayo ni shirikishi. Sasa, ni lini Serikali baada ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini kutenga eneo itatujengea shule yenye uhitaji maalum ambao watoto wetu wote hawa wataenda kusoma, hasa ukitilia maanani mazingira ya jiografia ya Morogoro Vijijini, kata 13 kati ya kata 31 zipo milimani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Hiyo Shule ya Mvuha ya Halmashauri ambayo ni shirikishi, tumeona tuanze na watoto hao. Tuendako inaonekana tutakapokuja kuanza kutakuwa na upungufu wa madarasa. Je, Serikali haioni kwamba wakati tunajiandaa katika shule hiyo kufungua iongeze walau madarasa manne ya shule, ili kuondoa masongamano ambao unaweza ukajitokeza kwa watoto wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuweka vipaumbele kwa kuhakikisha kwamba shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum zinajengwa na zinawekewa miundombinu stahiki, zinapelekewa walimu wenye mafunzo maalum kwa ajili ya kufundisha watoto wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limefanyika kote nchini ikiwemo katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini katika Shule ya Mvuha. Pia tunatambua kwamba bado kuna uhitaji wa shule za watoto wenye mahitaji maalum. Ndiyo maana kila mwaka wa fedha Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Kalogeris kwamba tunawapongeza wananchi wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini, pia wewe Mheshimiwa Mbunge, Baraza la Madiwani na Menejimenti nzima ya Wilaya na Halmashauri kwa kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule hii ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Serikali itakuja kufanya tathmini na kuona kama inakidhi vigezo kwa maana ya idadi ya watoto watarajiwa katika eneo hilo, ili tuweze kuendelea na hatua nyingine kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na hii Shule ya Mvuha, tumeendelea na ujenzi, tumeanza na ujenzi na shule shikizi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, lakini tunafahamu kwamba bado kuna uhitaji wa madarasa na miundombinu

mbalimbali. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu za mapato ya ndani ya halmashauri, pia fedha za Serikali Kuu ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga miundombinu katika shule hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madarasa ya watoto wenye uhitaji maalum katika Shule ya Msingi Mbande? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, ili tuweze kufanya tathmini na kufanya *mapping* ya uhitaji wa madarasa ya wanafunzi wenye uhitaji maalum katika Shule ya Msingi ya Mbande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaona namna ya kufanya kwa sababu dhaminra ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, huduma za elimu, malezi na mafunzo kwa watoto wenye mahitaji maalum zinaboreshwa popote ambapo inawezekana kuboreshwa. Kwa hiyo, jambo hili tumelichukua, tutalifanyia kazi na tutakupatia mrejesho Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, bado tupo Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki aulize swali lake.

Na. 616

**Ujenzi wa Miundombinu ya Shule Kongwe**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga fedha kukarabati na kujenga madarasa mapya katika Shule kongwe ili kuboresha mazingira ya kujifunzia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya ukarabati wa shule kongwe nchini ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 168.31 zilitumika kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za msingi 793 na sekondari 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga shilingi bilioni 26.13 kwa ajili ya ukarabati wa shule 259. Aidha, kutokana na baadhi ya shule kuwa chakavu kiasi cha kutokarabatika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika shule hizo kwa kujenga miundombinu mipya kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa shule chakavu au kujenga miundombinu mipya katika shule zisizokarabatika kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Shule nyingi sana katika Jimbo la Singida Mashariki, shule kongwe zina hali mbaya sana, hivyo kufanya mazingira ya kujifunzia watoto wetu kuwa siyo salama, ikiwemo kutokuwa hata na matundu ya vyoo ambapo ninayo mifano michache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, katika Shule ya Msingi Kinyamwandyo, Mahambe, Mwau, Sambaru, Dung'unyi, Damankia, Choda, Mkiwa, Makiungu, Mungaa, Minyinga, Sule, Siuyu, Ntuntu na Mampando. Shule hizi zina hali mbaya sana. Ninataka kujua Serikali ina mpango gani wa haraka kuweza kusaidia shule hizi ili watoto wetu waweze kupata mazingira mazuri ya kujifunzia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika Jimbo la Singida Mashariki au Wilaya ya Ikungi kwa ujumla tuna upungufu mkubwa wa walimu hasa walimu wa kike. Walimu hawa wa kike kuna baadhi ya maeneo shule nzima ina watoto zaidi ya 700 haina mwalimu wa kike hata mmoja. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili, kwa sababu ya kuendelea kuwasaidia watoto wetu makuzi mema?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Zipo shule ambazo ni chakavu na ni kongwe, lakini kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 168 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Shule za Sekondari zaidi ya 89 na za msingi zaidi ya 793.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili la ukarabati ni endelevu kupitia fedha za Serikali na programu mbalimbali. Tuna mpango wa *BOOST* kwa Shule za Msingi, tuna mpango wa *SEQUIP* kwa Shule za Sekondari, na zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki kwamba, Serikali inatambua uwepo wa shule hizo chakavu katika Jimbo la Singida Mashariki na tayari tumeweka mpango endelevu wa kwenda kuzikarabati na kuzijenga shule hizo na madarasa hayo kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na upungufu wa baadhi ya miundombinu, hususan vyoo, nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwamba ni wajibu wao kuhakikisha kwenye bajeti za halmashauri wanatenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya vyoo kwenye shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya tundu moja la choo ni takribani shilingi milioni moja. Kwa hiyo, hata kama unahitaji matundu sita au 12 kila shule, kwa shule 10 siyo zaidi ya shilingi milioni 200, unaweza ukajenga na ipo ndani ya uwezo wa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusisitiza kwamba ile bajeti ya 40% miradi ya maendeleo, 60% miradi ya maendeleo ifanye kazi za kutatua kero za wananchi zikiwemo changamoto za shule ikiwemo miundombinu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na upungufu wa walimu katika shule, tunafahamu Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa vibali vya ajira, na katika miaka hii minne watumishi wengi wa sekta ya elimu wameajiriwa kila mwaka ikiwemo mwaka huu 2025. Halmashauri ya Ikungi pia imepata watumishi na zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba kuna upungufu wa walimu wa kike pia hata wa kiume. Nitumie nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Ikungi pia Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida kufanya msawazo wa ndani wa walimu wa kike kutoka kwenye shule ambazo zina walimu wengi zaidi angalau kupata walimu katika shule zile ambazo hazina kabisa walimu wa kike, ili watoto wetu wa kike waweze kupata huduma stahiki kwa mujibu wa taratibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Halmashauri ya Mbogwe inazo shule chakavu, Kata ya

Ikobe, Lugunga na Ushirika zipo na hali ngumu sana. Je, lini Serikali itatoa fedha ili shule hizi zikafanyiwe ukarabati?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Maganga na wananchi wa Jimbo la Mbogwe kwamba, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati na kujenga miundombinu ya sekta ya elimu, madarasa, ofisi, maabara na majengo mengine muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kukarabati na katika Jimbo la Mbogwe pia fedha nyingi zimepelekwa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu hii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili ni endelevu. Tutatumia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbogwe pia aendelee kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kukarabati madarasa katika shule zake ambazo ni chakavu. Hayo ni mahitaji ya wananchi na ni jukumu lake na ndiyo kazi ya mapato ya ndani ya halmashauri wakati Serikali Kuu ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono na kukamilisha shughuli hizo za ukarabati.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka wazi mpango uliopo wa ukarabati wa shule kongwe sana za msingi na sekondari kule Vunjo na hata kwa Tanzania nzima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ukarabati wa shule kongwe na chakavu

uko wazi. Tunayo orodha ya shule za sekondari kongwe na chakavu. Kwanza, ni zile ambazo zimekarabatiwa na gharama ambayo imetumika kukarabati, na shule ambazo zinahitaji ukarabati kwa orodha, kwa jina, kwa kila Jimbo, kwa kila Halmashauri na kwa kila mkoa kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Jimbo la Vunjo ni moja ya majimbo ambayo shule zake chakavu zilishawasilishwa na Mheshimiwa Mbunge. Pia na wataalam wa Halmashauri na Mkoa, tayari tunayo orodha hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba orodha hiyo iko wazi, kukiwa kuna mahitaji itapatikana wakati wowote. Mpango wa Serikali ni kutafuta fedha kuhakikisha kwamba tunakarabati shule hizo.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Omari Kigua, atafuata Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi *Masagalu Mission* ni shule ya mwaka 1948 na ilikuwa ni *Middle School*. Sasa, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukarabati shule hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule hiyo ya Msingi *Masagalu Mission* katika Jimbo la Kilindi kwa kaka yangu Mheshimiwa Omari Kigua, kwa hakika ni shule kongwe ya mwaka 1948. Kwa vyovyote vile inahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilindi, kutuma wataalamu wake kwenda kufanya tathmini ya mahitaji, kwa maana ya gharama zinazotakiwa kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo na kuziwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kutupatia mpango wa mapato ya ndani tuone wanaweza kumudu kiasi gani na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maana ya Serikali Kuu tuweze kuona

namna ya kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kukarabati miundombinu ambayo imechakaa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuita Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi ya Karema, Ipola na Kaparamsenga ni shule zilizojengwa kati ya mwaka 1950, 1960 na 1970. Shule hizi ni chakavu kwa kiwango cha hali ya juu. Je, ni lini Serikali itaenda kuzikarabati au kujenga upya shule hizo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Karema, Ipola, na shule ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mpanda, nimhakikishie tu Mheshimiwa Kakoso kwamba kama ambavyo nimesema kwenye majibu ya swali la msingi, tayari tulishaainisha shule zote za msingi ambazo ni chakavu na kongwe zikiwemo shule hizo za Karema, Ipola na nyingine katika Halmashauri ya Tanganyika. Tayari Serikali imeendelea kutoa fedha karibu kila mwaka wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hizo ambazo ni chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, safari ni hatua, tunaendelea kwa awamu, na Serikali itaendelea kupeleka fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba shule hizo zinakarabatiwa. Ninatoa wito pia kwa Mkurugenzi wa Halmsahauri ya Tanganyika kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kukarabati majengo katika shule hizo chakavu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Babati Mjini tuna shule 19 ambazo ni kongwe, zilijengwa tangu miaka ya 1970. Tunaishukuru Serikali tulipata shule moja tu kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema Halmashauri zitenge *own source* zao. Kuna Halmashauri ambazo uwezo wao ni mdogo, mimi ya kwangu ni shilingi bilioni mbili tu. Naomba kauli ya Serikali, hamwoni kwamba ni wakati mwafaka sasa kusaidia zile Halmashauri ambazo *own sources* zao hazitoshelezi kwa sababu mahitaji ya wananchi ni mengi, na hizo shule ni nyingi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kwani alishawasilisha orodha ya shule kongwe na chakavu na Serikali imeendelea kupeleka fedha kama alivyosema kwamba tayari kuna shule moja imekarabatiwa. Pia kuna miundombinu mingi ya shule mpya imeendelea kujengwa katika Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua kwamba zipo Halmashauri ambazo hazina mapato makubwa ya ndani na haziwezi kumudu kukarabati shule hizi zote. Ndiyo maana katika kila mwaka wa fedha Serikali inatenga fedha kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka huu wa fedha Serikali imetenga zaidi ya shilingi 26,130,000,000.00 kwa ajili ya ukarabati, na zoezi la ukarabati linaendelea kote nchini. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na pia nisisitize kwamba ipo miundombinu midogo midogo ambayo pamoja na mapato madogo ya Halmashauri, bado wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ujenzi wa vyoo, kupaka rangi baadhi ya majengo, kurekebisha *ceiling boards* na baadhi ya majengo, hayo ni majukumu ambayo yako ndani ya uwezo wa halmashauri zote ambazo zinatenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hizo na Halmashauri ziendelee kutenga fedha pia kwa awamu kwa ajili ya kuendelea kukarabati miundombinu ya shule chakavu.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa, tumalizie swali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ninamwita sasa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba na swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwa niaba yake.

Na. 617

**Ujenzi wa Soko kwa Mpango wa *TACTIC* – Nanyamba**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa soko katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba chini ya mpango wa *TACTIC*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ni miongoni mwa Miji 45 ambayo imepewa kipaumbele cha kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu kupitia mpango wa *TACTIC*. Aidha, kwa Mji wa Nanyamba miradi iliyopendekezwa kutekelezwa kupitia *TACTIC* ni ujenzi wa barabara za Nanyamba – Nitekela – Nyundo – Mkondogo za kilometa 1.21, Migombani – Mnali kilometa 0.23, Mnali kilometa 1.27, Natindi kilometa 1.1, Shangani kilometa 0.45, Karume kilometa 0.71, Niteleka kilometa 0.85, na ujenzi wa stendi katika eneo la Madina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupitia mradi wa *TACTIC* utaandaliwa mpango kabambe utakaotumika kusimamia uendelezaji wa Mji wa Nanyamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa soko katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. Hivyo, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia mapato ya ndani, zimetengwa shilingi milioni 250 kwa ajili ya utekelezaji wa hatua za awali za ujenzi wa mradi wa soko na ghala la kuhifadhia mazao. Aidha, soko litajengwa katika Kata ya Nanyamba na ujenzi wa ghala katika eneo la Chitondola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa soko katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba kwa awamu na kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri ambayo imeyaleta mbele yetu, lakini kwa niaba ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, ni lini miradi ambayo imeainishwa kwenye majibu ya Serikali itaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Miongoni mwa *components* ambazo zitaendana na mradi huu, ni pamoja na ujenzi wa barabara kama vile ambavyo imeelezwa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ujenzi wa hizo barabara ambazo zimeainishwa kwenye huo mradi utaenda sambamba na ufungaji wa taa za barabarani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba iko awamu ya tatu au *tier three* ya mradi wa *TACTIC*. Hivi sasa Serikali iko kwenye hatua za kutangaza zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi

ambao watakwenda kufanya shughuli za ujenzi katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo husika kwamba Serikali inaendelea na taratibu za manunuzi na zinatarajiwa kukamilika wakati wowote kuanzia sasa ili kuhakikisha kwamba ujenzi wa miundombinu ya barabara, pia ujenzi wa soko na maeneo mengine unakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, katika mpango wa ujenzi wa barabara mijini, moja ya *component* muhimu ni kuhakikisha kwamba tunaweka taa za barabarani. Kwa hiyo, pamoja na ujenzi wa barabara hizi kuna *component* katika baadhi ya maeneo ya mijini kuhakikisha kwamba taa za barabarani zinawekwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya, utafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Halmashauri za Miji ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ametaja, Halmashauri ya Mji wa Bunda na yenyewe ni miongoni mwao. Nasi pale ni kujengewa barabara za lami kwenye mitaa ya Mji wa Bunda, kujengewa soko la kisasa, pamoja na machinjio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofuatilia huu mradi ilikuwa kwa Halmashauri ya Mji wa Bunda uanze tangu mwaka 2023, lakini mpaka sasa hivi kimya. Mwaka 2024 tuliambiwa ungeanza, na Mji wa Bunda unakua. Je, ni lini sasa mtakamilisha mradi huu ili Mji wa Bunda uendane na hadhi ya Mji hasa ukizingatia sasa hivi unaenda kuwa mji wa kitalii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Ester kwa namna ambavyo anaendelea kufuatilia miradi ya maendeleo, lakini nimhakikishie tu kwamba Halmashauri ya Mji wa Bunda iko awamu ya tatu *tier three*. Miaka iliyopita; mwaka 2023 na mwaka 2024 ilikuwa ni awamu ya *tier one* na *tier two*. Kwa hiyo, *tier three* haijachelewa, ndiyo muda wake sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu ambazo zinaendelea kwa sasa ni za manunuzi, kuhakikisha kwamba katika *tier three* Halmashauri zote zinakwenda kuanza utekelezaji wa miradi. Halmashauri ambazo ziko kwenye awamu ya tatu ni Bagamoyo, Bunda, Chato, Handeni, Ifakara, Kasulu, Kondoa, Mafinga, Makambako, Masasi, Mbinga, Mbulu na Nanyamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunatambua ujenzi wa barabara, ujenzi wa stendi, ujenzi wa machinjio, yote ni vipaumbele katika mradi wa *TACTIC* na tutahakikisha kwamba tunakwenda kuutekeleza baada ya kukamilisha taratibu za manunuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa, mradi wa Soko la Njia Panda ya Merya mradi huu katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida umekuwa ukisuasua, je, ni lini Serikali itaanza kujenga soko hilo katika Wilaya ya Singida?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Aysharose Mattembe nifuatilie kujua kwa nini ujenzi wa soko hilo katika Halmashauri ya Singida umekwama? Je, ni changamoto ya kifedha, ni changamoto ya mkandarasi au bado haijafanyika tathmini? Tukipata majibu hayo tutaweza kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha huduma za kijamii zinaboreshwa, stendi zinajengwa ili kwanza kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri, pia kuboresha huduma za kijamii katika nyanja za usafiri. Nimhakikishie Mheshimiwa Aysharose kwamba, jambo hilo tunakwenda kulifanyia kazi na tutampatia mrejesho.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Jesca Msambatavangu. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Kihesa ni moja ya miradi iliyoko kwenye *package* ya *TACTIC*. Tulikuwa tuna barabara, lakini pia tulikuwa tuna daraja linalotoka Kitwiru kuja Isakalilo. Hiyo yote ilikuwa ni *package* moja na ninafikiri tuko *tier two* katika miradi ya *TACTIC*, lakini kinachoonekana kinaanza pale, ni barabara tu, bado soko na daraja havijaanza. Je, ni nini sababu ya kutoanza hivyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Iringa iko awamu ya pili ya mradi wa *TACTIC,* na tayari tumeanza utekelezaji kwenye baadhi ya miradi kwa kuwapata wakandarasi na kuwapa kazi hizo kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine iko kwenye hatua mbalimbali za zabuni. Ikumbukwe kwamba miradi hii inatekelezwa na wakandarasi tofauti na taratibu za manunuzi zina hatua nyingi zikiwemo *negotiations* na mambo mengine kutokana na namna ambavyo wakandarasi wameomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo Iringa Mjini na Manispaa ya Iringa, kwamba tayari Serikali imeanza utekelezaji. Tayari tuko kwenye hatua za manunuzi, na wakati wowote tutakamilisha hatua hizo na miradi yote iliyoko kwenye *package* ya *TACTIC* Manispaa ya Iringa itaanza kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Nikushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Ninamwita sasa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 618

**Kilimo cha Umwagiliaji Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, ni hekta ngapi zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Mtwara?

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mkoa wa Mtwara una eneo la kilimo linalokadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 1,421,200, ambapo eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji linakadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 16,644.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, eneo linalomwagiliwa lina ukubwa wa hekta 3,848.6. Kati ya eneo, linalomwagiliwa ni eneo lenye ukubwa wa hekta 1,337.8. Linamwagiliwa kupitia miundombinu ya umwagiliaji iliyoendelezwa, na eneo lenye ukubwa wa hekta 2,510.8 linamwagiliwa kupitia mifereji ya asili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua mkakati wa Serikali ni upi kuhakikisha hizi hekta zote 16,644 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Mtwara zinaendelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo yote ambayo yana miundombinu ya umwagiliaji nchini yanatumika kwa kilimo mwaka mzima? Kwa sababu lengo la Skimu za Umwagiliaji ni kuhakikisha maeneo hayo yanatumika kwa kilimo mwaka mzima, lakini ukienda sehemu nyingi unakuta kilimo kinafanyika cha msimu kama kile cha kutegemea mvua ya kawaida. Je, ni nini mkakati wa Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Tunza Malapo kwa maswali ya msingi na kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano kuwawakilisha wanawake katika mkoa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu nimthibitishie; moja ya mkakati wa Serikali tulionao sasa hivi ni kwamba tunayafanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina maeneo yote haya ambayo tumeyaainisha yenye ukubwa wa hekta 16,000 ili kuhakikisha kwamba tunapata gharama halisi na baadaye tutatangaza kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo, hayo maeneo ni sehemu ya ile miradi yote ambayo tumeitangaza nchi nzima. Kwa hiyo, lipo katika utekelezaji wake sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo ya miundombinu ambayo zimepita skimu na hayatumiki kwa muda, moja ya mkakati mkubwa tuliopewa na ambao tunautekeleza sasa hivi ni kwamba, tutajenga mabwawa ambayo yatakuwa yanafanya kazi ya kukusanya maji wakati wa msimu wa mvua, lakini vilevile kupitia mito yetu ile ambayo haikauki katika mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndiyo jukumu kubwa ambalo tunalo sasa hivi ili tu kuhakikisha kwamba zile skimu hazitumiki tu wakati wa msimu wa mvua, bali zinatumika katika mwaka mzima. Kwa hiyo, tumeshafanya hivyo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha unaokuja, tunategemea kujenga mabwawa 100 ili kuondokana na hii adha ya watu kulima katika msimu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ndiyo sehemu ya mipango ambayo Serikali tunaitekeleza sasa hivi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Wilaya ya Mbarali ina wakulima wamwagiliaji wa mpunga. Yaani wapo wakulima wa mpunga na kuna umwagiliaji. Ni lini Serikali itaongeza nguvu hasa kama Naibu Waziri alivyosema kwenye jibu la msingi kuhusu kujenga mabwawa na kuwasaidia wananchi hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano kuwasaidia wanawake wa Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawathibitia tu kwamba suala la Mabarali lipo katika mpango. Mpango wa sasa ambao tunautekeleza ni pamoja na kwenda kujenga mabwawa katika eneo la Mbarali ili wananchi wale waweze kulima katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo tunalipa kipaumbele kwa sababu tunajua umuhimu wa Bonde la Mbarali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, nilikuona, ulishauliza swali. Haya, swali fupi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Mji wa Bunda kuna maeneo pia wanalima

mpunga. Je, ni lini sasa mtawajengea bwawa ili watu hawa waweze kulima kisasa?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kazi nzuri anayoifanya katika kipindi cha miaka mitano kuwakilisha wanawake katika Mkoa wake na wananchi wa Bunda. Kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba eneo la Bunda, na maeneo yote yale ambayo tumeyaainisha yanayofaa kwa umwagiliaji, tayari yapo ambapo usanifu wa kina umeshafanyika na sasa tunatafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji. Yapo maeneo ambayo usanifu unaendelea na baadaye tutatafuta fedha na kumpata mkandarasi ili yaweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niwathibitishie tu wananchi katika maeneo hayo kwamba mpango wa Serikali tunautekeleza kama ambavyo tumeahidi, na wananchi wale watapata mabwawa na *schemes* ambazo zitatumika katika kipindi chote cha mwaka, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Nimwite sasa Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba yake, swali litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 619

**Ujenzi wa Barabara ya *TAMCO* – Mapinga (Kilometa 23) kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa barabara ya *TAMCO* Mapinga kwa kiwango cha lami utakamilika, kwani imekuwa ikijengwa vipande tangu mwaka 2018?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi atajibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekuwa ikijenga barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo hadi sasa kilometa 4.7 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa sasa wakandarasi wawili wanaendelea na kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa sehemu ya kilometa 3.6 na kilometa 14.5 ambapo ujenzi kwa sehemu zote mbili unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2025 kwa mujibu wa mkataba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, maswali ya nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Mheshimiwa Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, analo swali moja la nyongeza na anauliza, "Lini upanuzi wa barabara kutoka Kibaha mpaka Chalinze utaanza?" *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, akimwakilisha Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Koka, ambalo limeulizwa kwa ustadi mkubwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, anayetaka kufahamu ujenzi wa barabara hiyo ya njia nane kutoka pale Kibaha kwenda mpaka Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakusudia kujenga barabara ya njia nane kutoka pale Kibaha mpaka Picha ya Ndege, lakini kutoka Picha ya Ndege kuelekea mbele Chalinze mpaka Morogoro tutajenga barabara nne. Tayari usanifu unaendelea na hatua za utafutaji wa fedha unaendelea, utakapokamilika, basi tutakwenda kujenga barabara hizo.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanaonesha, kwa kipindi cha miaka nane wamejenga kilometa nne. Kamati ya Bunge ya Bajeti ilishauri, kwa kuwa hakuna fedha, kwa nini wasiache kuleta miradi mipya, wakamilishe miradi ya zamani ili kuepuka kilometa nne kujengwa kwa kipindi cha miaka nane?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Halima Mdee, nadhani unatambua kwamba anamwakilisha Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Kwa hiyo, kama una majibu unaweza kuendelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima awe nayo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Halima Mdee kwa kufuatilia miradi ambayo Serikali inafanya. Nimhakikishie, haijalishi tumetumia muda gani? Dhamira ya Serikali ni kuikamilisha barabara hiyo mpaka Picha ya Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kutumia mfumo wa *PPP* (kushirikisha Sekta Binafsi) kuijenga barabara hiyo kuanzia pale Picha ya Ndege kuelekea Chalinze mpaka Morogoro. Alichokizungumza hapa, ametimiza wajibu wake wa Kibunge, ambao ni kuishauri, kuisimamia na kuikumbusha Serikali. Tumepokea ushauri wako Mheshimiwa na tumeona *concern* yake, tutaendelea kuifanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa ninaomba, ninadhani tumemaliza kwa upande wa ujenzi, sijaona mtu akisimama, lakini nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri tumalizane naye kabisa, kwa kuwa yeye anamwakilisha Waziri wa Uchukuzi.

Kwa hiyo, ninaomba twende kwenye swali Na. 622 na nimwite Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake, na kwa niaba yake, litaulizwa na Mheshimiwa Neema Lugangira.

Na. 622

**Hitaji la Usafiri wa Uhakika Kisiwa cha Mafia**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza: -

Je, lini Wananchi wa Mafia watapata usafiri wa uhakika wa njia ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa usafiri wa uhakika katika Kisiwa cha Mafia na maeneo yote ya mwambao wa Bahari ya Hindi. Katika kutatua changamoto hii, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO)* imempata Mshauri Mwelekezi ambaye atafanya kazi ya utafiti na kisha kuishauri Serikali namna ya kurejesha huduma ya uhakika katika Kisiwa cha Mafia na maeneo mengine katika mwambao wa Bahari ya Hindi yenye changamoto zinazofanana na Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi aliyopewa Mshauri Mwelekezi inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Serikali inatoa rai kwa wadau wa Sekta Binafsi

kwenda kuwekeza ili kuongeza huduma ya usafiri majini katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kufanya katika kuimarisha usafiri kwa ajili ya sisi Watanzania, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kwenye maziwa makuu kama vile kwetu Ziwa Victoria pamoja na Ziwa Tanganyika na kwingineko tunakuwa na usafiri wa uhakika ambao ni kwa ajili ya mizigo pamoja na sisi wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kutokana na ongezeko kubwa la ajali kwenye maziwa yetu hususan kwa wavuvi wadogo ikiwemo pia na kupoteza maisha, je, Serikali ipo tayari sasa kuja na mpango mkakati ambao utawezesha kuwa na vifaa vya uokozi kwa ajili ya wavuvi wadogo hususan wanawake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Neema Lugangira, kwa maswali yake ya nyongeza mawili; moja, likiwa ni ushauri, akimwakilisha Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, ambaye ndio mwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujibu swali la pili ambalo kimsingi ni ushauri juu ya Serikali kuwa tayari kuja na mpango kwa ajili ya kuwa na vifaa vya uokozi kwa wavuvi katika maziwa makuu hususan wanawake. Kwanza, nikubali ushauri wake kwa sababu ni ushauri mzuri na anatimiza jukumu lake la Kibunge la kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa sababu ni kweli kabisa katika maziwa yetu makuu watu wengi wanakufa wakiwemo wanawake, hivyo tumhakikishie kwamba mpango huo tutaufanyia kazi kama alivyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, aliuliza kuhusiana na usafiri wa uhakika katika maziwa makuu, nimejibu, na nimeeleza kwa kina kwenye jibu la msingi juu ya mpango wa Serikali katika kujenga na kuimarisha usafiri kwenye Bahari ya Hindi, na sasa Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu kwenye upande wa maziwa makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imeshaanza kufanya kazi mbalimbali za kujenga meli katika maziwa makuu na inafanya shughuli hizo kwa namna mbili. Moja, ni kuruhusu na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji binafsi au Sekta Binafsi ili waweze kuleta meli katika maziwa makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, mfano Ziwa Victoria tayari kuna meli mbalimbali au vifaa mbalimbali vya usafiri ambavyo vinafanya kazi na vimeendelea kutengenezwa kwa ajili ya kuboresha usafiri kwenye ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa upande wa Ziwa Tanganyika, hivi ninavyozungumza Sekta Binafsi wanajenga meli nyingine mpya nne ambazo zitakuwa zinasafirisha kutoka *New Kalemie Port* kuja mpaka bandari zetu za upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali kwa kutambua umuhimu mkubwa wa Sekta ya Uchukuzi, na kwa sababu wanataka kuboresha au kuleta muunganiko kati ya Bahari ya Hindi kupitia bandari zetu tatu kubwa ikiwemo ya Mtwara, Tanga na Dar es Salaam ili kuunganisha na nchi karibia nane ambazo zinapakana ambazo zinategemea bandari yetu kwa ajili ya kuzihudumia, tayari Serikali inajenga meli mbalimbali kwenye Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria pamoja na Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, aendelee kuwa na imani kwani miradi hiyo mbalimbali imesainiwa yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni moja katika maeneo mbalimbali. Vilevile, pamoja na kujenga meli hizo mpya, pia tunakarabati meli mbalimbali kwenye maziwa makuu ili kuhakikisha kwamba usafiri unaweza kuimarika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felix Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wananchi waishio mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Mkoa wa Kigoma, Katavi na Rukwa, tegemeo lao kubwa katika usafiri lilikuwa ni meli ya *MV* Mwongozo na Liemba. Lini ukarabati wa meli hizo utakamilika, kwa sababu mpaka sasa hivi meli hizi hazitoi huduma kwa zaidi ya miaka nane na wananchi hawana usafiri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wananchi wa Ziwa Tanganyika wana changamoto kubwa ya usafiri katika Ziwa hilo. Hii ni kutokana na kwamba meli zilizokuwa zimejengwa kuanzia miaka ya zamani (*MV* Liemba, *MV* Mwongozo na *MT* Sangara) zilisimama kwa zaidi ya miaka nane kama anavyosema, lakini tumpongeze Rais wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kuziboresha meli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, meli ya mafuta inayobeba lita 410,000 ya *MT* Sangara imeshaanza kufanya kazi mwezi huu Mei, 2025 na inafanya shughuli zake kati ya Bandari yetu ya Kigoma pamoja na nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, meli yetu ya Liemba ambayo Wanakigoma na wanamwambao wote wa Ziwa Tanganyika wanaipenda sana. Tulishasaini mkataba pamoja na kulipa fedha za awali *(advance payment)* na Mkandarasi anakaribia 20%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa meli ya Mwongozo, tumeshakamilisha taratibu za awali, tumeshampata mkandarasi, na hivi ninavyozungumza, tunategemea kusaini muda wowote ili ujenzi huo au ukarabati huo uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Kavejuru na Wabunge wote wa Ziwa Tanganyika kwamba Serikali inayo nia na itakwenda kuziboresha na kuzirejesha meli hizo zianze kufanya kazi kama ilivyokuwa inakusudiwa hapo awali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ninadhani tumemaliza, sioni mkono, lakini bado kuna swali moja. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa uliza swali lako.

Na. 623

**Kusafirisha Mazao ya Mbogamboga, Mifugo na Matunda Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, lini Bandari ya Dar es Salaam iliyoboreshwa itaanza kusafirisha Mazao ya Mbogamboga, Mifugo na Matunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliipatia *TPA* Kiwanja Na. P28 chenye ukubwa wa mita za mraba 239,053 kilichopo Kurasini, Dar es Salaam ili kiweze kutumika kwa shughuli za Kibandari ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa makasha, kukusanya na kupanga shehena kwenye makasha, kuhudumia shehena inayoharibika haraka yakiwemo mazao ya mbogamboga na matunda pamoja na maegesho ya malori yanayosubiri kuingia bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa matumizi ya eneo hilo ikiwa ni pamoja na usanifu wa kina vimeshafanyika, na hivi sasa *TPA* iko katika hatua za kutafuta rasilimali fedha ili kujenga eneo hilo. Kwa sasa shehena ya aina hiyo inasafirishwa kwa kutumia makasha maalumu *(reefer containers)* yaliyopo Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Serikali ni kuongeza idadi ya makasha hayo maalum *(reefer containers)* ili kukidhi mahitaji ya usafirishaji wa shehena aina hiyo ambayo inazidi kuongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niipongeze Serikali, lakini binafsi nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa umakini, ufasaha na weledi kwa namna anavyojibu maswali hapa ndani ya Bunge, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Ninapongeza hatua hii ya Serikali ya maboresho ya miundombinu ya vifaa vya uhifadhi wa mazao ya mbogamboga, lakini je, Serikali haioni kwamba ni muhimu pia mpango huu wa maboresho ukaendana sambamba na kuweka magari maalum yatakayokuwa yanasafirisha bidhaa hizi kutoka maeneo ya uzalishaji kuja katika eneo la bandari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mazao haya ya mbogamboga kwa kiasi kikubwa na kwa sehemu kubwa kwa mwaka yanalimwa Wilaya ya Lushoto kwa Mkoa wa Tanga, lakini kwa kanda ya Kaskazini ni karibia mikoa yote (Kilimanjaro, Arusha na Manyara) wanalima kwa msimu mzima wa mwaka. Je, Serikali haioni umuhimu pia kuweka mazingira ya miundombinu hiyo hiyo katika Bandari ya Tanga ili mazao haya yasitumie umbali mrefu wa kutoka maeneo ya uzalishaji kwenda katika bandari ya Tanga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rashid Shangazi katika swali lake la kwanza, anazungumza kuhusu kuwa na magari maalum. Hivi ninavyozungumza katika bandari zetu tatu, tulichokifanya ni kuweka miundombinu *(reefers' point)* ambapo wateja wetu au wawekezaji au wafanyabiashara wanakuja na *reefer containers,* kisha wanaziwasilisha pale bandarini na zinasafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda huu ninamwomba Mheshimiwa Shangazi, tuendelee kuhamasisha kulingana na uhitaji. Wawekezaji wetu binafsi hawa waendelee kufanya hivyo ili Serikali isianze kwenda kwenye kununua tena ma-*container* au magari kwa ajili ya kazi hiyo. Tuipe fursa Sekta Binafsi kuweza ku-*grow*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge pia kwa kazi ambayo inaendelea kufanyika, na ninamshukuru kwa jinsi alivyokuwa mfuatiliaji wa karibu sana wa maendeleo ya Mkoa wa Tanga, ikiwemo bandari yetu ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kwamba huko nyuma tulikuwa na changamoto kubwa sana na mahali pa kuhifadhi mazao ya mbogamboga na mengine yanayofanana na aina hiyo. Hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita mara baada ya kuingia madarakani mwaka 2023 tulifanya maamuzi ndipo tukajenga *reefer point* (sehemu za kuhifadhia yale ma-*container*) kabla hayajaingizwa kwenye meli kuondoka ambapo tumejenga 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikionekana kuna uhitaji zaidi, sisi kama Serikali tupo tayari kuendelea kuboresha na kuongeza zaidi ili tu bidhaa hizo zinapokuwa zinafikishwa kwenye bandari zetu *especially* Bandari ya Tanga ambayo ameizungumza Mheshimiwa Mbunge, ziwe zinabaki na ubora ule ule, na hivyo kuweza ku-*maintain* soko katika masoko yetu ya Kimataifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa, turudi kwenye Wizara ya Maji, nimwite sasa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, aulize swali lake.

Na. 620

**Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia – Mbulu Mjini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kujenga Mradi wa Maji kupitia Benki ya Dunia Kata za Murray, Nambis, Kainam, Nahasey na maeneo jirani Tarafa ya Nambis?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, atawakilishwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa kimkakati katika Wilaya ya Mbulu kwa kutumia chanzo cha Mto Tsoray.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji *(intake),* ujenzi wa nyumba ya mitambo, ujenzi wa matanki saba yenye jumla ya ujazo wa lita 4,600,000, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 369.8 sanjari na ujenzi wa vituo 320 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo unalenga kuhudumia vijiji 21 vilivyopo katika Kata Saba za Mbulu Vijijini sanjari na mitaa 58 iliyopo kwenye Kata Saba za Mbulu Mjini pamoja na vijiji 16

katika Kata, vilivyopo katika Kata za Murray, Nambis, Kainam na Nahasey.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaishukuru Serikali kwa kazi kubwa ya maji iliyofanya katika Jimbo la Mbulu Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa taarifa ya awali, mradi huu ni wa shilingi bilioni zaidi ya 80, ninaiomba Serikali itafute utaratibu wa kuweza kutupatia fedha hizo ili mradi huu ujengwe katika kata na mitaa hiyo iliyotajwa, kwa sababu tarafa nzima ya Nambis haikuwa na maji takribani toka kuanzishwa kwake, na vijiji hivyo vilikuwa vinachukua maji kwenye vyanzo ambavyo siyo salama. Kwa hiyo, ombi langu hili lifanyiwe kazi na sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pokea.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea, nimtoe hofu Mheshimiwa Issaay na nimshukuru sana kwa kuishukuru Serikali kwa jitihada zinazofanyika. Tumpongeze Mheshimiwa Rais, kwani anahakikisha maeneo yote ya mijini na vijijini tunaendelea kuwatua ndoo kichwani akina mama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kagera, *specifically* Wilaya ya Muleba tunashukuru kwa miradi mikubwa inayoendelea. Sasa tungependa kujua, tuna mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya kata sita. Ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa kwa ajili ya hizo kata sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza

sana Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kwa namna ambavyo ameendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Maji. Mradi wa Ziwa Victoria kwenye hizi kata sita, taratibu zinaendelea kufanyika kuhakikisha mradi huu nao unakuja kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ninashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa vile una maswali mengine katika Wizara yako ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba twende kwenye swali namba 624 ili usirudi hapa.

Sasa nimwite Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, aulize swali lake.

Na. 624

**Hitaji la Minara ya Simu Vijiji vya Jimbo la Manonga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu Vijiji vya Uswaya, Ncheli, Mwakabuta na Mpogolo, Manonga?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilijumuisha Kata za Igoweko na vijiji vyake, ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Uswaya, katika Mradi wa Tanzania ya Kidigitali kwa maana ya *DTP,* ambapo ujenzi wa mnara katika Kijiji hiki umekamilika, na wananchi wake wananufaika na huduma ya mawasiliano kupitia mtoa huduma *Vodacom.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Vijiji vya Ncheli, Mwakabuta na Mpogolo, *UCSAF* itavifanyia tathmini vijiji hivi ili kubaini changamoto na mahitaji halisi ya huduma za mawasiliano na kuvijumuisha katika zabuni ijayo kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Seif Gulamali, maswali ya nyongeza, kama yapo.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, naishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya Mawasiliano kwa ujenzi wa minara katika Kijiji cha Uswaya na Igoweko. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, tulikuwa tunaomba katika vijiji hivi ambavyo mmeahidi kwamba wananchi watafanyiwa tathmini hivi karibuni, imekuwa ni kero ya muda mrefu sana. Tunaiomba Serikali iviingize katika mpango wake ili wananchi hawa waweze kupatiwa hii huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika maeneo ya Simbo, Mwisi pamoja na Nkinga, tunahitaji kuwa na *4G,* tofauti na sasa hivi ambapo mnara uko chini. Kwa hiyo, tunaomba, kama Wizara, mu-*upgrade* ili wananchi waweze kunufaika na *internet,* ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Seif Gulamali kwa ufuatiliaji na ushirikiano wake ambao amekuwa ukitupatia sisi Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa hii kero ya muda mrefu, angalau maeneo haya tuweze kuyafikia katika ujenzi wa minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Gulamali kwamba, nia ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha Tanzania yote inakuwa ya kidigitali. Kwa hiyo, maeneo haya ambayo bado ujenzi wa minara haujakamilika, na haujafikiwa, kama Serikali, tutahakikisha tunafanya jitihada ya kuona tunayafikia, na yeye pamoja na wananchi wote wa maeneo haya aliyoyataja watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja yenye *2G,* kwa ajili ya ku ya-*upgrade,* naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwaagiza watoa huduma wote, maeneo ambayo wana *2G* wahakikishe wanakwenda kuya-*upgrade,* ili wananchi sasa

waendelee kunufaika na jitihada za Serikali kuifanya Tanzania kuwa ya kidigitali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wengi wa Kata ya Makanya hawapati mawasiliano ya simu, lakini wakati huo huo kuna mlima mmoja kule Makanya unaitwa Ndelemai, katika Kijiji cha Kweulasi. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati sahihi sasa kujenga mnara katika mlima ule wa Kweulasi, ili kuondoa changamoto wanayoendelea kuipata wananchi wangu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza pia Mheshimiwa Shabani Shekilindi kwa ufuatiliaji na kuhakikisha wananchi wake tunawapelekea mawasiliano ya uhakika, hususan Kata ya Makanya, katika mlima huu alioutaja Mheshimiwa Mbunge. Ninapenda kusema, ninachukua kama ushauri, ili wataalamu wetu wa *UCSAF* waweze kufika na kufanya tathmini kama mlima huo utaweza kukidhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Serikali, imeanza kuchukua hatua ya kutekeleza ahadi yake kwa kujenga minara katika baadhi ya maeneo katika Jimbo la Hai, lakini yapo maeneo machache yaliyobaki katika Kata ya Kia, Machame Kaskazini, Machame Mashariki na maeneo mengine madogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia kazi hii nzuri ambayo imeianza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, amekuwa akifuatilia hili na hata

jana na leo tumewasiliana. Nikutoe hofu, mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunakuja kujenga minara katika haya maeneo yote aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Kama tutashindwa kukamilisha tathmini katika mwaka huu wa fedha kwa sababu tuko mwishoni, basi mwaka ujao wa fedha tutahakikisha tunayafikia maeneo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako. Aah, kuna swali moja hujalimalizia. Ninamwita; nani ameuliza hili swali?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara Mwikwabe, yeye hayupo. Kwa niaba yake, ninaye Mheshimiwa Jafari Chege atauliza swali hilo. *(Makofi)*

Na. 625

**Ujenzi wa Minara ya Simu Kata ya Mwema, Nyasincha na Itiryo; Tarime Vijijini**

**MHE. JAFARI W. CHEGE K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka minara ya simu maeneo ya Kata ya Mwema, Nyansicha na Itiryo - Tarime Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Nyansicha imenufaika kwa kujengewa mnara mmoja uliojengwa na Kampuni ya *Airtel* katika Kijiji cha Nyansicha na vilevile katika Kata ya Mwema imenufaika kwa kujengewa mnara na kampuni ya *Halotel*. Minara hiyo

imekamilika na inatoa huduma za mawasiliano kwa wananchi, kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Kata ya Itiryo haijanufaika na miradi ya mawasiliano ya simu, hivyo *UCSAF* itaifanyia tathmini Kata hii na vijiji vyake, ili kubaini mahitaji halisi ya huduma za mawasiliano na kuyajumuisha maeneo yote yatakayobainika katika zabuni ijayo kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wizara hii ya kutatua huduma ya mawasiliano, hasa maeneo mengi ya mipakani, lakini kumekuwepo na changamoto ya mwingiliano wa kimawasiliano katika maeneo ya mpakani kati ya Tanzania na Kenya wakati wa kupiga simu. Nataka nijue, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto hii, ili wakati wananchi wanapiga simu wakiwa maeneo ya Tanzania isisome mawasiliano ya Kenya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Pamoja na kuwa, Serikali kufanya kazi kubwa ya ujenzi wa minara katika Kata za mipakani ikiwemo Kata ya Mkoma, Ikoma, Roche na Goribe, na kwa kuwa, tumejenga mnara wa mawasiliano aina ya *Tigo* peke yake, nataka nijue ni mpango gani Serikali ilionao kuhakikisha inapanua wigo, ili huduma nyingine zipatikane, ikiwemo *Vodacom* na *Airtel* kwenye maeneo haya? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Chege kwa umahiri mkubwa aliouonesha na namna ambavyo ameweza kuwasilisha maswali kuhusu mawasiliano katika maeneo haya ya Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingiliano wa mawasiliano mipakani, sisi kama Wizara, tayari tunafanyia kazi kuona kwamba, wataalamu wetu wanakwenda kuangalia kwa nini *signals* za majirani zinaingia kwetu kirahisi kuliko za kwetu ambazo pia, minara iko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeshatoa ushauri mara nyingi kuhakikisha wenzetu wa jirani wanaelekeza zaidi vile vifaa vyao waweze kukamata *signals* kwenye maeneo yao, ili watoe huduma kwa watu wao kuliko namna ilivyo sasa ambapo baadhi ya minara na vile vifaa vimeelekezwa na kuleta utata. Kwa hiyo, sisi kama Wizara tunaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la eneo ambalo lina mtandao wa mtoa huduma mmoja, naomba pia, nitumie Bunge lako Tukufu niendelee kuagiza. Hili nimekuwa nikilisema mara nyingi, watoa huduma waendelee kuwa na ushirikiano wa karibu kwa sababu, tayari lipo katika utekelezaji; waweze kufanya *call location,* ili waweze kuokoa muda na gharama kwenye mnara mmoja ambao tayari umejengwa waweze kuwasiliana wakaweke vifaa vyao pale, wananchi wapate *alternative* ya hawa watoa huduma. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Jesca J. Msambatavangu Alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msambatavangu. Si nilikuona unauliza maswali! Mbunge wa Kilolo. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni lini Wizara itakamilisha ujenzi wa mnara wa Kata ya Kimala na Idete uliopo kwenye Kijiji cha Kiwalamo, ili Vijiji vya Idunda, Kiwalamo na Kimala viweze kupata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kilolo kwa kazi nzuri unayoifanya, na ufuatiliaji. Suala la mnara kukamilika, kwa sababu kazi

zimeshaanza, mnara lazima ukamilike ndani ya wakati. Lengo ni kuona kwamba, pale mnara unapojengwa, basi uweze kuhudumia na hivyo vijiji jirani alivyovitaja. Kwa hiyo, tutahakikisha ndani ya mwaka huu wa fedha huo mnara uweze kukamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, nasikia minong'ono kwamba mnataka kuuliza maswali mengi. Tunao wachangiaji wengi sana leo. Kwa hiyo, tunakwenda na muda kama kawaida.

Mheshimiwa Getere. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hii minara ni biashara. Kumekuwa na minara inajengwa katika vijiji mbalimbali. Minara hii ikienda kujengwa wananchi wa kawaida wale wajanja wanaenda kufanya mikataba na wenye minara wanawalipa hela, lakini Serikali za Vijiji kwenye maeneo hayo hazipati hela. Je, utaratibu wa Serikali ni upi wa kufanya Serikali za Vijiji ambapo kuna minara wapate fedha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nampongeza Mheshimiwa Getere kwa swali lake. Napenda kutoa taarifa kwamba, minara hii yote inayojengwa, Serikali za Vijiji zinapata fedha. Kwa hiyo, kama kuna kijiji hicho yeye anaona hakipati, naomba baada ya hapa tuwasiliane kwa karibu ili tuweze kufuatilia waweze kupata haki yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Tabora Mjini kwenye Kata za pembezoni hakuna mawasiliano, ikiwepo Kata ya Itetemia, Ntalikwa, Kalunde, Kabila na nyingine zilizoko pembezoni. Nini mkakati wa

Serikali kuhakikisha kata hizi zinapata mawasiliano, kama ambavyo watu wengine wanapata? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kwa ufuatiliaji wake mzuri. Hili swali alishawahi kuniuliza, nilichukua hatua, mimi mwenyewe nilifika Tabora nikakutana na watoa huduma pale. Tayari tumempa kazi mtoa huduma wa *Airtel,* anajenga mnara, na vilevile niliacha maagizo kwa watoa huduma wengine. Kata hii ya Itetemia tayari eneo limepatikana na kazi imeanza. Kwa hiyo, ni suala la muda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zimeanza, niwatoe hofu watu wa Itetemia na maeneo yote aliyoyataja Mheshimiwa Hawa, wanakwenda kufikiwa na huduma ya uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako.

Waheshimiwa, turudi swali la 621, tulikuwa tumeliruka. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Ninamwita sasa Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 621

**Sheria Kumshurutisha Mtoto Kuwatunza Wazazi**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatunga sheria itakayomshurutisha mtoto kuwatunza wazazi wake wakizeeka?

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Waziri, namwita Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuwalea na kuwapatia matunzo Wazee wasiojiweza ambao hawana familia na ndugu wa kuwatunza kupitia makazi ya wazee na wasiojiweza 13 yanayomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaendelea kufanya tathmini wakati wa utekelezaji wa Sera ya Wazee iliyoboreshwa, ambayo ina tamko la kuwataka watoto kuwajibika kuwatunza wazazi. Endapo kutakuwa na umuhimu wa kuwepo na sheria maalum kwa wazee wakati wa utekelezaji, basi Wizara itaanzisha mchakato huo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Serikali ina mikakati gani ya kupanua mitandao ya wadau mbalimbali ambao wamejikita kwenye kusaidia kutunza wazee hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika Sera ya Taifa ya Wazee, kama alivyosema, kuna tamko linalowataka watoto kuja kuwatunza wazazi wao hapo baadaye kwa kuwa, swali hili au suala hili ni nyeti sana? Je, Serikali haioni kwamba, ni lazima hili suala la kisera liwekwe kwenye sheria kwa sababu, kwa kufanya hivyo itawaanda watoto wakishajua ni la kisheria kuja kuwatunza wazazi wao hapo baadaye? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwa kuwajali wazee kwa sababu, sisi sote ni wazee watarajiwa. Swali lake la kwanza, Serikali ina mwongozo wa mwaka 2019 ambao unaeleza kwamba, mashirika na taasisi binafsi ambazo zinaweza kutoa

huduma kwa wazee, basi zifanye kazi kutokana na miongozo iliyowekwa, na Serikali tupo pamoja nao. Sisi tunashirikiana kwa pamoja na wadau wote ambao wanawalea watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili. Serikali kwa kupitia maboresho ya mwaka 2003, toleo la 2024, inawataka watoto wote au jamii kuwalea watoto wao, kama nilivyoeleza katika swali la msingi. Itakapoonekana kwamba sera hii haifanyi kazi vizuri, basi tutatunga sheria na kuileta hapa Bungeni kuhakikisha wazee wanatunzwa na watoto wao, na hatua kali zitachukuliwa kwa wale ambao wanawadharau au kutowajali wazee wao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimewaona mliosimama. Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tafiti zinaonesha kwamba, kuna idadi kubwa sana ya wazee ambao hawapati huduma stahiki katika uzee wao. Wengine wana watoto, wengine walibahatika kuzaa watoto, lakini wametangulia mbele ya haki kabla ya wazazi wao, na kuna wengine katika ujana wao hawakubahatika kupata watoto kabisa. Idadi ya vituo uliyotoa hapa ni 13 tu. Serikali haioni kwamba, kuna haja sasa ya kuhakikisha wanajenga vituo vya kuwalelea wazee katika Wilaya ili kuwasaidia wazee hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Esther kwa kujali wazee. Ni kweli, kuna wazee wengi ambao hawana watoto wa kuwalea, lakini Serikali kwa jitihada zake kama nilivyoeleza, hivi sasa tuna vituo 13 na tumeruhusu wadau au mashirika yasiyo ya Kiserikali kuendelea kujitokeza kuwatunza wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutokana na utaratibu ambao tuliuweka, tunahakikisha kwamba tutawapa nafasi hizo ili

wazee wetu waweze kuwa na mahali salama na kupata huduma zote za kijamii, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii na wasaidizi, ili waweze kutumika kwa ajili tu ya kufanyia kazi changamoto za wazee? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuajiri wafanyakazi wa Ustawi wa Jamii, ili kuwalea wazee hawa. Kwa Mwaka wa 2024/2025 Serikali iliajiri maafisa 178 na wasaidizi 176, jumla ni 2,323. Serikali itaendelea kuomba kibali cha kuajiri wafanyakazi hawa ili kuwapa huduma wazee wetu ambao ni watarajiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Danielson Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hii nafasi. Hivi karibuni kumekuwa na matukio ya wazee kuuawa katika mazingira ambayo hayaeleweki. Je, Serikali imejidhatiti vipi katika kupambana na matukio haya ya mauaji kwa wazee? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuwalea wazee wetu. Hivi tarehe 15 tulikuwa na siku ya kupinga ukatili kwa wazee. Kwa hiyo, Serikali inashirikiana na dunia nzima kuhakikisha sera, mikakati ya kuwalea wazee kupata ulinzi na usalama wao zinaimarishwa kuhakikisha wanakuwa salama, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali. Naleta kwenu majina ya wageni ambao wametutembelea leo katika Bunge letu.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Spika. Hawa ni Wachungaji 24 wanawake kutoka Jiji la Mbeya, wakiongozwa na Mchungaji Elika Mwakiyolile. Msimame tuwaone. Karibuni sana kwenye Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ambao wako Jukwaa la Spika, nina heshima kubwa kuwatambulisha wageni wangu wakiongozwa na mama yangu aliyenilea kutoka siku za mwanzo. Mama yangu yupo, lakini kwa sababu ya kiafya, yeye hakuweza kuja, lakini aliyempokea kunilea mpaka kuniozesha, ametutembelea katika Bunge letu, anaitwa Jane Mwanyika. Karibu sana Mama. *(Makofi)*

Mama yangu mlezi ameongozana na dada zangu na kaka zangu. Anayefuata ni dada yangu wa tumbo moja, anaitwa Hosana Mwanyika; anayefuata ni dada yangu mwingine ambaye ni mtoto wa kwanza wa mama aliyenilea, anaitwa Nancy Mwanyika; anayefuata ni Mhandisi Geofrey Mwanyika ambaye pia naye ni mtoto wa pili wa mama aliyenilea.

Waheshimiwa Wabunge, nitawataja kwa utaratibu huo. Anayefuata ni David Mwanyika, anayefuata ni Erke Mwanyika, anayefuata ni Roland Mwanyika, mwingine ni Christine Mwanyika, mwingine ni Erita Mutalemwa, mwingine ni Joyce Mbiyu, mwingine ni Jayday Sophia, mwingine ni Brian Kessy, mwingine ni Robert (huyu hakuweza kuja). Tunawakaribisha sana kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 79 wa Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais, Menejmenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hawa ni wanafunzi, waalimu na wazazi wa Kata ya Pwaga kutoka Jimbo la Kibakwe Mkoani Dodoma. Wapo pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni 23 wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge, na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hii ni Taasisi ya Kiraia ya *Tanzania Samaritan Community Organization (TASACO)*. Hawa wametoka Dar es Salaam, wapo pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hawa ni watoto wake kutoka Mkoani Mbeya. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge; hawa ni viongozi wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM kutoka Vwawa Mkoani Songwe. Karibuni sana viongozi wetu wa CCM. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge. Huyu ni ndugu yake, anaitwa Theonas Kinyonyo, ni Katibu wa Siasa na Uenezi Mkoa wa Katavi. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge; huyu ni ndugu Dayana Deus, Mwandishi wa Habari kutoka Bukoba Mjini Mkoani Kagera.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nape Moses Nauye, Mbunge; hawa ni rafiki zake. Katika ugeni huo kuna wageni mashuhuri wawili ambao ni wasanii ambao mnawatambua, mmoja ni Ndugu Haid Mohamed *(TID)*. Tuna mgeni mwingine mwanasanaa au msanii maarufu, huyu anaitwa Judith Wambura au kwa jina lingine Lady Jaydee kutoka Dar es Salaam. Tunawakaribisha sana kwenye Bunge, na tunatambua kwamba mtafanya *performance* pale *Royal Village*. Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana kwenye muziki ambao utakuwepo kwa siku ya leo na kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge; hawa ni waalimu wa Shule ya Msingi Mbande kutoka Chamazi Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; hawa ni wanafunzi 54 na waalimu nane wa Shule ya Sekondari Shefat kutoka Jijini Arusha. Simameni tuwaone watu wa Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 20 na waalimu wanne kutoka Shule Awali na Msingi Muungano ya Dar es saalam. Karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 90 na waalimu watano wa Shule ya Awali na Msingi Meta Dei kutoka Dar es salaam. Karibuni sana wageni wetu kwa mafunzo. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Olelekaita Kisau, hawa ni viongozi wa madhehebu ya dini mbalimbali kutoka Kiteto, Mkoani Manyara. Wapo pale! Tunawakaribisha sana viongozi wetu wa dini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo majina kwa sasa. Leo tunao wageni wengi na wengine bado wanangoja kuingia kwenye ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo machache, Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina mengi hapa ya wachangiaji wa siku ya leo. Tutaanza na mchangiaji wetu wa kwanza, nimwite Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, na Mheshimiwa Dkt. Pius Steven Chaya ajiandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni muweza wa kila jambo katika dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii ya kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa sababu ninaamini kabisa inakwenda kuakisi matarajio ya wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na timu yake yote ya Mawaziri, akiwemo mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Profesa Kitila Mkumbo na wasaidizi wao wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu aliyesimama hapa ametaja mafanikio katika eneo lake. Hakuna hata Mbunge mmoja ambaye amesimama hajataja mafanikio katika jimbo lake. Mimi siyarudii mafanikio haya ambayo yametajwa na wenzangu wote kwa sababu na mimi pia ni mwakilishi ambaye ninawakilisha kundi kubwa sana la wazazi, wanawake na watoto wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upande wangu sitataja miradi mikubwa. Ninajua kuwa imekamilika yote na mingine inaendelea kumaliziwa, ukiwemo uwanja wa ndege wa Kimataifa wa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni mmoja tu kwa upande wa bajeti. Ninaelewa sana kwamba kulipa kodi ni wajibu wa kila mwananchi. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wananchi wote wa Tanzania, waelewe kwamba huu ni wajibu wetu. Bila kukwepa kulipa kodi, nchi yetu itakwenda mbele kwa hatua ambazo tunahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa upande wa Serikali. Ninaiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu sana, tuwe waadilifu katika kukusanya kodi za wananchi. Kuweka makadirio ambayo hayaakisi biashara au kazi anayoifanya mwananchi ni kurudisha nyuma maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba katika eneo hilo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na timu yake pamoja na Mheshimiwa Profesa Kitila tuangalie kwa umakini, watu tunaowatuma kukusanya kodi wawe waadilifu. Wasifanye makubaliano na wafanyabiashara hao wakubwa ama watu wenye kipato kikubwa kuweza kupunguza kodi yetu katika Taifa letu. Huo ni ushauri katika sehemu ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mwakilishi wa wazazi, wanawake na watoto katika Taifa hili, nami nina mafanikio ambayo nimeyapata na ninataka niyataje leo hii hapa. Kwanza kwenye sehemu ya amani na utulivu. Ninaipongeza sana Serikali

ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Rais Samia kwa kuendelea kuitunza amani na utulivu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maendeleo yote tunayoyaona, bila amani na utulivu kudumu katika Taifa letu, tusingeweza kufika hapa. Kwa hiyo, ninaomba na nitoe wito kwa Watanzania, mwaka huu tunakwenda kwenye uchaguzi, amani yetu tuendelee kuidumisha, tukapige kura kwa amani, tuchague viongozi wetu ambao ninaamini kwamba bado Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ina uwezo mkubwa wa kuongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika eneo la elimu, elimu, malezi na maadili ndiyo sehemu kubwa ambayo nimeihudumia katika Bunge hili kwa kipindi hicho cha miaka mitano. Ninaomba tu nikumbuke au tukumbushane maneno ya Baba yetu wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alisema, "elimu siyo njia ya kuepuka umaskini, bali ni njia ya kupiga vita umaskini."

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hayati Abeid Aman Karume mwanzilishi wa Taifa letu la Zanzibar alisema, "tumesoma hatukuelewa, tumejifunza tumejua." Kwa nini nimekumbuka maneno hayo? Kwa sababu ninasema mimi kama mzazi, hakuna elimu ndogo. Elimu yoyote ambayo mtu amejifunza ikaweza kumsaidia kupigana na umaskini, hiyo ni elimu tosha kwake. Kwa hiyo, nikisema hivyo, na maneno yetu ya dini yanasema kwamba, aliye na elimu na asiye na elimu hatuwezi kuwafananisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kutambua, thamani ya elimu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweza kuongeza 57% katika Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Afya. Siyo hilo tu, imefanya maboresho makubwa ya sera ya elimu nchini. Mitaala yetu pia imeweza kufanyiwa kazi na kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo, mtoto au mwanafunzi aliyeko Zanzibar, na mwanafunzi aliyeko Tanzania Bara mitaala yao inafanana. Ni jambo la kujivunia sana. Mtihani utakapotungwa katika Baraza la Taifa la Mitihani *(NECTA)*

wanafunzi wote hawa watakuwa katika *level* moja. Hilo ni jambo la kujivunia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kuingiza elimu ya uraia, uzalendo na maadili kwenye mitaala yetu, ninaipongeza sana Serikali kwa kufikiria na kuingiza jambo hili kwa sababu huo ndiyo msingi wa kuwasaidia vijana wetu kuweza kulijua Taifa lao, kulipenda na kujua haki zao kama raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa upendo wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa nchi yetu ametoa ruhusa ya watoto wote waliositisha masomo kurudi kwenye masomo yao kwa sababu mbalimbali ikiwemo kupata ujauzito wakati wakiwa masomoni. Hili ni jambo la kujivunia kwa sababu hakuna mtoto mwenye akili na mwenye kutamani kusoma ambaye anasitisha masomo yake akaona raha. Mama kwa kuona hilo, ameona warudi masomoni waendeleze maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwa kuweka shule jumuishi kwa ajili ya watoto wetu wenye mahitaji maalum. Watoto wenye mahitaji maalum sio chaguo la mzazi kumzaa, bali ni majaaliwa ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, kwa kutambua thamani ya watoto hawa katika Taifa letu, na kwamba wao wana haki ya msingi ya kupata elimu, Serikali yetu imeweka maeneo tofauti au shule nyingi jumuishi kwa ajili ya watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali tuzingatie kuongeza bajeti katika eneo hili, kama siyo mwaka huu, basi kuanzia mwakani 2026 ikiwezekana, ili waweze kupata vifaa ambavyo vitaweza kutumika kwa wepesi kuwasomeshea watoto hawa, na waalimu mahiri katika eneo hilo, kwa sababu kuwasomesha watoto wa namna hiyo kunataka umahiri wa aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie namna ya kuwapata au kuwa-*train* waalimu hawa waweze kuwasimamia watoto wetu hawa ambao nao wana haki ya kupata elimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa kutengeneza au kutunga sheria mbalimbali, na kuzileta na sisi Bunge tukazitunga sheria mbalimbali za kudhibiti vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake. Tuna sheria nzuri sasa ambayo imedhibiti vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya wanaume kuwapa ujauzito watoto wakiwa shuleni. Kipindi cha miaka 30 jela kimekuwa ni tishio na fundisho kubwa, na vitendo hivi vimepungua kwa kiasi kikubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia adhabu ya kifungo cha maisha kwa wabakaji sugu, wale watoto wadogo chini ya miaka 10 hiki kimekuwa ni kielelezo kizuri cha kuonesha kwamba jambo hili sasa tumelikataa kwa namna zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kuwajali wazee. Wazee hawa wametumikia Taifa letu kwa muda mrefu. Kuongeza pensheni yao kutoka shilingi 125,000 hadi kufikia shilingi 250,000 imefikia takribani 150%. Ni jambo la kujivunia kwa jinsi ambavyo thamani ya wazee inaonekana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ninaliomba, nimezungumza muda mrefu sana, ninaamini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, watanisikia popote walipo, ni kuhusu Sera ya Malezi ya Taifa kwa watoto na vijana wa Taifa letu. Nimelizungumza mara nyingi sana hapa nikiamini kwamba tutakapokuwa na Sera ya Ttaifa ya Malezi kwa watoto na vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu linakwenda kuondokana na mporomoko wa maadili mkubwa sana, kwa sababu malezi siyo malezi ya mtoto tu. Nimejaribu kuuliza maswali mara nyingi, lakini nikapewa majibu yanayoelekea kwa watoto tu, lakini malezi siyo watoto, malezi ni kuanzia *zero-month* kwa maana anatoka kuzaliwa mpaka miaka mitatu, kuna aina yake ya malezi. Kuna miaka minne kuendelea mpaka sita kuna malezi yake, kuna saba mpaka 14 kuna aina ya malezi yake, kuna miaka 15 hadi 25 kuna aina ya malezi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapo tumeanza, ni mtoto mpaka kijana ambaye sisi tunasema ni mtu mzima tayari miaka 25. Kwa hiyo, huo ni ulezi wa Taifa hili. Kwa hiyo, kuanzia mtu anazaliwa mtoto, anaanza shule chekechea, anakwenda shule ya msingi, anakwenda sekondari, lakini mwisho anakwenda mpaka chuo kikuu, tunahitaji Sera ya Taifa ya pamoja ili wananchi wote kwa pamoja tuwajibike. Kwa sababu ninaamini kwamba sera ni miongozo ambayo inatolewa katika Taifa ili kila mmoja afuate miongozo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze kuokoa maadili ya Taifa letu, tuwe na sera moja. Nilitoa mfano hapa, nikasema tuna Sera ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 1987 ndiyo maana tukisema kwamba chama hiki kina misingi imara na hakuna wa kukitoa madarakani, tunamaanisha, kwa sababu sera hiyo imeweka wazi na bayana. Pamoja na kwamba ni ya muda mrefu, mimi nimeipitia yote nimeiona, bado inaweza kufanya kazi katika wakati tuliopo ikifanyiwa maboresho na chama.

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaheshimu sana muda wako na leo umesema una wachangiaji wengi, ninaomba sana nimalizie kwa kusema, naendelea kuunga mkono hoja. Niwaombee Watanzania wote waende kupiga kura na kuchagua viongozi ambao wanaona wataweza kufanya kazi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana na ninawatakia kila la heri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Najma Giga. Nilimwita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Dkt. Pius Chaya ajiandae, atafuata Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2025/2026 ambayo tumewasilishiwa wiki iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uzima kuweza kukutana katika Bunge lako Tukufu. Kama haitoshi, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba leo nasimama hapa nikiwa nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kumaliza miaka mitano ya utumishi wangu kwa maana ya kuwatumikia; na leo inawezekana ikawa ni siku ya mwisho katika kuchangia hapa Bungeni, na baada ya hapo tunakwenda kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wale wa Jimbo la Singida Mashariki kwa kuniamini na kuendelea kunipa fursa ya kuendelea kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu na kwa hakika katika muda wa miaka hii takribani mitano tumefanya mambo makubwa katika jimbo lile ambalo kwa hakika lilikuwa lina changamoto nyingi sana za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajivunia wote kwa pamoja na ninawaomba tuendelee kuwa pamoja kwa sababu tunaamini bado kuna mambo tunatakiwa tuyafanye na kwa sababu njia ya kufika huko ninaiona, basi tuendelee kushikamana pamoja unapofika wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kuonesha njia katika kuhakikisha anawaletea wananchi maendeleo. Zaidi nimpongeze sana Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, pamoja na Waziri wa Mipango, ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwa kutuwasilishia taarifa zao hapa, na leo tumepata fursa ya kwenda kuzijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ninawapongeza sana viongozi wote wa Serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya ambayo leo inaleta matumaini makubwa kwa Watanzania. Nimefurahi kuona kwamba tuna bajeti ya shilingi trilioni 56 takribani, hii ambayo ninaamini inaenda kutoa mwelekeo mpya kwenye maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependa sana kwamba, mwongozo uliopo kwenye bajeti hii ambao unasema mageuzi jumuishi ya uchumi kupitia uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, uwekezaji wa kimkakati wenye kuzalisha fursa za ajira na uboreshaji wa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yoyote lazima ilenge kwenda kubadilisha maisha ya watu na msingi mkuu wa kuweza kuhakikisha kwamba unaboresha maisha ya watu, lazima uweke mipango ya kukusanya fedha zitakazokupa nguvu ya kuweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Tumeona tumepatiwa tathmini fupi na Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu namna ambavyo kwa muda huu wa miaka hii alianza toka miaka mitano tulipoanza, miaka minne ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kazi kubwa imefanyika kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia miradi mikubwa ya kimkakati imejengwa. Ukiangalia katika kuchochea shughuli za Uchumi, tumeona mabadiliko ni makubwa sana, mfano *SGR* kwa maana reli ya kisasa, leo inatoa huduma mpaka Dodoma, na pia, Mradi wa Umeme wa Mwalimu Nyerere. Ili uweze kuwa na uhakika wa uchumi wa nchi yako, lazima uwe na chanzo cha uhakika cha nishati ambacho kinaenda kusaidia kwenye viwanda na shughuli mbalimbali za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za lami zimejengwa katika maeneo mbalimbali kuunganisha mikoa na wilaya, lakini madaraja na barabara za vijijini zimejengwa, na sisi ni mashahidi kwenye maeneo yetu. Pia, uboreshaji wa miundombinu ya elimu, Vyuo vya *VETA*, ujenzi wa hospitali na vituo vya afya, zahanati pamoja na vifaatiba, ni mambo ambayo ni ya muhimu yanayolenga kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa uboreshaji wa huduma hizi ni upatikanaji wa rasilimali fedha. Tumeshuhudia mapato yameongezeka kutoka ule mwaka 2021 ni shilingi trilioni 20.59 ambayo ilikuwa ni wastani wa shilingi trilioni 1.72 kwa mwezi. Kitu ambacho tunaona wazi kabisa kwamba Serikali imefanya kazi kubwa katika jitihada ya kuongeza mapato ambayo leo yanatupa nguvu ya kuweza kuhakikisha kwamba miradi hii tunaenda kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu kwenye eneo hili la ukusanyaji wa mapato, ninaiomba sana Serikali iendelee kuweka mazingira mazuri ya biashara katika nchi yetu. Zile ambazo zilikuwa ni changamoto, na bahati nzuri Mheshimiwa Rais aliweza kuunda tume ya kwenda kufuatilia changamoto ambazo tunazo katika sehemu za biashara, ambapo kumekuwa na urasimu kwa baadhi ya sekta mbalimbali zinazosimamia biashara, maoni ya wafanyabiashara yazingatiwe, na sisi kama wawakilishi wao tumekuwa tukiyaainisha hapa, na bahati nzuri kuna hatua zimeanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wafanyabiashara washirikishwe katika suala hili ili waendelee kutoa kodi bila kusukumwa, bila kulazimishwa, watoe kodi wakiwa wana furaha na mwisho wa siku waweze kufanya biashara zao na wenyewe waendelee kuboresha maisha yao. Eneo hili tukilifanya vizuri, tutaongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na tutaiongezea Serikali nguvu ya kuweza kuhudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye eneo hili nitaongelea kidogo suala la utalii. Tumeona namna ambavyo Mheshimiwa Rais alivyojitoa kwenye *Royal Tour*. Alienda kuitangaza Tanzania pamoja na vivutio vyake. Rasilimali za nchi yetu ambazo ni muhimu, zipo Tanzania, na mahali pengine hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama tulionao katika nchi yetu, mahali pengine hakuna. Kuna maeneo mazuri ya kutembelea yenye vivutio kama Serengeti, Mlima Kilimanjaro na baadhi ya maeneo mbalimbali. Tuendelee kuyatunza na kuwapa

ushirikiano wahifadhi ili waendelee kuwa na uwezo mkubwa wa kutunza yale maeneo ya vivutio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo ni kwamba, wenzetu wa *TANAPA* wanafanya kazi nzuri sana kupitia Mkurugenzi, Kamishna ndugu yetu Kuji, wanafanya kazi nzuri sana pamoja na wenzake, wanasimamia vizuri rasilimali hizi. Mapori yaliyotengwa (mapori tengefu) yaendelee kulindwa, yaendelee kutunzwa ikiwemo Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuona namna ambavyo Serikali imeweza kuhifadhi eneo lile ambalo wenzetu wa taasisi za Kimataifa wameendelea kusema ni eneo la kulindwa sana kwa sababu ni eneo pekee katika dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye eneo hili nilikuwa ninaomba wenzetu hawa wamekuwa kama ni miongoni mwa taasisi zinazokusanya mapato mengi ya kuisaidia Serikali kuweza kupata mapato ikiwemo fedha za kigeni. Kwa hiyo, kwenye eneo hili kumekuwa na changamoto kidogo. Tunaiomba Serikali wanapopokea fedha kuleta Hazina, basi waachiwe fedha kidogo kwa ajili ya kuendelea kupambana na suala la kibiashara ambalo halihitaji sana mpaka wasubiri fedha kutoka Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo kwenye barabara zinazoingia kwenye hifadhi zetu, barabara zile zikiboreshwa watalii watatembea wakiwa hawapati changamoto katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika eneo la elimu tumefanya kazi kubwa sana ambayo kimsingi tumewekeza kwenye madarasa, maabara na kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha elimu ya watoto wetu. Hata sera ya elimu imeweza kutolewa hivi karibuni ambayo inaenda kutoa mwongozo wa namna ambavyo changamoto zilizokuwepo, sasa tuziondoe tuboreshe elimu ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili ninaomba sana tuendelee kuboresha suala la *hostel* kwa watoto wetu.

Tumejenga shule nyingi za sekondari, tumejenga maabara katika maeneo mbalimbali, lakini tumekuwa na changamoto ya *hostel*. Kwa hiyo, tupate *hostel* watoto wetu waweze kupata sehemu ya kulala ili waweze kuwa karibu na shule ili wasipate changamoto mbalimbali ikiwemo mimba zisizotarajiwa kwa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumekuwa na tatizo la nyumba za walimu. Maeneo mengi ya vijijini hakuna hata nyumba za kupanga, walimu wanapatwa na changamoto kubwa. Ninaomba sana Serikali iendelee kuliona hili kupitia bajeti hii ili waweze kujenga nyumba za walimu ili walimu wetu waweze kufurahia, wakati wanatoa huduma katika maeneo mbalimbali, ikiwemo kuongeza idadi wa walimu kama nilivyouliza swali hapo asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa majisafi na salama, ni eneo la kichocheo kikubwa cha kuhakikisha kwamba watu wanaishi wakiwa na afya njema. Kwa hiyo, tumefanya kazi kubwa. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ameleta mitambo ya kutoboa maji kwa sababu chanzo ni muhimu sana kipatikane na baadaye tuweze kutafuta miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hili hata nikitoa mfano kwenye Jimbo la Singida Mashariki tumepata miradi mingi. Wakati tunaingia 2020 tulikuwa na 43%, leo tunaelekea 73%. Kiukweli tumepiga hatua kubwa sana kwenye eneo la sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili, ninaomba sana miradi iliyobakia tuweze kuletewa fedha ili iweze kukamilika kule kwa ambao tumeshapata vyanzo vya maji ikiwemo Vijiji vya Ujaile, Sambalu, Choda, Damankia, Samaka, Mandimu, Mahambe, Kinyamwandyo na Msule. Haya maeneo tayari tuna vyanzo vya maji, tunachoomba sasa tusaidiwe miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kilimo nipongeze sana, kazi kubwa ambayo ilifanyika. Mheshimiwa Waziri amefanya

kazi kubwa sana kuondoa kodi kwenye viuatilifu, ambavyo ndiyo vinaenda kusaidia changamoto ya kilimo cha Tanzania. Tumeweza kufanya kazi nzuri sana kwenye pembejeo kwa maana ya mbegu, tunalipa ruzuku pamoja na mbolea. Kazi nzuri imefanyika, leo inaenda kuongeza uwezo wakulima wetu kuweza kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la uzalishaji likifanya kazi vizuri sana, tutabadilisha maisha ya wananchi kijijini kwa sababu wengi wao wanafanya kilimo katika maeneo yetu. Kwa hiyo, eneo hili la kuondoa kodi kwenye viuatilifu vinavyotoka nje, inasaidia sana kuongeza uwezo wa uzalishaji ambayo imekuwa ni changamoto kubwa. Ninaomba sana Serikali eneo hili iendelee kulikazia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kushauri kwamba ili tuwe na uwezo mkubwa wa kufanya kilimo, tuendelee kuongeza nguvu kwenye eneo. Nimeona Mhadhiri, Mheshimiwa Prof. Kitila ameeleza suala la kuweka mkazo kwenye kilimo cha umwagiliaji. Mipango ya Serikali ilenge huko ili tuweze kupata fedha kuhakikisha kwamba tunapata eneo kubwa la umwagiliaji, tuweze kuwa na uwezo wa kuvuna mara mbili kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kushukuru sana na sera ya fedha iendelee kuangaliwa ili tuweze kuangalia shilingi yetu isiendelee kushuka, iweze kupambana na sarafu nyingine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naendelea kuunga mkono hoja na ninawatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo katika kazi kubwa inayoendelea kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Pius

Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia leo kwenye hii bajeti ya Wizara hizi mbili. Wizara ya Fedha ambayo ni Bajeti Kuu, lakini Wizara ya Mipango na Uwekezaji, niwashukuru hawa maprofesa wawili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Prof. Kitila, kwanza kwa kuwasilisha taarifa zao mbili ambazo kimsingi zimekuwa taarifa ambazo zimetusaidia kufanya tathmini ya Serikali kuona imefanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niseme, sisi Manyoni hatumdai Mheshimiwa Rais. Manyoni imekuwa mpya sasa hivi. Mambo makubwa yamefanyika Manyoni ndani ya hii miaka minne ya uongozi wake. Tukizunguka kufanya mikutano kule, watu huwa wanatuuliza, hivi haya mambo kwa nini hayakufanyika huko nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni mashahidi, katika majimbo yetu Tanzania nzima kuna mambo makubwa sana ambayo yamefanyika ndani ya huu muda mfupi wa miaka minne ambayo kimsingi huko nyuma yalikuwa magumu sana kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mradi mmoja wa maji, ulikaa zaidi ya miaka 20 wa Kintinku – Lusilile, bilioni 13, unaenda kwenye vijiji 11. Ndani ya miaka miwili ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa shilingi bilioni 13. Mradi ulishakamilika na wananchi wanapata maji. Kwa kweli sisi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, amewatua ndoo akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna Daraja la Sanza, kwenye kila Ilani huwa linawekwa, lakini mwaka 2023 Mheshimiwa Rais akatoa *commitment* Daraja la Sanza litangazwe. Lilishatangazwa, mkandarasi alishapatikana na wakati wowote ule mkandarasi anaweza akaenda *site*. Haya ndiyo mambo ambayo wananchi wanayataka huko. Wananchi hawataki siasa, wanataka waone maendeleo yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, upande wa elimu Manyoni sisi ni wanufaika wa zile shule za wasichana za mikoa. Tumepewa zaidi ya shilingi bilioni 4.5 kujenga shule ya wasichana ya mkoa, na tayari tumesha-*enrol* zaidi ya mabinti 500, wapo pale. Haya ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi shule zimejengwa watu hawakutegemea. Mikoa yote zimejengwa shule za wasichana na tumeenda kumkomboa mtoto wa kike. Sasa sisi watu wa Manyoni tuseme nini? Kwa kweli sisi watu wa Manyoni tumesema, ikifika Oktoba, tunaenda kuweka *tick* na tunategemea Mheshimiwa Rais akirudi, atafanya mambo makubwa sana Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hii miaka minne aliingia katika kipindi kigumu wakati huo Hayati Dkt. Magufuli alikuwa amefariki, ameweza kufanya mambo makubwa. Je, tukimpa miaka mitano mingine tuna uhakika atafanya mambo makubwa sana, na sisi tumekubaliana watu wa Manyoni tunaenda kumpa kura za kishindo Mheshimiwa Rais kwa sababu ametujali, ametuheshimisha. Yaliyobaki, hayo tunajua watayamudu. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunamwamini, Mheshimiwa Profesa Kitila tunamwamini, tunajua kabisa kupitia bajeti hii wanaenda kutatua zile kero mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niongelee kuhusu *SGR*. Wakati Mheshimiwa Rais anachukua nchi, *SGR* ilikuwa 30%. Mimi nipo kwenye Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tumetembelea huu mradi. Kwa kweli lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa *commitment* kubwa aliyoiweka katika *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote ni mashahidi, *SGR* imeshaanza kufanya kazi na wanufaika wengi wengi wamenufaika kupitia *SGR*, lakini ukiacha hilo, tayari tulishasaini *lot* nyingine kutoka Makutupora kwenda Kigoma, lakini vilevile kutoka Makutupora kwenda Mwanza. Haya ni mafanikio makubwa na wakandarasi wapo *site*. Tunataka nini Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *SGR* inaishia pale Makutupora, na nimemwona Naibu Waziri wa Uchukuzi pale, na tayari miundombinu imekamilika. Sasa hii treni basi iishie pale Manyoni - Makutupora ili na sisi tupande treni hii ya Mwendokasi. Kwa kweli sisi watu wa Manyoni tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, pale Manyoni tulikuwa na mradi wa umwagiliaji wa Udimaa ambao umepigiwa kelele sana. Kila Ilani ya Uchaguzi ulikuwa unawekwa. Mheshimiwa Rais alitoa *commitment* mradi ukatangazwa kwa kupitia Mheshimiwa Waziri Bashe. Tayari tumeshapata mkandarasi wa shilingi bilioni 18 kwa ajili ya kujenga Mradi wa Umwagiliaji wa Mbwasa. Haya ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaposimama hapa tunasema Manyoni imekuwa mpya, tuna sababu za msingi za kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ameonesha *commitment* kubwa. Kama nilivyosema, alichukua nchi kwenye mazingira magumu, lakini Mungu alimjalia, ameweza kufanya haya makubwa ndani ya hii miaka minne. Kwa hiyo, kwa sisi Wanamanyoni kwa kweli tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme, hawa Waheshimiwa Mawaziri wetu hawa, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Prof. Kitila, kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa-*exclude* kwenye haya mafanikio ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya, kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ndio amekuwa Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, tunaamini kabisa ushauri wake ndiyo umemsaidia Mheshimiwa Rais akaweza kutoa fedha zikaenda kwenye maeneo yetu. Leo hii Wabunge tunakuja kifua mbele kwa sababu tunajua kwamba yeye na Mheshimiwa Prof. Kitila walimshauri Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ninawashukuru viongozi wangu wa mkoa. Leo inawezekana ikawa ni siku ya mwisho ya kuongea hapa Bungeni, lakini nimshukuru mkuu wetu wa mkoa. Kwa kweli Mkuu wa Mkoa wetu, Halima Dendego anafanya kazi

kubwa sana, na tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kutuletea Mkuu wa Mkoa. Pia, Mwenyekiti wetu wa CCM wa Mkoa, Martha Mlata, anafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuna *RPC* wa mkoa, huko nyuma miaka 10 iliyopita pale Manyoni usalama haukuwa mzuri sana, lakini Mheshimiwa Rais alipoingia ameenda kukomesha hali tete ya usalama pale Manyoni, kwa kupitia *RPC* huyu huyu na wengine wote waliofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mkuu wa Wilaya wetu, Dkt. Vincent Mashinji, kwa kweli anafanya kazi kubwa sana, na sisi tunamshukuru sana, ameituliza Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunaye Mkurugenzi wetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Anastazia Tutuba, kwa kweli ametusaidia sana. Pale kulikuwa kuna shida shida ya mapato, lakini sasa hivi amewanyoosha, Manyoni sasa hivi ina mapato ya uhakika kwa hiyo mimi ninamshukuru. Vilevile, amepeleka fedha nyingi sana kwenye miradi ya mapato ya ndani. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mkurugenzi wetu wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, *OCD* wetu Msungu pale Manyoni, kwa kweli ametusaidia sana. Ninyi ni mashahidi, kuna muda pale Manyoni hali haikuwa nzuri, lakini tangu ameletwa pamoja na *OCCID*, Mpelelezi Fatuma Mtalimbo, wamejitahidi sana kutuliza pale, na sasa hivi watu wanaishi kwa usalama mkubwa sana. Haya yote ni kwa sababu ya *commitment* ya Mheshimiwa Rais, na ndiyo maana tunaona nchi ipo salama na watu wa Manyoni kwa kweli wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, ninamshukuru vilevile *RAS* wa Mkoa wa Singida, amefanya kazi kubwa sana, anamsaidia sana Mkuu wetu wa Mkoa. Pia, Mwenyekiti wangu wa CCM wa Wilaya ya Manyoni, wamenilea ndani ya hii miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki ambao walinipa hii heshima ya miaka mitano kuwa mwakilishi wao. Ninaamini sijawaangusha, na niwaombe tuendelee kupeana ushirikiano. Baada ya kuyasema haya, ninawashukuru sana. Ahsante sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuletea maendeleo Watanzania. Pia ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili pamoja na timu zote za wataalamu wa Wizara zao kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza maono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa miaka mitano, nimeshuhudia dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais katika kuwaletea Watanzania maendeleo na katika kuhangaika sehemu mbalimbali kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyakati nyingine tumeshuhudia Mheshimiwa Rais ameweza kutafuta nyongeza ya bajeti ili kufidia mapengo ambayo yalionekana, na kwenye hili ninampongeza sana Mheshimiwa Rais tena na tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaunga mkono maoni yote ya Kamati yaliyotolewa hapa. Pia, ninaunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu hapa. Tumeona asilimia kubwa ya maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti imeweza kuzingatiwa

kwenye utekelezaji wa mpango huu wa bajeti ambao Mheshimiwa Waziri aliusoma hapa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, tumeona kuanzia mwaka 2020/2021 – 2023/2024, ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Tulianza utekelezaji kwa 89.7% na mpaka 2023/2024 tumeona utekelezaji umekua kwa 96.7%. Kwenye hili vilevile ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha Bajeti za Serikali zinatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yametokana na kuboreshwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa kodi. Kwenye hili ninaomba nimpongeze kipekee kabisa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa mipango yake thabiti na jitihada zake za kuendelea kuhakikisha mapato ya Serikali ya kodi yanaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Hadi kufikia Mei, 2024/2025 tumeona makusanyo ya kodi yameongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 26.86 ambayo ni sawa na 91.23%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, ni wazi kabisa tukiendelea na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato, tunaona ni dhahiri kwamba kwa siku zijazo, basi bajeti ya Serikali inaweza ikahudumiwa hata zaidi ya 90% na mapato ya Serikali ya ukusanyaji wa kodi pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja kwenye mapendekezo ya kikodi aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, ninaipongeza Serikali, tumeona wameweza kupunguza kodi ya punguzo la *VAT* kutoka 18% hadi 16% kwenye malipo yanayofanywa kwa njia ya mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasababisha kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwa wananchi, na ndiyo dunia inapoelekea kwenda kwenye *cashlite economy*. Hii itarahisisha malipo, na vilevile itarahisisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato na hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Ninaipongeza sana Serikali kwa jitihada hii iliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia kwenye mapendekezo ya kikodi, tumeona kwamba kwenye ukurasa wa 160 Mheshimiwa Waziri alitueleza hapa, amependekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura Na. 147 "Kuongeza Ushuru kwenye huduma za mawasiliano ya Kielektroniki kutoka 17% hadi 17.5%." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kufikia 2050, tunaona kwamba tumejiwekea malengo ya kupeleka Tanzania kidijiti. Ongezeko hili la asilimia sifuri nukta tano, litaenda kuongeza gharama ya miamala kwa wananchi wetu, na hivyo basi, kuondoa malengo yetu haya kwenda kwenye Tanzania ya Kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya bajeti mara kwa mara imekuwa ikiishauri Serikali kupunguza gharama za miamala ili wananchi wengi waweze kutumia mitandao ya kielektroniki, lakini pia waweze kutumia bidhaa za kielektroniki. Kuongezeka kwa asilimia sifuri nukta tano kutasababisha Watanzania wengi washindwe kumudu gharama za miamala na gharama za mabando mbalimbali, na hivyo basi, malengo ya Serikali kutofikiwa kupeleka Tanzania Kidijiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia upya pendekezo hili, kwani litarudisha nyuma kufikia malengo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee kidogo kwenye vyanzo vya mapato. Ili bajeti yetu iweze kuendelea kufanikiwa kwa ufanisi mkubwa, ni lazima tuendelee kubuni vyanzo vipya vya mapato siku hadi siku. Pia tuangalie vyanzo ambavyo haviwezi kumuumiza mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninaomba niongelee biashara ya hewa ukaa (biashara ya Kaboni) ambayo biashara hii mtaji wake ni rasilimali zetu tulizonazo. Serikali bado haijatilia mkazo biashara hii, na nchi nyingine za jirani wananufaika sana na biashara hii ya hewa ukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii ni chanzo cha uhakika kama Serikali ikiweza kutilia mkazo. Kwa kuwa Tanzania tumebarikiwa misitu mikubwa, na kwa kuwa tuna maeneo mbalimbali ya malisho ambayo yakiboreshwa tunaweza tukafaidika na biashara hii ya hewa ukaa, ninaishauri Serikali, pia iweze kuangalia basi ni jinsi gani tunaweza tukafaidika na biashara hii ili tuweze kuongeza mapato yetu na tuweze kufadhili vizuri Bajeti yetu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaomba niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi mingi ya maendeleo aliyotuletea wananchi wa Mkoa wa Arusha. Sisi kwa ujumla tunasema hatumdai chochote Mheshimiwa Rais. Wabunge wa Majimbo wamesema hapa, kila Mbunge wa Jimbo amesema hakuna jimbo linalomdai Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pamoja wananchi wa Mkoa wa Arusha tunasema, "*Ashenaleng.*" Oktoba tunaenda kutiki, lakini siyo tu kutiki, tunaenda kumchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na tunaenda kuchagua Chama cha Mapinduzi kwenye ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimwia Maimuna Salum Mtanda, na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii iliyoko Mezani kwetu. Kabla sijasema lolote, kwa kuwa leo ni sehemu ya mwisho ya mchango wangu kwa awamu hii, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mungu ambaye amenipa kibali cha kuwatumikia wananchi wenzangu

wa Jimbo la Hai. Pia ninamshukuru sana kwa afya na uzima na kutuwezesha haya yote kuweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amefanya kazi kubwa, mapinduzi makubwa tumeyaona kwa kipindi ambacho amekuwa hapa. Pia nimpongeze Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri. Tunaona namna ambavyo anapambana kuweka mipango ya Serikali, na ninampongeza amehakikisha kwamba mipango hii ya Serikali sasa iwe inaletwa Bungeni. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwapongeze wananchi wa Jimbo la Hai na kuwashukuru kwa imani kubwa ambayo wamenipa kunifanya niwe Mbunge wao. Ninawashukuru sana sana wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaishukuru familia yangu kwa namna ambavyo wamenivumilia miaka hii mitano. Ninashukuru Viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Mzee Maganda mpaka ngazi ya Mabalozi. Ninawashukuru Waheshimiwa Madiwani ambao tumeshirikiana nao wakiongozwa na Mwenyekiti wetu wa Halmashauri, kaka yangu Edmond Lutaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Watendaji wote wa Serikali kwa namna ambavyo wametuwezesha kufanya kazi yetu: Walimu, Askari, na Watendaji wote wa Serikali; pia Wakuu wa Taasisi, ndugu yangu Kuya *Engineer* wa *TARURA*; ndugu yangu Mwampashe, *Engineer* wa *RUWASA*; ndugu yangu Bagabaji, *Engineer* wa *TANESCO*, pamoja na Watendaji wote wa Serikali wakisimamiwa na Mkuu wa Wilaya. Bila kuwasahau Viongozi wa Dini wote, baba yangu Dkt. Fredrick Shoo; na Shekhe wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, leo sina maneno mengi ya kushauri. Tumeshashauri miaka yote mitano hiyo, ninadhani iko kwenye kumbukumbu za Serikali. Leo ninampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mambo aliyoyafanyia nchi hii ni makubwa sana, anastahili

heshima kubwa sana. Ni lazima sisi Watanzania tukubali, tunadaiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninataka leo niwaulize, Mheshimiwa Rais alipoingia alisema, "Kazi Iendelee" na kweli tumeona kazi imeendelea. Hii miradi mikubwa yote aliyoitekeleza, bado alikuwa na utashi wa kuweza kusema mimi nianzishe miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuwa na sehemu anafungiwa labda ni lazima ahakikishe Bwawa la Mwalimu Nyerere limalizike, lakini amehakikisha limekamilika. Hakukuwa na mahali anafungwa kwamba, Daraja la Busisi lazima aliendeleze, angeweza kwenda kuanzisha daraja lingine, lakini akasema hii miradi mikubwa yote itekelezwe. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale katika Jimbo la Hai, mimi ninadhani amenipendelea zaidi. Shule mpya zilizojengwa ndani ya Jimbo la Hai ziko shule 10 mpya, tangu tumeingia na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ametuletea shilingi bilioni 37 tumejenga Chuo cha Kikuletwa na Waziri wa Elimu ameenda kuweka jiwe la msingi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga *VETA,* tumefanya ukarabati wa shule kubwa, Shule ya *Machame Girls*, Shule ya Lyamungo, Shule ya Harambee, Shule ya *Hai Day*, na hizi zote zimepelekewa zaidi ya shilingi bilioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa kwenye Sekta ya Afya. Wakati tunaingia Hospitali yetu ya Wilaya ilikuwa ni magofu, pale ametuletea shilingi bilioni 1.3, tumejenga jengo la Mama na Mtoto, *Pharmacy*, *Walkway, ICU* ya kisasa, na vifaatiba viko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga vituo vya afya vipya vinane. Nani kama mama Samia? Sisi tunakubali ni wadeni wazuri wa Samia, na Oktoba tunaenda kumlipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji, wakati tunaingia pale, Boma Ng'ombe kulikuwa hakuna maji. Nikazungumza hapa Bungeni, Mheshimiwa Rais akatupatia shilingi bilioni 3.9, mradi umekamilika, watu wa Hai wanapata maji ya kunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Skimu za Umwagiliaji, sasa hivi tuna shilingi bilioni 19 kule Mtambo; tuna shilingi bilioni tisa hapo hapo Mtambo, na pia tuna Skimu nyingine Metromu, Makeresho, Bolutu, wanafanya *Feasibility Study* pamoja na mifereji yake. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelia hapa na ushirika, Mheshimiwa Rais ametusikia. Unaona sasa ushirika umeimarika katika jimbo letu la Hai. Amefanya shughuli nyingi kwa kweli, sisi tunaenda kumlipa Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, nimefanya mikutano kata zote hivi karibuni kwenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Hai. Kata zote 17 wamenituma kwa hakika kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alichotutendea, ninyi mnafahamu Jimbo la Hai tulikuwa tumesimama miaka 15 hatukuwa na mtu anazungumza huku Bungeni, na ndiyo maana nimetumia muda mwingi kuuliza maswali mengi, kuchangia mara nyingi ili ku-*replace* ile miaka 15 ambayo hatukuwa na mwakilishi humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo matokeo ya Chama cha Mapinduzi kuongoza miaka mitano ndani ya Jimbo la Hai, kila mmoja anaona, barabara zimejengwa. Pale Boma Ng'ombe barabara za lami na taa juu, barabara ya Makoa – Mferejini kilometa 15; sasa hivi kuanzia Makoa mpaka pale kwa Mengi imewekwa lami na taa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za Mkandarasi yule, tumeongeza Mkandarasi mwingine. Hiyo barabara ina wakandarasi watatu; barabara ya kimkakati Boma Ng'ombe – Chekimaji – *TPC*, mkandarasi yuko *site*. Mheshimiwa

Rais ametuheshimisha, amefanya kazi kubwa, sisi ni wadeni wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo makubwa ambayo kwa hali ya kawaida hatukutegemea kwamba angeweza kufanikiwa. Leo Soko la kwa Sadala limeshatangazwa, shilingi bilioni 11.6; Soko la Mula tayari shilingi milioni 700 Mkandarasi ameshapatikana, na muda sio mrefu anaanza kazi, ametuheshimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* kilikuwa kimelala zaidi ya miaka 30, leo Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* kinafanya kazi. Waziri wa Mipango alinikubalia hapa, akasema wameweka kwenye mpango. Kile kiwanda tutakapomaliza suala la Makaa ya Liganga na chuma cha Liganga kule, tutumie Kiwanda hili cha *Kilimanjaro Machine Tools* kuzalisha chuma pale, watu wetu waweze kupata fedha. Ninakushukuru kwamba aliliweka kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwenye bajeti na hotuba zao, ninawapongeza sana. Moja, namna ambavyo wameweka mamlaka ya kusimamia wale wafanyabiashara wanatoka nje ya nchi. Ninaamini Mheshimiwa Waziri sasa ataenda kutembelea Kariakoo baada ya kupitisha bajeti yake kwa kishindo hapa, kuwaangalia wale wafanyabiashara wa Kitanzania; tuwalinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunaheshimu Diplomasia, ni kweli hatuwezi kuwa Kisiwa, lakini kazi zile zinazopaswa kufanywa na wageni, ziwe ni zile kazi kubwa, lakini hizi kazi ndogo ndogo ambazo ni za Watanzania ni lazima tuwalinde. Kile kinachoendelea Karikakoo na maeneo mengine pale hakikubaliki, kinarudisha nyuma uchumi wetu. Hata hivyo ninawapongeza kwa kupokea mawazo ya Wabunge na kuliweka kwenye utaratibu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine, naomba sana kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi wameweka kwamba tutajenga maghorofa ya kisasa pale eneo lile la *KIA* baada ya

mgogoro ule kukamilika. Ninawaomba sana, hili kwa kweli Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo asukume jambo hili, uchumi wa Jimbo la Hai sasa hivi tunatakiwa tuubadilishe kwa sababu ardhi yetu imekwisha, tutafute vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema hata kule kwenye ushirika, yale mashamba ya ushirika sehemu yake tuyatumie kujenga mahoteli ya kitalii. Jimbo la Hai tukilitumia kwenye utalii, linaweza kutusaidia sana. Ni pamoja na kujenga machinjio ya kisasa pale *KIA*. Pia ninawashukuru kwamba Mheshimiwa Prof. Mbarawa ameniahidi kwamba, atatupatia maeneo ya kulima kwenye eneo lile la Uwanja wa Ndege.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka ni kengele ya kwanza hiyo. Ninakushukuru sana kwa namna ambavyo kwa kweli mmefanya mambo makubwa kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kushukuru pia kwamba, Serikali imetazama, na mimi ni miongoni mwa watu ambao nimesema sana mara kadhaa, wazee wetu wastaafu wa Serikali mmeongeza kima cha chini mpaka 149.5% ya Pensheni yao, ahsanteni sana; lakini katizameni Maprofesa wa Vyuo Vikuu. Je, kwenye hili ongezeko, wale Maprofesa waliokuwa kwenye mfumo wa tofauti ya mafao yao waliokuwa wanafundisha Chuo Kikuu ambao kwa sasa hivi mafao yao ni madogo sana, hii *formular* inawahusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nina ombi la mwisho. Mtusaidie, kwani Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji wanafanya kazi kubwa sana. Ninajua *wage bill* inatengnezwa kulingana na pato la Taifa, lakini elekezeni sasa halmashauri zihakikishe zinalipa posho za Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji kwa wakati ili tuwa-*motivate* kwa maana hawa ndio wanaofanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Hai. Niwaambie, mimi bado ni kijana, nina nguvu, nina ari kubwa ya kuwatumikia. Oktoba kama ambavyo wameniahidi, nitarudi hapa kuendelea na haya ambayo tumeyapanga kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua nimebakiza kiporo cha shule chakavu, nimebakiza kiporo cha baadhi ya maeneo ya kujenga barabara, na maeneo mengine, niko tayari kuwatumikia kama ilivyo kawaida yangu. Ninawashukuru sana na ninaomba Mama Samia tukamlipe deni letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mheshimiwa Charles John Paul Mwaijage, ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii nami nichangie hoja ambayo iko Mezani leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya leo nikaweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pia ninashukuru kwamba kwa miaka hii mitano nimeweza kukaa Bungeni nikawatumikia wananchi wa Jimbo la Newala vizuri ipasavyo. Vilevile, ninaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupatia afya ili tukamalizie na yale mengine ambayo bado yalikuwa hayajafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli amefanya kazi kubwa katika nchi hii, na sisi wana Newala Vijijini ni wanufaika wa yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyatenda katika kipindi chake hiki alichoshika uongozi. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Newala Vijijini tulihamia kule tukiwa hatuna jengo la Utawala, hatuna nyumba za Watumishi, hatuna Hospitali ya Wilaya, na mambo mengi, hata umeme hatukuwa nao, lakini hayo yote leo yapo. Tunaendelea kumwombea Mheshimiwa Rais afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwaombe Wananewala Vijijini kwamba, ifikapo Oktoba basi na sisi tukatiki kwa nguvu. Mheshimiwa Rais anatakiwa kupewa mkono wa shukrani kwa yale ambayo ameyatenda katika Jimbo la Newala Vijijini. Basi tukamlipe kwa yale ambayo ametufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru Mawaziri wetu ambao wamewasilisha bajeti hii akiwemo Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wake, tunawashukuru kwa hotuba nzuri sana. Pamoja na Waziri wa Mipango na timu yake yote, tunawashukuru sana kwa utendaji kazi uliotukuka katika nchi yetu, tunaona Tanzania ambayo inasonga mbele, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nilisema kwamba sisi Wananewala Vijijini pia ni wanufaika? Tumenufaika kwa mengi, ukianzia umeme; pia tumetengewa fedha za maji, Mradi wa Makonde kule Newala Vijijini, Newala Mjini, Tandahimba pamoja na Nanyamba ni eneo ambalo ni kavu, maji ni ya shida, lakini kupitia Serikali hii tumepewa fedha, shilingi bilioni 84.7. Barabara ya uchumi kutoka Mtwara – Nivata – Tandahimba – Newala – Masasi, Wakandarasi wako *site,* na zaidi ya shilingi bilioni 230 zimewekezwa hapo, lakini yako mengi kama nilivyotangulia kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini yale yametekelezwa? Yametekelezwa kwa sababu Serikali ilifanya juhudi kubwa ya kutafuta fedha, fedha ambazo zimeenda kutekeleza yale ambayo leo tunayaona katika maeneo yetu. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuwekeza, na sisi Wananewala ni wanufaika wa miradi mingi ambayo imeendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia bajeti ambayo imewasilishwa, bajeti hii inalenga kuongeza mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo. Hongereni sana. Bajeti hii ikienda kama vile ambavyo imepangwa, maana yake sisi Wananewala Vijijini tunaenda kutoka pale tulipo, tusogee hatua nyingine mbele zaidi ili Newala na maeneo mengine ya Mtwara pamoja na Tanzania yaweze kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika maeneo machache. Nimeangalia hii bajeti katika vyanzo vyake vya ndani ni pamoja na mapato ya ndani ikiwemo *TRA,* na Serikali za Mitaa. Sasa hatuwezi kupata, ni lazima tujiwekeze zaidi kuangalia namna ambavyo tutapata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna zipo nyingi zikiwepo pia sekta ya miundombinu, ambazo ni sekta muhimu ili mapato ya Serikali yaweze kupatikana. Sasa hapa kwenye miundombinu nilitaka kuongelea kwa kifupi kuhusu barabara zetu ambazo zinasimamiwa na *TANROADS,* lakini pia zile ambazo zinasimamiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na barabara zetu za *TANROADS,* watu wa Kusini tunayo barabara ya kutoka Kibiti – Lindi kwenda Mtwara. Ni barabara muhimu sana, tumeiongelea muda mrefu, na Serikali inafahamu. Barabara ile lazima tuhakikishe inatengenezwa vizuri, na inajengwa upya. Tukiijenga upya, faida ni nyingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ikikamilika ipasavyo, hata mchango kwenye pato la Taifa utakuwa mkubwa sana, kwa sababu usafirishaji wa bidhaa za sokoni, mashambani na viwandani utakuwa rahisi. Kama bidhaa zitasafirishwa kwa urahisi maana yake ni kwamba biashara itafanyika, Serikali itakusanya mapato na mambo mengine yataenda kama hivi ambavyo tume-*plan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu tu kwa Serikali ni kwamba tunafahamu juhudi kubwa ambazo zimefanywa kuwanusuru wananchi wa kusini, kuweza kupita

katika maeneo yale hasa kile kipindi cha masika. Naomba tuendelee kuiangalia barabara ile kwa jicho la pekee ili iwe ni sehemu ya kukusanya mapato ambayo yataisaidia Serikali yetu kujiendesha yenyewe na kuepuka utegemezi kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchakavu wa barabara ile sasa hivi, unakuta hata wenye magari wanasita, kwa sababu ukisafiri, kwanza gharama za mafuta ni kubwa, kwa sababu tu ya hali ya barabara ilivyo. Pia mazao kwa sababu mengine yanaharibika huko njiani, lakini mazao kama ya Samaki, watu wanashindwa wakati mwingine kwa sababu tu ya uharibifu na vipuri vya magari vinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hali hiyo ikiendelea kwa muda mrefu tafsiri yake ni kwamba wenye magari watakata tamaa ya kupeleka magari, na hata mapato yetu ambayo tulitarajia tuyakusanye yanaweza yasifikie lile lengo kwa kupitia njia hii ya barabara kwa sababu tu ya hali ya barabara jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaomba sana Serikali tuendelee kuwekeza kwenye ile barabara, tuijenge ili usafirishaji wa bidhaa pamoja na wananchi uwe rahisi na matokeo yaje yawe chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda upande wa *TARURA*, zipo pia barabara zetu. Nashukuru sana Serikali imewekeza fedha nyingi kupitia *TARURA*. Tulikuwa hatuna barabara ya lami, wananchi wa Newala Vijijini, ukienda Makao Makuu ya Halmashauri sasa hivi lami ipo. Ukitoka Miyuyu kwenda Ndanda sasa hivi lami ipo. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali, lakini tuendelee kutenga fedha ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi na kupata huduma za jamii kwa urahisi zaidi, kwa sababu yapo mazao ambayo yanashindwa kwenye usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta Newala Vijijini hasa Kata za Mikumbi na Mkoma mazao yanaishia kule chini, mapato yanaenda Wilaya jirani badala ya kuja huku Halmashauri ya Newala. Kwa hiyo, tuendelee kuitengea bajeti *TARURA* ili waweze

kuboresha barabara zetu kwa ajili ya mazao pamoja na binadamu waweze kusafiri kwa urahisi na hatimaye tuweze kukusanya mapato kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia kwenye bajeti hii ambayo imesomwa, ukurasa wa 35 imezungumzia suala la Serikali kuendelea kutafuta wabia kwa ajili ya kujenga reli ya kusini ambayo inatoka Mtwara kwenda Mbamba Bay na matawi yake ya Liganga na Mchchuma kwa mpango wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuwatia moyo, tutafute hizo fedha kwa haraka, kwa sababu kama mradi ule utaenda kutekelezwa, bandari yetu ya Mtwara ambayo Serikali imewekeza fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 157 itafanya kazi muda wote wa mwaka, pia hata barabara zetu, kwa sababu sasa hivi makaa ya mawe yanapita kwenye barabara kwenda bandarini, barabara zinaharibika kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba suala hili liwekewe mkazo ili reli ya *SGR* ya Kusini iweze kujengwa na hatimaye kufungua milango ya kiuchumi kwa mikoa ya kusini kwenda katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutashukuru sana kama hili litafanyiwa kazi kama lilivyoelezwa ili nasi basi uchumi wa watu wa kusini uweze kupanda. Sasa hivi kuna maeneo kwa sababu ya hali ilivyo, yamesinzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaishukuru Serikali, imetupatia umeme. Ukienda Jimbo la Newala Vijijini, vijiji 107 vilikuwa havina umeme kabisa. Umeme ni ajira na kupitia ajira ile ya umeme wananchi wetu sasa wanaanza kupata vipato, na Serikali pia inakusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu, kwa kuwa umeme ule unakatikakatika kwa sababu ya miundombinu chakavu, ninaomba ile gridi ya Taifa iendelee kujengwa kama ilivyokusudiwa ili kuwakomboa wananchi wa Kusini ambao wanahangaika na kukatikakatika kwa umeme na hatimaye

tuweze kufanya uwekezaji kupitia viwanda. Pia wananchi mmoja mmoja waweze kufanya kazi zao na biashara zao kwa urahisi, na Serikali iweze kukusanya mapato yao, ili lengo la Serikali la kukusanya mapato kupitia mapato ya ndani kupitia *LGA's* basi yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwamba suala hilo la umeme limeweza kutimia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda, kengele ya pili imeshagongwa, kwa hiyo, naomba umalizie.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Nilikuwa na mengi, lakini naendelea kuishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuifanya. Sisi tupo sambamba tutaunga mkono Serikali na Chama, bega kwa bega. Nitamke tu kwamba na mimi naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawatakia Mawaziri wetu utekelezaji mwema na Serikali pia utekelezaji mwema wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, nilimtaja Mheshimiwa Charles John Poul, nikasema Kajege, lakini hapana; atakuwa ni Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani.

Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema sisi sote wakati tunatimiza wajibu wetu kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kuhudumia nchi yetu kwa upendo, na kwa kwa sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, kwa mara ya kwanza macho yangu yanaona *disbursement* ya bajeti tuliyoipitisha mwaka 2024 kabla mwaka haujaisha inafika zaidi ya 90%. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Hii inaonyesha jinsi gani ambavyo Mheshimiwa Rais na Serikali yake wanachokipanga ndicho ambacho wanakisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu, kaka yangu pamoja na msaidizi wake Mheshimiwa Chande ninawapongeza kwa moyo wa dhati kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya shilingi trilioni 50.2 ya *development* ilikuwa shilingi trilioni 16, mpaka sasa imeshatolewa shilingi trilioni 15 ambayo ni 95%, lakini ya kawaida ilikuwa shilingi trilioni 33.7, na mpaka sasa imeshatolewa shilingi trilioni 30 ambayo ni 90.8%. Nawapa pongezi sana Mawaziri, walichokileta Bungeni mwaka huu unaoisha, ndicho ambacho wamekwenda ku-*disburse* tena kwa 90% wakati mwaka haujaisha na wamefanya mambo makubwa; sitaki kuyarudia ya Kitaifa na katika Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimenifurahisha sana katika bajeti hii ambayo tunaimalizia, ni upande wa watumishi. Ukiachilia mbali barabara zetu, miundombinu ya shule ya madarasa, hospitali, na watumishi wa Taifa hili Mheshimiwa Rais amegusa maisha yao na maslahi yao katika bajeti hii inayoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini ikifika Oktoba watatiki, watumishi watakuwa wa kwanza kutiki, kwa sababu katika bajeti hii, shilingi bilioni 689, kulikuwa na malimbikizo ya watumishi, Mheshimiwa Rais amelipa fedha hizi tunampongeza kwa moyo wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipandisha mishahara, vyeo vyao, na malimbikizo yalikuwa shilingi bilioni 318. Watumishi zaidi ya 137,000 Mheshimiwa Rais aligusa maisha yao. Alilipa malimbikizo yao na Serikali iliwafikishia fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 300,000, akaenda mpaka shilingi 370,000, na sasa kwenye Mei Mosi ya juzi Mheshimiwa Rais ametangaza kima cha chini kitakuwa shilingi 500,000. Amegusa maisha yao. Sio hao tu waliopo kazini, Mheshimiwa Rais na Serikali, wamegusa pia wastaafu wetu kwa kuongeza kima cha chini cha *pension* toka shilingi 100,000 mpaka shilingi 250,000. Mheshimiwa Rais na Serikali yake, pokeeni maua ya watumishi, ninaamini haya maua ambayo tunawakabidhi watumishi tunaowawakilisha, watatiki Oktoba na watakuwa wa kwanza katika vituo vya kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa upande wa watumishi, kwa kuwa hawa watu wa *pension* tumewagusa vizuri, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha itusaidie basi kutengeneza mwongozo kwa wazee wale ambao sio watumishi wa ofisi zetu za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wazee ambao walikuwa wakulima, wapo mitaani, tunayo mikopo ya 10%, ile 4:4:2 kwa vijana, wanawake pamoja na walemavu. Ombi langu, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu na Serikali yetu sikivu iweke hata asilimia mbili kwa wazee ambao hawapati chochote, waingie kwenye dirisha la mikopo, ninaamini malalamiko yataisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye zile 4:4:2 naomba wazee wale tuwawekee na asilimia mbili, tunaweza tukapunguza moja kwa vijana, moja kwa wanawake tusiwatenge wale wazee ambao ni wa kiume. Maana wa jinsi ya kike wao watapata

kwenye dirisha la wanawake, wa jinsia ya kiume hawana dirisha la kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati tunawafurahisha hawa ambao walifanya kazi katika ofisi za umma, naomba sasa na hawa badala ya kudai wapewe *pension,* basi tuwape dirisha la kupata mikopo bila riba. Ninaamini Serikali yetu sikivu itachukua hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ni kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais wetu kwenye bajeti hii ambayo wameileta mbele yetu, bajeti ya shilingi trilioni 56.4. Ninapongeza maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia bajeti hii, nimeona Serikali imeenda kusamehe *VAT* katika viuatilifu na dawa ambazo wanazitumia wakulima wetu. Tumeona juzi Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Kilimo amenunua ndege kwa mara ya kwanza Tanzania, ndege ambayo itatumika kwenda kunyunyiza hizi *pesticides* pale ambapo wadudu wanasumbua wakulima wetu. Hongereni sana kwa Mheshimiwa Waziri, pokeeni maua yetu wakulima kwa kupunguza *VAT* katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali pia kwa upande wa mbolea ambayo inazalishwa ndani, na *VAT* imeondolewa, Mheshimiwa Waziri hongera sana hii ni jitihada za Mheshimiwa Rais na Serikali kupandisha kilimo chetu. Hii ni safari ambayo Mheshimiwa Rais ameshaanza, bajeti ya kilimo ni zaidi ya shilingi trilioni moja, na kipindi hiki pia imeendelea kuongezeka. Kwa hiyo, kusamehe *VAT* katika mbolea, pokeeni maua ya wakulima, naamini wakulima tutakuwa wa kwanza kwenda kutiki Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *VAT* pia kwenye mitungi ya gesi tunampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, maana yake nishati safi tunakwenda kutekeleza kwa vitendo katika kuweka ruzuku na kuondoa *VAT* kwenye mitungi ya gesi na matenki ya gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maamuzi hayo ya Mheshimiwa Waziri ambayo ametuletea sisi tuyabariki, kwani yanakwenda kugusa maisha ya Watanzania wa hali ya chini kabisa. Ndiyo maana tunapongeza maamuzi haya na tunayaunga mkono. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, maana amejibu kero za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa wafanyabiashara, nimeona *Service Levy* imepunguzwa kutoka 0.3 kwenye pato ghafi mpaka 0.25 ya pato ghafi, kwa lengo ni kuboresha mazingira ya biashara. Kwa kweli kwa hili tupongeza sana. Mimi natoka jimbo la mjini ambapo tuna wafanyabiashara. Hili la *Service Levy* lilikuwa likileta kizungumkuti, na limekuwa likiwasumbua wafanyabiashara wengi. Nimefurahi kuwaona Serikali imeanza kupunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tena wakati wanafanya *calculation* ya hii kodi, wataalam wetu wa Halmashauri wapatiwe mafunzo ya kutosha, na hiki chanzo kifanye vizuri, kwa sababu ni miongoni mwa chanzo ambacho tukiongeza nguvu ninaamini tutakusanya fedha nyingi sana. Pamoja na kwamba tumepunguza, tumewaonea wafanyabiashara wetu huruma katika kodi hii, Serikali imesikia kilio chao, lakini tuongeze nguvu katika makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wafanyabiashara tena ambao tunawawakilisha katika Majimbo yetu, wapokee salamu za Mheshimiwa Rais na bajeti hii, kwa kupunguza *Hotel Levy* kutoka 10% mpaka asilimia mbili. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hongereni sana kwani kupungua kwa hii *Hotel Levy* kutoka 10% mpaka asilimia mbili, wafanyabiashara wadogo wadogo tunaowawakilisha sisi Wabunge wao, tumelipokea kwa moyo wa upendo. Naomba wafanyabiashara sasa tuongeze nguvu katika kulipa kodi hii kwa sababu Mheshimiwa Rais amesikia maombi yetu ya kupunguziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kwa kupunguza ada ya usajili wa

pikipiki. Tunao vijana wetu wengi sana ambao wanajihusisha kwenye biashara hizi za pikipiki. Wamepunguza kutoka shilingi 340,000.00 mpaka shilingi 170,000.00 kwa mfululizo wa miaka mitatu. Ahsanteni kwa niaba ya bodaboda wale, pia mmepunguza kodi ya mapato toka shilingi 290,000.00 mpaka shilingi 120,000.00 ambayo ni *Preservative Tax* ambayo italipwa wakati wa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba kwenye hili Mheshimiwa Waziri kama kuna mtu hawezi kulipa wakati ule wa usajili, basi mui-*break down* kwa *quarter* zile nne badala ya kulipa zote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha, atupatie ufafanuzi kwa sababu ukurasa wa 90 wa bajeti amesema hivi, magari binafsi ya kukodisha amesema utaratibu wa sasa, pikipiki ya miguu miwili ilikuwa inalipa shilingi 65,000.00, utaratibu anaopendekeza kwamba hawatalipa, akasema namna mbili; pikipiki ya miguu mitatu, maana yake bajaji pamoja na zile guta walikuwa wanalipa shilingi 120,000.00 anapendekeza kwa utaratibu wa sasa kwamba hawatalipa chochote, hakuna anachokipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Mheshimiwa Waziri amesema amepunguza kutoka shilingi 290,000.00 mpaka shilingi 120,000.00. Nilikuwa naomba aweze kutuweka kwenye njia moja tuweze kufahamu ipi ni ipi? Ni hatua nzuri sana. Hajaishia hapo, amepunguza ada ya leseni ya uendeshaji pikipiki kutoka shilingi 70,000.00 mpaka shilingi 30,000.00. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais, vijana wa Kitanzania tunaowaongoza wanasema ahsanteni sana kwa kuona hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kubwa zaidi ni hili la Kifungu cha 3(4) cha Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara Sura Namba 101 ambayo umekwenda kuelekeza mamlaka zinazokusanya leseni wasifungie biashara za wafanyabiashara. Mheshimiwa Rais ahsante sana kwa hili, Mheshimiwa Waziri ahsante sana, kifungu hiki mmekwenda kuelekeza kwamba wafanyabiashara

wasifungiwe biashara zao. Kwa mantiki hii watafanya biashara zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninaomba maeneo ya kuongezea nguvu. Mheshimiwa Waziri ikiwapendeza tuongeze nguvu katika madarasa ya shule za msingi ambayo mpaka sasa tumejenga 155,000. Ikitupendeza tuongeze nguvu kwenye fedha za *TARURA*. Kilomita za changarawe 44,000, na kipindi hiki fedha zimeenda, naomba tuongeze nguvu hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwapendezeni tuongeze nguvu sasa kwenye *REA*. Najua shilingi bilioni 574 zimetumika, lakini kwa mtu mmoja mmoja, umeme jazilizi, naomba tuongeze nguvu. Ikitupendeza zaidi, kwa kuwa hospitali za kanda na shule zimejengwa, tuangalie gharama za matibabu katika hospitali za kanda na za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwapendeza zaidi Mheshimiwa Waziri tuongeze nguvu kwenye ujenzi wa masoko makuu na machinjio katika Halmashauri za Miji na Manispaa. Vinginevyo pokeeni maua yenu, tunawaombea, Babati Mjini hatuwadai, ni vitu vidogo ambavyo ni vya kawaida na vipo kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. tuwatakie kila la heri Waheshimiwa Mawaziri, Oktoba tunatiki, kura za Mama zinatosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul. Nilimwita Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Ninakubaliana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, nakubaliana na Bajeti Kuu kama alivyoiwasilisha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ‘*omwana wo-mukazi*’.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia ukurasa wa 33 mpaka 67 wa Bajeti ya Waziri wa Fedha, anapozungumzia mafanikio ya Serikali, maelezo yake yanaakisi hali halisi tuliyoiacha huko nyumbani, tuliyoiacha *site,* kazi imefanyika, kazi imefanyika kuliko uwezo wa mtu wa kawaida kufikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja bajeti hii ila naomba twende na marekebisho au mapendekezo nitakayoyatoa. Jambo la kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba aliyoitoa wakati anazindua ile programu ya kuchanja mifugo na utambulisho wa mifugo aliyoifanya juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, tuliyoyajadili kwenye Bajeti ya Mifugo, Mheshimiwa Rais anasema ndiyo uelekeo wake, yaani yale mapendekezo yetu ya kuongeza uwezeshaji wa sekta ile ya mifugo, Mheshimiwa Rais amesema ndiyo uelekeo wake; nimemsikia kabisa nikiwa nimetulia. Kwa hiyo, tuliyoyapendekeza Mheshimiwa Rais ameshayaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza mchangiaji aliyepita, Mheshimiwa Rais ukimwambia kitu yeye anatekeleza, ilimradi kinaendana na dira pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa Fedha sijui kama wataalamu wake wapo *standby* kuandika, kwa sababu tamko la Mheshimiwa Rais ni maelekezo. Ukisoma katika ukurasa wa 62, maboresho na tozo kwenye sekta ya uvuvi, kumekuwepo na msukumo wa kuwataka wananchi wafuge samaki kwa kutumia vizimba. Katika utaratibu wetu wa kuhamasisha sekta hiyo tuliweka tozo kwa samaki wanaotoka nje makusudi. Ulikuwa ni mjadala mkubwa sana, tukaweka dola 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde Mheshimiwa Waziri asipunguze kiasi hiki. Tutaelewana akisema atatoza dola tatu, lakini ninamwomba chonde chonde asipunguze. Kitendo cha kuzuia wale samaki wanaotoka nje, kimewafanya wafugaji

hasa Sekta Binafsi waweze kuhamasika, hivyo wahamasishwe kusudi waweze kufuga, na wameanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Serikali shilingi bilioni 13 zilizowekwa kwenye ufugaji wa samaki zimeanza kuleta matunda. Ninachotaka kuieleza Serikali yangu, suala la ufugaji wa samaki kwa vizimba halihitaji mgeni. Hii ni sekta ambayo vijana wa Kitanzania ukiwawezesha na ukawaelekeza, wataweza kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa mimi sioni kwa nini tulete samaki kutoka nje ili tuweze kuwadhoofisha hawa. Ukienda katika gharama *(cost wise)* samaki wale wanaoletwa kwa hadhi yake, kwa ubora wake ni samaki wa shilingi 3,000.00 mpaka shilingi 4,000.00. Samaki wazuri wa *tilapia* au mboju ni shilingi 8,000.00 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uwaache Watanzania wale vitu vizuri. Mtu ajinyime ale mboju, ale *tilapia*, wenye ubora mzuri kuliko kuleta hao samaki ambao bahati mbaya wamekaa kwenye friji miaka miwili, miaka mitatu kuja kuwalisha Watanzania. Wale samaki wabaki kule, sisi tutafuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo, kwa nini hatuzalishi samaki wengi Ziwa Victoria? Ni kwa sababu ya uharibifu wa Ziwa. Tumependekeza kwenye Bajeti ya Wizara ya Mifugo kwamba waweke Mamlaka ya Udhibiti wa Ziwa ili tuweze kupata samaki wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Musoma alizungumza juzi hapa kwamba viwanda vyako vyote vya Musoma havifanyi kazi. Mwanza ni *under capacity*, Kagera, Bukoba ni *under capacity,* lakini ni aibu upande wa Uganda, viwanda vya samaki vinashamiri na wanaendelea kupata kazi. Hii ina maana wanatengeneza ajira, sisi tunaharibu ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu Mheshimiwa Waziri nina imani naye na ndiyo maana nikaomba watendaji wake wawe *standby* wasikilize ninazungumza nini? Niko tayari

kuwaletea vielelezo, kwa nini tunataka kufuga samaki? Tunataka kufuga Samaki, siyo mboga tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanataka kuagiza samaki, eti kuleta chakula hapa, hapana. Sisi tunafuga samaki ili kutengeneza ajira, kwani sisi tatizo letu ni ajira. Mtu akishapata ajira, kuhusu atakula nini, ni juu yake. Ufugaji wa samaki kwa watoto wazawa na wananchi wazawa wa nchi hii, tunatengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapo-*import,* una *export* ajira za Watanzania. Katika hili Mheshimiwa Waziri niko chini ya miguu yako, usichezee ajira za wapiga kura, usichezee ajira za Watanzania, ni hatari. Tuwape watoto ajira zetu waendelee kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maelezo ya kina, ninaweza kulieleza hilo kwa mapana marefu. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais. Tunapotafuta rasilimali za kujitosheleza ni Sekta ya Mifugo pamoja na Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza na ikimpendeza Mheshimiwa Waziri atakuwa hapa mwezi Desemba tunapopitia bajeti, aweke fedha za kibabe katika sekta ya mifugo kusudi tuweze kufuga wanyama mbalimbali; mbuzi, kondoo, na ng'ombe ambayo ni masoko yaliyoko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati tunasherehekea *Eid* ya kuchinja, ilikuwa ni *deal* kubwa kupata mbuzi. Mbuzi kwetu wamekwenda mpaka shilingi 250,000.00. Ukanda wote wa Pwani na Tanga wamekosa mbuzi. *The market is ready for us,* na niliwahi kusema katika Bunge hili kwamba soko letu linalotusubiri ni dola bilioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi na Mifugo inaweza kufanya vizuri kuliko Sekta ya Madini, na hili ni *renewable.* Madini yanaisha, lakini mifugo, kwa sababu tuna nyasi, tuna ardhi tunaweza kuitekeleza. Mheshimiwa Waziri, chonde chonde, ikibidi

nikuletee hesabu, kwa sababu na mimi nilisoma hesabu, lakini zile ngumu ngumu, nije nikuoneshe hesabu, hapo msiguse.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nimpongeze kidogo Mheshimiwa Waziri kwani amepunguza kodi kwenye viuatilifu. Mimi hoja yangu ni je, lile punguzo litamfaidisha mlaji? Ile punguzo ya 18%, mlaji wa mwisho atafaidika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipunguza bei ya mafuta, lakini yule mlaji wa mwisho hapati ile *benefit*. Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba atapunguza *VAT* kwenye mitungi ya gesi. Tujiulize kama Taifa, kwa nini Tanzania hatumwambii yule anayetengeneza mitungi kule anakoitengeneza aje hapa Tanzania aitengenezee hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 nilikwenda Harare, Zimbabwe kukagua usalama wa mitungi ya gesi, nilikuta wana viwanda vya kutengeneza mitungi ya gesi. Kutengeneza mitungi ya gesi *is very simple.* Siyo sawa na kutengeneza makombora ya *Panasonic*. Ni kitu rahisi. Kwa nini msiwaambie hao wanaoleta mitungi waitengeneze hapa kusudi tutengeneze ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ninarudia tena. Sisi biashara yetu ni kutengeneza ajira. Mtu asikudanganye, tengeneza ajira, mambo ya kodi na mambo mengine yatakuja baadaye. Wawekee masharti katika bajeti yako 18% iwe kwa wale watakaotengeneza mitungi hapa. Atakayeagiza mitungi alipe *VAT,* lakini atakayetengeneza hapa *VAT* iondolewe. Lazima tutengeneze ajira. Mimi ajenda yangu 2025 mpaka 2030 ni kutengeneza ajira, wenyewe watajua baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *VAT* kwenye nguo za pamba. Ninampongeza kwa kutoa *VAT* kwenye pamba, lakini na yenyewe lazima tuhakikishe tuwe na usimamizi kuhakikisha kwamba ile nguo inayolengwa kupata *exemption* ya 18% ni nguo iliyolimwa hapa. Watu ni wajanja, na Waziri najua ni mtaalamu wa kupambana na wajanja, lakini lazima tudhibiti hizi fursa. Haya

mambo yakitengenezwa, *VAT* katika pamba, maana yake watu watalima sana na tunatengeneza ajira sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mafuta ya kula ya mbegu. Mafuta ya kula kama alizeti yanaweza kutoka nchi nyingine yakaja hapa yakapata hiyo *VAT exemption*. Lazima tuhakikishe ni mafuta ya mbegu zilizolimwa hapa lakini kwenye alizeti kwetu Singida ilikuwepo fursa ya ku-*export* haya mafuta ya alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta ya alizeti ni *royal product* inaliwa na ma-*monarchy*. Siyo mafuta ya kula watu wa kawaida, na soko lililokufa Ulaya, *task* ninayoitoa, tutafute hili soko la Ulaya lilikwenda wapi? Ilikuwepo *opportunity* ya ku-*export* Ulaya. Ninataka mafuta ya alizeti yawe *exported* hapa, lakini haya yatakapopata *exemption,* lazima watu wa *TRA* wavae sura ya kazi wahakikishe kwamba mbegu hizi ndizo zilizolimwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono wazo hili la kusamehe *VAT* kwenye matairi ya trekta na ninaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwamba itakuwa mnakodisha matrekta kwa ruzuku, hilo ni wazo jema. Nimemwona mtumishi amevaa sura ya kazi huko alikokuwa anasema atakuwa anatoa matrekta na amenihakikishia kwamba na kwangu Wilaya ya Muleba atapeleka matrekta ya kutosha kusudi tujifunze na sisi kulima kwa trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna suala la gesi. Unasema utatoza ushuru kwenye tani ya ukaa itakayozalishwa kwenye gesi asilia na itakayozalisha mkaa wa mawe, ninaomba kutofautiana. Niliomba mwaka 2024, tukakubaliana kwamba hii sekta ya gesi muiache kwanza tuingie. Watu wakishaingia, tutakuja kutoza. Ngoja niwaambie, dunia imevaa bukta na miwani ya mbao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi asilia ni usalama wa nchi. Mmesikia watu wanarushiana makombora, mmoja akasema kwenye ule mfereji wa Canal anataka kuhakikisha kila meli

itakayopita itapigwa. Kuwa na gesi na kuwa na magari yanayotumia gesi asilia ina maana *we are safe*. Wakipiga meli zote zisije, haya malori yatatembea vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu, usiweke kodi yoyote, lakini hamasisha malori yote, hakikisha mabasi, haya mabasi mazuri ya Katarama, Kaizirege, Abood, *SATCO* na Shabiby yatumie gesi asilia, kwamba itakapotokea wale wanaopigana makombora wamezuia meli za mafuta zisije, sisi tutumie gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu gesi hii siyo lolote. Gesi ni usalama wa nchi. Watu hawalizungumzi kwa *capital letter,* lakini *I want to tell you,* kama una gari inatumia gesi na wale wajanja wanaopigana makombora wakaanza kupigana makombora, wewe na gari yako utatembea kwa sababu gesi iko hapa hapa. Ninakuomba chonde chonde, huo ushuru unaotaka kuweka kwenye gesi, tulia kwanza, tafuta vyanzo vingine na niko tayari kufanya *homework* kuanza kusaidiana na wataalamu wake kutafuta vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha kwanza, tuweke ushuru kwenye samaki wanaotoka nje. Mheshimiwa Waziri ongeza dola tatu ziwe saba, samaki wasitoke nje kuja hapa, lakini kwenye gesi usiguse.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, kwenye makaa ya mawe, sisi tuna-*export* makaa ya mawe kwenda Rwanda, Burundi, Kenya, na Uganda. Sasa unapoweka ushuru, unawazuia wale watu wasi-*export*. Wale wanaochoma mkaa na kuchafua hali ya hewa huko kwao ndiyo walipe ushuru wa *carbon*. Ushuru wa *carbon* sisi hatuchomi mkaa wa mawe, lakini mkaa wa mawe ndugu yangu, huu mnaoweka mnauongeza bei kusudi usiuzwe, mtautumia lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wababe wa vita wakati wowote wanaweza kutangaza, tusitumie mkaa wa mawe. Mtaufanyia nini? Kwa hiyo, punguza hizo kodi na tozo kwenye rasilimali hii

ambayo hatujui usalama wake, wapelekee wanaotaka kuchoma waweze kuchoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitaandika kwa maelezo. Hotuba yangu ilikuwa ni ndefu sana, lakini hayo ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono bajeti hii. Mambo ni mazuri, ninaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kutengeneza Bukoba *International Airport* pale Kiabajwa. Pia, ninaiunga mkono bajeti inayokuja, kwa sababu inakwenda kutengeneza ile *Ngono Irrigation Mega Project* Wilaya ya Muleba, ahsanteni sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles John Mwijage kwa hotuba. Nilimwita Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti Kuu ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana mawaziri wote wawili. Bajeti hii ni ya Watanzania na imelenga kugusa maeneo ya msingi kabisa ambayo ni maisha ya kawaida ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa akiendesha nchi yetu tangu aliposhika usukani mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nitumie fursa hii, kwa sababu ninajua hii inaweza kuwa ndiyo hotuba yangu ya mwisho kwa Bunge hili la mwaka 2020 – 2025, nakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi binti mdogo niliyekuwa na umri wa miaka 24 kutokea familia ya kawaida kabisa kuja kuwawakilisha vijana wenzangu na kuzungumza, sauti yangu ikasikiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kwangu imekuwa ni heshima kubwa siyo kwangu tu, bali kwa familia yangu na kwa vijana wote wa Kitanzania. Imekuwa ni imani kuwa Chama cha Mapinduzi ni cha wote. Yeyote anayetaka fursa ndani ya Chama cha Mapinduzi, fursa hiyo inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuushukuru sana uongozi wangu wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi, Mwenyekiti wangu, Mohamed Ali Kawaida; Makamu Mwenyekiti, Rehema Sombi na Katibu Mkuu wetu Jokate Urban Mwegelo, kwa ushirikiano mkubwa pamoja na viongozi wote; wenyeviti, makatibu wa mikoa na wilaya zote kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa tukifanya kazi pamoja kuhakikisha ajenda za vijana zinasukumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipongeze na kulishukuru sana Bunge hili Tukufu lakini mahususi kabisa Spika wetu wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kunipa nafasi kwenda kuwakilisha katika Bunge la Afrika, Bunge la Kimataifa. Binti mdogo, lakini sauti imesikika kupitia Bunge hilo ndani ya Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wamezungumza hapa, na Wabunge wengi wa majimbo kwamba inawezekana wao majimbo yao yamependelewa zaidi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini mimi ninasimama hapa kusema, ninahisi sisi vijana tumependelewa zaidi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi hiki cha miaka minne ambayo amekuwa madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipiga kelele za muda mrefu juu ya matatizo na changamoto zinazokumba kundi hili mahususi kabisa la vijana, lakini tumepata majibu na matokeo makubwa chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu katika Sekta ya Elimu tumepiga kelele muda mrefu kwamba changamoto namba

moja inayomfanya kijana wa Kitanzania haajiriki ni changamoto zilizopo katika mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyozungumza hapa tumepitisha sera mpya ya elimu, na mitaala mipya ambayo inakwenda kutoa majibu kwa changamoto zote za kijana. Pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia tu, alituita vijana katika Mkoa wetu wa Mwanza, akatupa maelekezo, na akatoa maelekezo kwa Serikali na maelekezo hayo yametekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa ilikuwa ni kilio cha muda mrefu, vijana wanaokopeshwa mikopo ya vyuo vikuu walikuwa wanapata changamoto sana katika zile 6% za *retention fee* na 10% za adhabu ya kuchelewa kulipa mikopo ile. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifuta vyote hivyo na leo hii hakuna tena mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa, katika elimu yetu tuna ongezeko kubwa la bajeti katika Mikopo ya Elimu ya Juu kutoka shilingi bilioni 484 mpaka shilingi bilioni 787, na hiyo imeongeza udahili mkubwa sana wa vijana wanaokwenda kusoma katika vyuo vikuu. Pia, hajaongeza tu fedha, ameongeza pia wigo wa vyuo ambavyo vitapokea mikopo kuingiza pia vyuo vya elimu ya kati ambavyo vinatoa zile fani za kipaumbele hasa hasa fani za sayansi. Katika kuongeza tu wigo huo, zaidi ya vijana 7,800 wamenufaika na mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa, wigo wa elimu bure umeongezeka siyo tu kuishia kidato cha nne mpaka kidato cha sita, maana yake ni kwamba mtoto wa Kitanzania anasoma kuanzia darasa la kwanza mpaka *form six,* elimu bure. Vilevile, akiingia chuoni anapata mikopo na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongeza *boom* kwa wanachuo kwenda mpaka shilingi 10,000.00 kwa siku jambo ambalo tumeshukuru na tunaendelea kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa, katika elimu yetu ya Tanzania, kuna suala linaitwa *Samia Scholarship*.

Mabinti wa kike ambao wanakwenda kusoma sayansi wanaenda kupewa *scholarship* ya 100% kwa ajili ya kujiendeleza kielimu. Si hivyo tu, amejenga shule 26 za sayansi za watoto wa kike katika mikoa yote ya Tanzania Bara ili kuendelea kusukuma au kuweka msukumo katika elimu ya sayansi kwa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia hajamsahau mtoto wa kiume, amejenga shule saba katika kanda zote za watoto wa kiume wanaosoma sayansi ili kuhakikisha maendeleo yanakwenda sambamba kwa watoto wote wa kike na wa kiume. Tuseme nini sisi vijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja katika suala la elimu, mimi peke yangu nimesimama hapa kama mwakilishi wa vijana, sijawahi kuacha kuzungumzia changamoto ya ajira, lakini majibu tumeyapata. Pia, mimi siwezi kuzungumza sana juu ya Mabunge mengine kwa sababu mimi ni mbunge wa kipindi cha kwanza, lakini ninakiri kusema, hoja zote nilizosimama kuzungumza ndani ya Bunge hili zilizogusa maslahi ya vijana, zimepata majibu. Kama hazijapata majibu, zimeanza kufanyiwa kazi na nimeshirikishwa moja kwa katika kuanza kufanyiwa kazi kwa hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa, vijana wenzangu ni mashahidi, kwa miaka saba nchi hii ilikuwa haijatangazwa ajira hata moja, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kaingia, ajira zaidi ya 45,000 zimetangazwa na vijana wameingia Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia diplomasia yake ya uchumi, tunavyozungumza sasa, zaidi ya vijana 7,000 wameshatafutiwa kazi katika nchi za nje ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga nazo mazingira mazuri ya mahusiano ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tulitumia kuomba kura mwaka 2020 iliahidi ajira 8,000,000 kwa Watanzania. Hata hivyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia kuongeza uwekezaji na ajira kupitia Sekta Binafsi, leo hii ajira zaidi ya 8,084,000

zimeshatolewa kwa Watanzania. Hii ni zaidi ya 100% ya ahadi ambayo tumetoa. Tuseme nini sisi vijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la uwezeshaji wa vijana kiuchumi, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwaka 2021, mifuko ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ilikuwa ina fedha kiasi cha shilingi bilioni 945 tu. Leo hii tunavyozungumza, mifuko hiyo ina fedha kiasi cha shilingi trilioni 3.5 kwa ajili ya kuwezesha wananchi kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza Wabunge wote wa majimbo tunafahamu kwamba, kulikuwa na changamoto sana ya mikopo ile ya asilimia kumi. Mikopo ile ilikuwa inatumika kisiasa, na yale makundi ambayo yalikuwa yanatakiwa kupata fedha hizo yalikuwa hayapati inavyostahili, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia akaweka utaratibu mzuri na bora ambao sasa hivi mikopo hiyo inakwenda moja kwa moja kwa watu waliokuwa wanastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, wakati anatoa hotuba yake katika Bunge hili, aliwaahidi Watanzania kwamba, nitahakikisha mikopo ya kwenye kilimo inashuka kwa kiwango cha *single digit interest rate*. Tunavyozungumza, leo hii wakulima watatoa ushahidi kwamba benki zetu; si Benki ya Kilimo peke yake, lakini mpaka benki za kibiashara zinatoa mikopo kwa asilimia tisa tu kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais haijaishia hapo, juzi juzi hapa tumeanzisha Benki ya Ushirika ambayo inakwenda kumgusa mkulima moja kwa moja, kumwezesha katika sehemu ambazo alikuwa hawezi kuingia katika benki za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala la kilimo, sisi vijana *Program* ya *BBT,* ajira zaidi ya 111,000 zimezalishwa na vijana zaidi ya 686 wako shambani sasa hivi wanaendelea na kazi katika *program* hii. Tukiongelea *BBT* ugani, tunaongelea zaidi ya vijana 1,200 Maafisa Ugani ambao wako kwenye pamba katika

mikoa yetu ya Kanda ya Ziwa wanawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji katika zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji huo umeongezeka na mwaka huu utakuwa ni mwaka wa kwanza kuwa na uzalishaji wa juu zaidi katika zao la pamba kuliko mwaka mwingine wowote. Zote hizo ni juhudi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumzia sasa, mapinduzi katika kilimo ambayo moja kwa moja yanamgusa kijana, tunazungumzia ruzuku katika mbolea, mbegu na matrekta. Leo hii bajeti inatuonesha, kuna matrekta zaidi ya 10,000 ambayo tunategemea kuyapokea, pia, yatatolewa kwa ruzuku. Kuna msamaha wa kodi wa vifaa mbalimbali kwenye kilimo katika bajeti hii ambayo imewasilishwa kwetu. Yote haya ni mambo ambayo yanakwenda kumgusa kijana moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia suala zima la mitandao ya kijamii, tulipiga kelele hapa ndani kwamba, sisi vijana wengi kwa sasa hivi katika dunia hii ya utandawazi, tunajiajiri kupitia mitandao ya kijamii. Gharama ya bando, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisikia na kujibu, mwaka 2021 wakati anaingia *MB* moja ilikuwa inanunuliwa kwa shilingi 25 au shilingi 24, leo hii tunavyozungumza *MB* moja inanunuliwa kwa shilingi 9.4 tu. Hilo ni punguzo na ni nafuu kubwa sana kwetu sisi vijana.

Meshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau makundi mahususi kabisa ya vijana, leo hii tunavyozungumza bodaboda ni sehemu ambayo vijana wengi sana wanajiajiri. Amesikia kilio chetu na kwa kiwango kikubwa kwa kweli, tunashukuru. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani, tulipiga kelele kuhusu faini za bodaboda, akashusha kutoka shilingi 30,000.00 mpaka shilingi 10,000.00 lakini leo katika bajeti hii iliyowasilishwa hapa ya mwaka 2025/2026 imekwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipiga kelele kwamba vijana wengi wanapata ajali kwa sababu hawakupata mafunzo na hawana leseni, kwa sababu, gharama ilikuwa juu. Leo hii

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba amekuja na suluhisho, badala ya shilingi 70,000.00 kijana atalipa shilingi 30,000.00 tu, kwa ajili ya kupata leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wameshusha gharama ya *registration* ya bodaboda, badala ya kulipa shilingi 340,000.00 kijana atalipa shilingi 170,000.00 tu. Wameshusha pia gharama ya kodi ya mapato kwenye pikipiki, badala ya shilingi 65,000.00, sasa hivi kijana halipi na badala ya shilingi 120,000.00 kwenye bajaji, halipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya yote haya, katika bajeti hii ya mwaka 2025/2026, ameona kilio chetu sisi vijana tuliotaka kujiajiri katika sekta binafsi, ameongeza ushuru katika bidhaa mbalimbali zinazotoka nje kuingia ndani, ili kumpa nguvu kijana anayetaka kujiajiri katika viwanda kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea ushuru wa mafuta ya kula yanayotoka nje, umeongezeka. Tunaongelea ushuru wa *sausage,* viberiti, bidhaa zote kubwa na sabuni, ambapo kijana wa Kitanzania ana nafasi ya kujiajiri. Kwa sasa hivi kijana amepata nafasi kwa sababu, masoko yamelindwa bara bara kabisa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa hivi, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya yote, hayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa wakili msomi, Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika chache tu.

**MWENYEKITI:** Ninaomba umalizie.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitimisha.

**MWENYEKITI:** Maana yake, yako mengi ya kuongea kuhusu Mheshimiwa Dkt. Samia.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anayafanya mambo hayo machache tu niliyoyasema kati ya mengi kwa vijana, hakuacha ajenda kuu za Kitaifa. Ndani ya kipindi cha Mheshimiwa Rais, leo hii tunaongelea mambo makubwa sana yamefanyika; Sensa ya Watu na Makazi, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, zoezi la Anuani za Makazi na miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho tunakwenda kuzindua daraja letu la JPM Mkoani Mwanza, tunaongelea miradi ya *SGR,* tunaongelea kuendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa fedha zetu za ndani, na sasa katika Uchaguzi Mkuu pia tunakwenda, maana yake huo ndiyo uhuru wa kisiasa tunaouzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi niseme tu kwamba, sisi vijana wa Tanzania tunashukuru sana kwa yale aliyotufanyia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuna imani naye. Tutapambana kuhakikisha mwaka huu 2025 kura zinapatikana za kishindo, ili yale tuliyoahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2025 na 2030 yatekelezwe tena kwa kishindo kama alivyotekeleza sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na Oktoba tunatiki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mbunge wa Vijana, Mbunge machachari. Sasa namwita Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi. Pia Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi nami niweze kuchangia bajeti yetu ya Serikali ya mwaka 2025/2026. Ninatambua kabisa katika mpango wetu wa tatu wa miaka mitano, huu ndiyo mwaka wa mwisho kwa maana ya 2025/2026 ukiwa imeanzia mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwa kweli, tutumie nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri wetu wote wawili, kaka zangu, wajomba zangu, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo pamoja na Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Hassan Chande na kwa umuhimu sana wataalamu wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango kwa kazi nzuri, ambayo kwa kweli, wameendelea kuifanya kwenye nchi yetu. Sisi kama Wabunge tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu tu kueleza juu ya mafanikio, kama wengine walivyosema. Ndani ya mafanikio, kama ipo changamoto ya kushauri, ni ndogo, ambayo itakuwa imejielekeza moja kwa moja kwenye Jimbo la Kibamba, lakini kwa mafanikio ni lazima niseme ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Nchemba amesema kwamba, katika kipindi chetu chote hiki cha miaka mitano kwenye bajeti hii ya mwisho tumeona ongezeko kubwa la uchumi, pato la Taifa kutoka 4.8% hadi 5.5% kufikia mwaka 2024. Hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuongezeka kwa mapato ya kodi kutoka shilingi trilioni 20 hadi shilingi trilioni 29.83, mwaka 2024/2025 inaenda sambamba na mapato au makusanyo ya kodi kwa mwezi. Unaweza ukaona mwaka 2021 ilikuwa takribani 1.7, lakini mwaka 2024 imeenda mpaka kufikia shilingi trilioni 2.83. Haya ni mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mabadiliko mengi sana ya watendaji wetu kwenye Taasisi yetu ya Mamlaka ya Mapato,

lakini ninawapongeza sana, hata huu uteuzi wa mwisho wa *CPA* Yusuph Juma Mwenda kwa kweli, ni wa wazi kabisa. Ni kijana mchapakazi, mwenye historia nzuri. Tunatambua sana amekuwa Meneja wa Walipakodi Wakubwa kwa miaka mingi na baadaye ameenda kutusaidia kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kusimamia mapato, na mwisho Mheshimiwa Rais ameona anayo sababu ya kuja kusimamia upande huu wa Tanzania nzima. Tunamshukuru sana kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la ziada kwenye upande mzima wa kibajeti, tumeona ongezeko la bajeti kuu kutoka shilingi trilioni 34 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 57.04 mwaka 2025/2026. Hii ni kazi nzuri inayofanywa na hawa Mawaziri. Kupandisha bajeti siyo kazi ndogo, ni lazima uone makisio ya maoteo kama yanaweza kufika. Nje ya hivyo, huwezi kuongeza bajeti mwaka kwa mwaka. Kwa hiyo, ninaendelea kuwapongeza Mawaziri wangu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kiweledi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mafanikio kwenye sekta ya afya; pamoja na mambo mengine, lipo hili la kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023. Hili ni jambo kubwa sana na Watanzania ni lazima walione. Huduma ya afya tukiipata kwa *level* ya *universal* inaweza ikatusaidia tulio wengi. Wengine wanaumwa na wengine hawaumwi; kuliko ambavyo ipo sasa ambapo bado ni mtu mmoja mmoja na gharama zinakuwa kubwa, zinaweza zikayashinda hata mashirika yetu ya kutoa huduma ya bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la ziada kwenye eneo hili, tumeona kupungua kwa vifo vya mama na mtoto na hata kupungua kwa vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano. Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kwenye bajeti yake ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka, eneo la elimu utaweza kuona ongezeko la shule nyingi sana za msingi na sekondari. Kwenye Jimbo la Kibamba tumejenga shule 13; sita za msingi mpya kabisa na saba za sekondari mpya. Pia zipo zile 26 ambazo Mheshimiwa Rais alizijenga katika kila Mkoa ambapo ndani ya Dar es Salaam imejengwa kwenye Jimbo la Kibamba,

Kata ya Kwembe, Mtaa wa Njeteni kwa shilingi bilioni 5.2. Ninawapongeza sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tutoe pongezi sana kwenye eneo la uchukuzi. Tunaona kaongeza ndege saba, moja ya mizigo na hizi sita zimeenda kufikisha ndege 16. Hili siyo jambo dogo. Katika kipindi cha miaka minne Mheshimiwa Rais katupeleka hapo tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Reli ya *SGR,* mimi ni mpandaji kweli kwa wiki hata mara tatu nakimbiakimbia humu. Kila siku unaenda Dar es Salaam na unafika Dodoma vizuri kwa kasi kubwa sana, lakini vinaendelea hivyo vipande vingine hadi kufikia mwisho. Mimi nina imani sana Mheshimiwa Rais katika kipindi cha pili anaenda kumaliza mambo yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze maeneo mawili ya mafanikio kwenye jimbo, lakini yana changamoto ndogo sana. Eneo la kwanza ni maji. Tumefanikiwa sana. Wakati ninaingia Bungeni ilikuwa 35%, leo nimezunguka jimbo zima, tumefikia 93%, tunaenda kukamilisha kabisa ile ilani inavyosema 95% mijini. Kwa hiyo, tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo dogo ambalo limeanza na ninamwomba Mheshimiwa Rais na Wizara walione ni Bwawa la Kidunda, sasa limefikia 30% na ninajua zinahitajika shilingi bilioni 335. Ni imani yangu kwenye bajeti hii zimetengwa, ili likakamilike. Litatusaidia nyakati kame za mwezi wa Tisa, wa 10 na 11 kupeleka maji kwenye Mto Ruvu ambao ndiyo chanzo cha maji toka tunapata uhuru. Kwa hiyo, kwa jinsi idadi ya watu inavyoongezeka kutoka Sensa ya Mwaka 1967 hadi sensa ya sita, mwaka 2022, mnaweza mkaona Bwawa la Kidunda litatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ule Mradi wa Mwalimu Nyerere wa kufua umeme *megawatts* 2,115 Mheshimiwa Rais kakamilisha; aliachiwa 35% leo imekamilika. Ninawapongeza sana, lakini tunajua ndani yake pamoja na kufua umeme kuna mambo mawili; moja ni kupeleka maji Kusini, Ruvuma, Mtwara na

Lindi na sasa hivi mpo kwenye *design* ya mradi wa kuleta maji Dar es Salaam. Hii itatusaidia sana. Maji ya Ruvu sasa yataishia huku Kusini kwetu au pembezoni. Watu wa Kibamba na maeneo mengine watapata maji kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo ni faraja kwangu ni la miundombinu. Kwa kweli, kwa barabara za *TARURA* na *TANROAD* kazi imefanyika kubwa. Mimi wakati ninaingia madarakani na Mheshimiwa Rais, barabara hizi zilikuwa ni chini ya kilometa tano, leo kuna maeneo yana zege zinajengwa, kwa Msuguri - Kifaru yote kupitia Msingwa na sasa hivi tunaendelea nazo barabara za zege, wananchi wanazijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara za zege zinaendelea King'ong'o, wananchi wanaona. Tayari barabara za lami zimeanza na zinaendelea kujengwa Kibamba Shule, Mpiji na Majohe. Kwa kweli, kazi kubwa inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ushauri wangu? Upo huu mradi wa *DMDP,* tumeanza nao vizuri, wakandarasi wamepewa, lakini kwa maana ya mikataba hawajaingia. Wengi wamekaa miezi mitano hadi sita hawajaingia *site*. Nimeona juzi wanaanza kuingia, lakini barabara moja muhimu ni hii ya Suka – Golani kwa Mheshimiwa Kitila, inaunganisha na Kinyerezi, kilometa 10.1, tuna shida ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakumbuka vikao vya Wabunge wote wa Dar es Salaam tulimwomba kwamba kama Benki ya Dunia haitalipa fidia, atusaidie kutulipia *almost* shilingi bilioni moja na nusu hadi mbili, ili ule mradi kule uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwa wananchi wote wa Ukombozi, Saranga, Upendo na Kata ya Saranga, ni muhimu kweli. Sasa hivi barabara ni mbaya na haitengenezwi kwa sababu tunajua iko kwenye mradi wa *DMDP*. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri tuiweke kwenye bajeti ya fidia ili ule mradi usiondoke kwenye jimbo letu, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Kitila, pacha wangu katika Wilaya ya Ubungo, amesimamia kama Mwenyekiti ilani yetu ya 2025 kufikia 2030, hii hapa, lakini moja nililowahi kuliongea Bungeni kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ni juu ya maendeleo ya makazi ya watu. Dar es Salaam tukachukue Magomeni, Manzese na Tandale iwe na maghorofa. Tuingine makubaliano na wananchi pale, ghorofa ya kwanza hadi ya pili, ya tatu hadi ya kumi tuuze, iwe ni makazi bora ya wananchi, leo ameiingiza kwenye ilani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Kitila, Mungu akubariki sana na ninakuombea kila la heri, hata asitokee wa kuchukua fomu na yeye pale. Waache waje kwangu Kibamba niwaoneshe, na hapa tutakutana tena mwaka 2025 mwezi wa Kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Mungu ibariki Afrika, Mungu libariki Bunge la Tanzania. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ninakushukuru sana Mheshimiwa Mtemvu. Kabla ya mchangiaji mwingine hajafuata, niwalete wageni ambao tunao katika kumbi zetu.

Tunao wageni 60, hawa ni Bunge la Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Tuwaone, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika; hawa ni wageni wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge, Naibu Waziri wa Uchukuzi. Ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Iringa, nitawataja kwa uzito wao.

Tunaye Ndg. Daud Yassin, Mwenyekiti CCM Mkoa wa Iringa, Ndugu Said Goha, Katibu wa CCM Mkoa wa Iringa, Ndugu John Kiteve, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilolo, Ndugu John Kavenuke, Mwenyekiti wa CCM Wilaya Mufindi, Ndugu Constantino Kikwele, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Iringa Vijijini, Ndugu Said Lubeya, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Iringa Mjini,

na Ndugu Joseph Ryata, Katibu wa CCM wa Siasa na Uenezi wa Mkoa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Kihenzile, hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Iringa, wako pale. Ninaomba niwataje wote halafu mtasimama kwa pamoja.

Wenyeviti na Makatibu Wenezi wa CCM Wilaya za Mkoa wa Iringa, Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmshauri za Wilaya na Meya Manispaa ya Mkoa wa Iringa, Wenyeviti na Makatibu wa Jumuiya za CCM ngazi ya mkoa UVCCM, UWT, Wazazi na Wilaya, Wenyeviti na Makatibu wa Jumuiya za UWT, Wazazi na UVCCM, Wilaya za Mkoa wa Iringa. Tunawakribisha sana.

Tuwaone kwa pamoja kwa umoja wenu. Karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Iringa vilevile wameambatana nao. Pia, yupo katibu wa Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, Bi Aida Kaduma. *(Makofi)*

Wapo Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Iringa, wameambatana na ujumbe huu. Vilevile, kwenye ujumbe huu wapo watumishi wa Ofisi ya CCM ya Mkoa. Karibuni sana kwenye Bunge lenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 20 wa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay. Hawa ni Wanakwaya ya Mtakatifu Agustino, Parokia ya Nkuhungu, kutoka Jijini Dodoma. Wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 21 wa Mheshimiwa Fatuma Hassan Toufiq. Hawa ni Viongozi na Wanachama wa Taasisi ya *Support* Mama Samia kutoka Tanzania Bara na Visiwani. Tuwaone, wapo pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge mwenzetu. Hawa ni Makatibu Kata wa Chama cha Mapinduzi kutoka katika Kata zote za Jimbo la Segerea wakiongozwa na Katibu wa Mbunge, Ndg. Lutta Aloyce Rucharaba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni Ndg. Titus Msoka na George Joseph kutoka Jijini Arusha, Walimu wawili na watumishi saba kutoka Taasisi ya Elimu ya Cariado ya Unguja, Zanzibar, Wanakikundi watano wa sala kutoka Parokia ya Kiwanja cha Ndege ya Jijini Dodoma, wako pale juu, na Wanafunzi 68 na Walimu 11 wa Shule ya Msingi Padre Corado kutoka Wilaya ya Kongwa, Mkoani Dodoma. Tuwaone, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bado tuna wageni wengine wataingia baada ya hawa kutoka.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilimwita Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana kwa kunipa fursa, ili niwe miongoni mwa wachangiaji katika bajeti hii ya Bajeti Kuu ya mwaka huu 2025, leo hii Tarehe 18 ya mwezi Juni. Kwanza kabisa ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika nchi yetu kuhakikisha kwamba, Tanzania inaendelea kusonga mbele kwa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Kitila Mkumbo, Waziri makini kabisa na mwenye viwango vya *standard gauge railway*. Hongera sana kwake Profesa kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Tumeona kwa kipindi kifupi kabisa ambacho Mheshimiwa Rais amemwamini katika eneo hilo amefanya vizuri sana. Mimi binafsi pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana. Wiki iliyopita nilimpelekea changamoto yangu kubwa niliyokuwa nayo kuhusiana na eneo

la uwekezaji na ameitendea haki, amenitendea haki. Hakika nimerudi humu ndani ya Bunge nikiwa ninakiri ushuhuda kabisa kwamba, yeye ni mtu makini, mtu mahiri, mwenye uwezo usiotiliwa mashaka; hongera sana kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Maendeleo tunayoyazungumzia maana yake vilevile yametokana na umakini mkubwa wa namna ya kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais hakuna kitu kinakwama. Maendeleo tunayoyashuhudia sasa kimsingi Mheshimiwa Mwigulu ana mchango wake mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vilevile Naibu Mawaziri wao, wamefanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba wanawasaidia ipasavyo ili Mawaziri waweze kutimiza majukumu yao. Kipekee ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Chande, rafiki yangu, kaka yangu Chande kwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu, hongera sana. Ninajua kwa kuwa mimi ni rafiki wa Mheshimiwa Chande basi hatanisahau kwenye ufalme wake pindi atakapoona jina linakwenda pale. Hakika ninaamini mbele ya Mwenyezi Mungu na kwa ushuhuda wote kwamba ataweka tano pale ili mambo yaweze kwenda barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wake wa jana pale, kule kwenye ziara yake ambayo anaendelea nayo katika Jimbo la Kisesa. Mheshimiwa Rais amenikumbusha kwamba, pale ambapo mwiba unaingilia ni pale pale mwiba unatakiwa utokee pale pale. Kwa hiyo, bila kupoteza muda Mheshimiwa Rais alimjibu Mheshimiwa Mpina kwa vitendo, kwamba anachokifanya hayuko sawasawa. Kwa hiyo, yale majibu ambayo alipewa Mpina kwa kweli yamenipa raha sana, yameniletea furaha sana. Kongole nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwa na mtoto umemzaa mwenyewe, umemlea mwenyewe kwa tabu na raha halafu

baadaye anakuja kukupiga mateke hadharani. Ulipoingilia mwiba na mwiba ukatokea hapo hapo safi sana. Aendelee kutufundisha na aendelee kutuelekeza kwa vitendo, mwisho wa siku tutaelewa tu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie suala la ajira. Kwenye suala hili la ajira bado ninahitaji kabisa kwamba, Serikali yangu ione umuhimu wa kuweka ubunifu mbalimbali wa kuhakikisha kwamba wasomi wetu ambao wanamaliza kwenye vyuo mbalimbali waweze kupata namna ya ajira; kama siyo ajira za Serikali basi hata katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitolee mfano, mwaka 2018 nilipata fursa, nikiwa pamoja na Wabunge wenzangu 19 mimi nikiwa wa 20 tulisafiri kwenda nchi ya China, na kule tumejifunza mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo ambayo tulijifunza ni namna ya Nchi ya China ambavyo inaweza kupeleka vijana shuleni na vyuoni. Baada ya kumaliza wanapata mainjinia wa ujenzi. Pia kwenye suala hilo la mainjinia wa ujenzi baada ya kumaliza masomo yao, wanachokifanya wanawaweka wale vijana wakiwa kwenye *organization* moja, kwamba, kama ni kikundi au kama ni kampuni vijana wanafungua kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana wanakuja katika nchi za Afrika wanatafuta kazi zinazohusiana na masuala ya ujenzi, wakishapata kazi wanapeleka *certificate* ile inayoonyesha kwamba wamepata kazi katika Serikali yao. Wakishapeleka ile *certificate* Serikali inatoa fedha ili kuwa-*support* wale vijana na wanafanya kazi baada ya kufanya kazi kunakuwa na kitu kinaitwa *MOU* kati ya hicho kikundi au kampuni ambayo inahusiana na hao vijana pamoja na Serikali. Kwa hiyo, wanapofanya kazi wakimaliza kufanya ile kazi waki-*raise certificate* kinachofuata baada ya kuingizwa fedha, fedha ile inakuwa *deducted* kuelekea kwenye Mfuko wa Serikali. Kwa maana nyingine wale vijana wanabaki na faida na wanakuwa wamefanya kazi, wanakuwa katika sehemu ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Serikali yetu pia, tunao ma-*engineer* ambao wamemaliza vyuo, wako tu

mitaani huko wanatembea tembea hawana ajira, wanatembea na vyeti, wamekuwa *affected* wanadhani kwamba vile vyeti vyao ni lazima wapate ajira. Kwa hiyo, wako wanapita kwenye korido za Serikali ili kutafuta ajira. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Kitila Mkumbo, pamoja na mipango yake aweka huu mpango, kwamba vijana wetu wakimaliza vyuo wafanyiwe utaratibu kama huu, itapendeza sana na tutawainua vijana kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba, ninadhani ingefaa sana tuone umuhimu wa kuwainua wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, wananchi ambao wamekuwa wakifanya kazi ya uzalishaji katika sekta ya kilimo, wamewekeza sana katika sekta ya kilimo hasa kwenye kilimo cha mahindi ambalo ni zao la biashara pia ni zao la chakula. Bei ambayo wakulima wamekuwa wakipewa na Serikali yetu iko chini, ni bei ya shilingi 700. Zaidi ya miongo mitatu mpaka minne bado wananunua kwa bei hiyo hiyo shilingi 700 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme leo hapa kwamba, gharama za uzalishaji wa zao hili ziko juu sana tofauti na hali halisi ya soko iliyoko sasa. Ni kwamba, zao hili kulizalisha kila kitu kimepanda bei, kuanzia kwenye kulima, kupalilia, utiaji wa mbolea, mambo mengi kama ya utunzaji kwa ujumla gharama ni kubwa. Kwa hiyo haiwezekani wakati kila bidhaa nchini kwetu inaendelea kupanda siku hadi siku ionekane kwamba, bidhaa zinazohusiana na uzalishaji wa zao la mahindi tu ziko pale pale. Niombe sana bei hii ipande kutoka kwenye shilingi 700 na hatimaye twende kwenye shilingi 900, angalau hii itamsaidia mkulima kuweza kuendelea kufanya uwekezaji wenye tija katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba niseme kwamba, zao hili la mahindi limekuwa likileta pato kubwa sana katika halmashauri zetu katika Mkoa wa Ruvuma. Ni zao ambalo limekuwa likilimwa kila mahali. Kwa hiyo ninaamini kabisa kwamba litaongeza pato kubwa sana endapo kama tutawasaidia wakulima hawa na kuwatia moyo ili waweze kuwekeza zaidi katika zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la zao la soya. Zao la soya limekuwa na bei chini sana. Mwaka jana bei ya soya ilifikia shilingi 2,000, lakini sasa hivi tunavyozungumza soya inauzwa takriban shilingi 900. Niombe sana Serikali yetu ione umuhimu wa kutafuta soko kwa ajili ya zao la soya. Ninaamini masoko yako maeneo mbalimbali nje ya nchi yetu, kama kutawekwa mkakati mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mashaka na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya kilimo. Anajitahidi sana na anafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo ninaomba niseme kwamba ninamtia moyo; kwamba hata soko hili la zao la soya linaweza kupatikana; lakini hata soko hili la zao la mahindi linaweza kupatikana. Kwa hiyo, ninaomba hatimaye na mahindi nayo yauzwe kwa njia ya mnada. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la Barabara ya Songea – Makambako. Barabara hii imebeba mzigo mkubwa sana unaohusiana na ukuaji wa uchumi katika mikoa hii miwili, mitatu ya kule Kusini. Ninataka niseme kwamba, barabara hii imekuwa ina shida kubwa sana. Barabara imeharibika kwa kiwango kikubwa; lakini bado ina matumizi makubwa sana ya malori ambayo yanabeba makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, makaa ya mawe ni mradi mkubwa sana ambao umeinua pato kubwa sana katika sekta ya madini. Kwa hiyo, tukiitengeneza barabara hii itasaidia kuongeza pato, kwamba magari yale yatasafiri kwa haraka kusafirisha ule mzigo na watakuja kuchukua. Kwa hiyo uzalishaji wa makaa ya mawe utakuwa mkubwa; na pato kubwa sana litaelekea kwenye Serikali yetu kwa kuwa barabara ni safi na ina uwezo mkubwa sana wa kusafirisha kwa wakati hilo zao ambalo ninalizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ambayo yanatoka mashambani kwetu vilevile inatakiwa tuhakikishe kwamba fedha ipelekwe kwa haraka sana. Nitampenda Mheshimiwa Mwigulu akipeleka fedha kwa haraka, fedha ya kutosha ya ukarabati wa Barabara ya Songea – Makambako yenye urefu wa kilometa 395.

Kwani shida ni nini kwa Mheshimiwa Mwigulu? Mbona yeye yuko vizuri? Ni kwamba angeweza hata kutoa fedha ya kilometa tu 100 ikaanza; inaanzia pale Songea inakuja hadi hapa Lutukila, hapo awamu ya kwanza anakuwa amekwishamaliza; awamu ya pili aitoe Lutukila hadi anakuja kuileta hapa kwenye mpaka wa Njombe na Songea na hatimaye atamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu aanze sasa; tunavyoelekea aanze kwa sababu tayari amekwishatoa fedha za kulipa fidia, kwa hiyo watu wanataka waone vitu vile, vyombo viko kule; kama magreda, vifaa vyote viko kule vimeanza kazi. Tunamhakikishia kwamba sisi Wanaruvuma wote tumekubaliana kwa nguvu moja kwamba tunakwenda ku-*tick* kwa ajili ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunakwenda ku-*tick* kwa ajili ya Wabunge wetu ambao ni Wabunge wa Majimbo; tunakwenda ku-*tick* kwa Madiwani wetu. Hakuna shaka kwamba CCM itashinda kwa 100% katika Mkoa wetu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninaomba nizungumzie Barabara ya Likuyufusi – Mkenda. Barabara hii inatoka Songea Mjini inakwenda Mkenda ambako panaunganisha Tanzania na Mozambique. Barabara hii ni muhimu sana katika masuala ya kiuchumi; ina urefu wa kilometa 124.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie tu kwamba barabara hii ni barabara ambayo inatumika sana na wenzetu wa Mozambique, inatumika sana na wenzetu wa Botswana, inatumika sana na wenzetu wa Malawi kwa sababu wenzetu hawa wanatumia Bandari ya Dar es Salaam kusafirisha bidhaa zao, ikiwa ni pamoja na yale magari ambayo wanayaita IT. Kwa hiyo, ni muhimu sana barabara hii ikatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi; si lazima tuianze yote kwa kilometa 124. Dada yangu Jenista Joakim Mhagama kila siku amekuwa akifuata huko na kufuatilia hii barabara. Pamoja na jitihada zake hizo zote, basi ninaomba tuendelee kumuunga mkono ili hii barabara iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa haraka sana ili kuweza kufungua uchumi

wa Tanzania, Mozambique, Botswana pamoja na Malawi kwa ukamilifu kisawasawa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tu namalizia.

**MWENYEKITI:** Ninaomba umalizie.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde chache tu, niaomba niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Ruvuma. Wanawake wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma ninawashukuru sana kwa kunipa heshima hii waliyonipa na vilevile kwa kunipa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa na wakanipa wepesi wa kutekeleza majukumu yangu. Ninawapenda Mungu awabariki sana, ninaomba wanipe mitano tena; haki ya Mungu nitafanya zaidi ya hapo nilipofanya, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia kaka yangu Joseph Mhagama na Wabunge wenzangu wengine wote kwa ushirikiano mkubwa walionipa, pamoja na majirani zangu hapa wa Kakonko, Mbunge wa Buhigwe, Mbunge wa Madaba yuko hapa, pia na Mbunge wa Singida Kaskazini. Unajua watu wanashukuru lakini wanashindwa kujua hapo walipo kaa kwenye kiti walikuwa na majirani zao kushoto na kulia. Vilevile na wewe mwenyewe Mwenyekiti Mwanyika ulikuwa nyuma yangu hapa ninakushukuru sana, kongole nyingi sana kwako, Mungu akubariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Amina, ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Nilimwita Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Dkt. Hamis Andrea Kigwangala na Mheshimiwa Francis Mtinga Isack ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nianze kwa

kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimpongeze sana tena sana kwa kuchaguliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea pekee kwa mwaka huu 2025 pamoja na Dkt. Nchimbi akiwa naye kwa kuweza kuchaguliwa akiwa Makamu wake ambao watakwenda pamoja kusaka kura za Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Morogoro. Ninasema ninawapenda sana, tena sana. Niko humu ndani ya Bunge kwa sababu yao na ninaomba tena niendelee na wao kwa sababu bado tuna mambo mengi ya kufanya ya kimaendeleo kwenye Mkoa wetu wa Morogoro. Kweli ninawapenda sana wanawake wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Kitila pamoja na Mheshimiwa Waziri Mwigulu kwa bajeti hii nzuri ambayo wameileta. Kwa kweli ni bajeti nzuri, ni bajeti ya wananchi, kwa hiyo ninawapa pongezi sana. Pia, ninawapa pongezi Manaibu Mawaziri wenu akiwemo Mheshimiwa Chande pamoja na Mheshimiwa Nyongo; kwa kweli wanafanya kazi nzuri kwa kuwasaidia hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia na Naibu wake Mheshimiwa Zungu kwa kazi nzuri wanazozifanya. Hata Wenyeviti, wasaidizi wao ninawapa pongezi sana kwa kazi nyingi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa mafanikio. Mafanikio ni mengi kwenye bajeti zetu. Nianze kwa kuwapongeza watu wa *TRA*. *TRA* kwa kweli wamefanya kazi nzuri ya kukusanya mapato. Mapato haya ndiyo tunayoyatumia kwenye kuendeleza miradi yetu ya maendeleo hapa nchini kwetu. Kwa hiyo, tunasema ahsante sana *TRA,* ila waongeze nguvu katika ukusanyaji zaidi ya hapo wanapokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli unajua kuwa wananchi wengi bado hawajajituma sana kulipa mapato. Ninaomba elimu

itolewe, hamasa itolewe, kuwa wananchi wote waweze kulipa mapato kama ilivyo kodi waweze kulipa kodi kama wanavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi mikubwa ya kimkakati. Sisi Mkoa wa Morogoro na mikoa yote ya Tanzania tunashukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa miradi hii ya kimkakati, hasa nikianza na *SGR* ambayo wananchi wengi wanaipenda sana na wanasafiri sana kwa *SGR*. Mkoa wetu wa Morogoro tumefaidi. Kwa mfano unaona kuwa inapita kwenye vituo vingi ikiwepo Kilosa na Ngerengere. Vituo hivi vimekua kibiashara kwa sababu ya *SGR;* na *SGR* hii itaendelea kujengwa. Mkoa wa Dodoma tayari tunaitumia na itaendelea kujengwa kwenda Mikoa mingine ya Tabora, Mwanza, Kigoma na kuvuka nje ya nchi. Kwa kweli tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni makubwa sana kwenye miradi hii. Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo litaleta umeme megawati 2,115 ambazo ni nyingi sana, ambalo tayari limeshakamilika. Umeme huu tutaweza kuuza nje na kwa ajili ya matumizi ya ndani. Hili Bwawa la Mwalimu Nyerere ninasema kuwa kwenye bajeti hizi ni kivutio pia na ni utalii pia. Kwa upande wa Mkoa wa Morogoro ukileta vijiji vinavyopakana na bwawa hili kikiwemo Kijiji cha Kisaki tayari vimeshaanza kuinuka kuwa na maendeleo makubwa kwenye uzalishaji na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Daraja la Busisi ambalo kesho linafunguliwa, kwa kweli tunasema ahsante sana kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa Mkoa wa Morogoro tunasema mafanikio yamekuwa mengi na tunasema kuwa hatuna deni na yeye na hivyo mwezi wa kumi tuta-*tick* ndiyo, tutasema ahsante sana; na wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro watampa *tick* ya ndiyo. Tunasema kazi na utu tunazidi kusonga mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye barabara Mheshimiwa Rais ameunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Kwa upande wa Morogoro tuna barabara za lami, tunashukuru sana tumepata bajeti ya kutosha kwa upande wa

barabara ambazo tunatumia. Tunamshukuru Mama Samia kwa mambo aliyotufanyia Mkoa wa Morogoro, tunasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara chache ambazo bado lakini tunajua kuwa kwa bajeti hizi zitatimilika. Kwa mfano Barabara ya kutoka Kibaoni – Kivukoni – Lupilo – Malinyi – Kitanda – Namtumbo hiyo barabara najua iko kwenye mpango wa bajeti, lakini hiyo barabara wakati wa mvua kweli inakuwa ni mbaya sana; Wao Mawaziri wanajua kuwa ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Malinyi wanapata shida, wananchi wa Ifakara, Kilombero wanapata shida kwenda huko Malinyi. Kwa hiyo, ninaomba hiyo bajeti iliyotengwa iweze kutolewa kwa mara moja ili iweze kutengeneza hii barabara. Barabara hii ninakazia kusema ni mbaya sana hasa wakati wa mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ambazo tayari ziko kwenye bajeti kama Barabara ya Bigwa – Kisaki iko kwenye bajeti, mkandarasi amesimama. Ninaomba hii bajeti itoe hela iweze kuwalipa hawa wakandarasi waweze kumaliza barabara hii. Ni barabara ambayo inakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ina maana sana sana. Ninaomba na barabara zingine kama hii ya kwenda Ifakara mpaka Mlimba na zenyewe ziweze kutekelezwa. Barabara nyingi za *TARURA* ninaamini kuwa zitatengenezwa kwa sababu hela zimeongezeka, kwa hiyo ninaomba tuweze kuona kuwa barabara hizi zinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kupunguza umaskini kwa wananchi hasa wa Tanzania wanaotegemea kilimo ni sekta ya uzalishaji. Kwa hiyo, kwa upande wa kilimo ninashukuru sana tumeweza kuinua uzalishaji, uchumi umeongezeka, tutapata matrekta ambayo wananchi wataweza kulima kwa kutumia ruzuku, mbolea itatolewa *VAT,* viuatilifu vitatolewa *VAT*. Ninaamini kuwa kilimo kikisimamiwa kinaweza kumkomboa Mtanzania na kinaweza kutoa ajira hasa kwa vijana na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, nilikuwa ninasema kuwa hela zimeongezwa, lakini ninaomba ziongezwe zaidi, kama tunavyosema, kama tunavyojua makubaliano ya Azimio la Maputo na Malabo ya 10% tunaomba hizi bajeti kadri zinavyopanda ziweze kufikia 10% kusudi wananchi waweze kunufaika na kilimo chao kwa kutegemea hizi. Pamoja na hii bajeti ya kilimo, uvuvi pamoja na mifugo kutolewa ninaomba zitolewe kwa wakati ili ziweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye mifugo, unakuta viwanda vimejengwa, lakini bado tunaomba viongezeke kusudi viweze kuchakata mazao ya mifugo. Kwenye uvuvi, kuna kilimo cha vizimba kiweze kutumika, kiweze kuzalisha pamoja na ajira kiweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda, ninaamini kuwa kwenye bajeti hii viwanda ambavyo havifanyi kazi na hasa kwenye Mkoa wetu wa Morogoro, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Tanga na Mikoa mingine. Hasa Mkoa wa Morogoro iweze kufufuliwa, ijapokuwa vinaanzisha vingine lakini na hivi ambavyo havifanyi kazi viweze kufanya kazi ikiwepo Kiwanda cha *MOPROCO*, *Leather Goods* pamoja na viwanda vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ya mwaka huu ni mwendelezo wa bajeti iliyopita ya mwaka 2025; inamkomboa mwananchi kwa sababu hii ina matumaini mengi ya kuongeza pensheni kwa wazee kutoka 100,000 mpaka 250,000; inaongeza ajira; inafanya Bima ya Afya kwa Wote; itainua sekta ya uzalishaji; Mikopo kwa Elimu ya Juu pamoja na Vyuo vya Kati; na kuendeleza sekta ya kutoa huduma ambayo kuna maji, afya na elimu. Kwa Mkoa wa Morogoro tumejenga shule nyingi tunamshukuru sana Mama Samia kwa yote aliyotufanyia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni ya wananchi, bajeti hii itawakomboa wananchi, bajeti hii itanua maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, ninasema ninaunga mkono hoja ila

ninawashukuru wanawake wa Morogoro tuweze kuendelea tuone tunafanya nini. Yajayo yanapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, ahsante sana. Nilimwita Daktari Hamisi Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii adhimu ya kusema hapa Bungeni siku ya leo. Awali ya yote ninatumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia uhai na aliyetupa zawadi na heshima ya kuwa wawakilishi wa wananchi wenzetu na kuingia katika jumba hili tukufu kwa kipindi cha miaka mitano tukiwa wazima bukheri wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitatumia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Chama changu Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa imani mimi na Wabunge wenzangu katika kujenga Taifa imara la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa Hotuba nzuri ya bajeti. Kwa namna ya kipekee ninampongeza Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri ya Ilani ya Uchaguzi ya Miaka Mitano inayokuja, nimepata fursa ya kuipitia kwa kweli inafurahisha na nina hakika mipango ya Taifa letu ipo kwenye mikono salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonisukuma kuzungumza leo mbali na mambo mengi mazuri yaliyo kwenye bajeti yetu ni mjadala wa Deni la Taifa unaoendelea. Katika mjadala huu watu wanajaribu ku-*compare* Deni la Taifa katika kipindi cha miaka mitano, kumi iliyopita na miaka ishirini, thelathini iliyopita basi na mimi nikaamua kufanya uchambuzi kidogo ili niweze kuona tulikuwa wapi? Tumefika wapi? Na tunaelekea wapi? Na kwa nini tumefika hapa tulipofika? Nikasema basi na mimi walau nitoe

mchango wangu wa senti mbili katika mjadala huu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza bahati nzuri wewe umekulia kwenye sekta binafsi na hivyo ninafahamu una uelewa mpana wa umuhimu wa kukopa kwenye biashara kubwa. Utakubaliana na mimi hata pale nyumbani kwa mfano kama unalipwa mshahara wa shilingi milioni tatu na unataka kujenga nyumba, unataka kupeleka mtoto wako shule nzuri ya *private* ya kulipia, unataka kununua gari zuri, lakini unalipwa milioni tatu tu leo una *choice* mbili udundulize *savings* zako kwenye hiyo milioni tatu ili uje ununue gari baada ya miaka thelathini. Uje ujenge nyumba baada ya miaka thelathini ama ukakope leo ufanye kazi kwa bidii leo, ujenge nyumba nzuri leo uishi kwenye nyumba nzuri, ununue gari zuri leo utembee kwenye gari zuri, upeleke mtoto wako shule nzuri leo kwa sababu pia hasubiri wewe udundulize ili umpeleke shule nzuri, maana yake anahitaji kusoma leo haitaji kusoma kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo ambavyo mashirika binafsi yanaendeshwa, ndivyo ambavyo nchi zinaendeshwa. Kwamba una mahitaji makubwa na ya muhimu leo huwezi kusema utaacha kukopa kwa kuogopa kelele za wasiyolitakia mema Taifa letu eti ukae huna umeme wa kutosha kwa miaka thelathini ijayo kwa miaka arobaini ijayo wakati kuna sehemu unaweza ukakopa na unakopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kule nilikozaliwa mimi wanaume wenye heshima ni wale wenye mikopo. Wanasema kama huna mkopo maana yake huna heshima wewe siyo mwanaume kamili, unakuwaje unaishi kifalafala hauna mkopo hata kidogo, mwanaume lazima uwe na madeni ndiyo mwanaume kamili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo katika uchambuzi wangu nikaona hivi katika miaka ya sitini na katika mwaka 2010 ambao mimi niliingia katika Bunge hili Tukufu ambapo Deni la Taifa lilikua halizidi trilioni 10 lilikuwa trilioni 9.5 nimetazama takwimu mwaka 2010. Hata hivyo, wakati huo bajeti pia ilikuwa *around*

hapo hapo ilikuwa trilioni 9.5 leo bajeti yetu ni takribani trilioni 56.45 kuna jambo la ajabu deni lilikua pia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *GDP* yetu imeongezeka. Leo haiko kama ilivyokuwa wakati deni likiwa deni likiwa dogo. Pia, miradi ya maendeleo tuliyofanya katika kipindi hiki cha miaka mitano, kumi iliyopita ni mingi sana hususan miradi ya kimkakati. Huwezi kutegemea ulinganishe bajeti yetu ya mwaka 2010 na bajeti ya mwaka 2020 kwa mfano ama 2024 kwa mfano, kwa sababu 2024 hata ukitaka ku-*compare* mfano umeme tu tulikuwa na *megawatts* katika nchi hii zisizozidi 500 mwaka 2010 wakati huo deni lilikua trilioni 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bajeti imekua, lakini pia deni likua ila tumepata umeme *megawatts* zaidi ya 2,100. Sasa huwezi kusema bajeti ya mradi katika nchi ambayo unatuletea *megawatts* 2,100 ikaenda sawa na deni la kipindi ambacho bajeti ilikuwa trilioni tisa na tulikuwa tuna *megawatts* 500 tu hatuwezi kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ikawa sawa bajeti ambayo imeenda kujenga vituo vya afya katika nchi kila kona kila Jimbo limepata vituo visivyopungua vitatu katika kipindi cha miaka hii mitano tu. Vilevile, kila Jimbo limepata *ambulance* katika kipindi cha miaka hii mitano tu huwezi kulinganisha bajeti ya namna hii na bajeti ya kipindi ambapo hayo mambo hayakutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo wanaojaribu kulinganisha deni kwa kuangalia awamu za Serikali wakome, kwa sababu hawatumikishi akili zao ipasavyo. Hata ukitazama tu idadi ya watu mwaka 2010 wakati deni likiwa trilioni 9.5 na leo wakati deni limefikia milioni 107 idadi ya watu pia ni tofauti. Unazungumzia *population density* tofauti katika miaka hii na miaka ile lakini leo hii unazungumzia bajeti…*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umeisha?

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea endelea unaongea madini makubwa sana… *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kwanza nimeanza…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unazungumzia bajeti katika Taifa ambalo lina watu takribani milioni 70 huwezi kulinganisha na bajeti katika kipindi ambacho Taifa lilikua lina watu milioni 30 huwezi kulinganisha. Pia, huwezi kulinganisha bajeti katika kipindi ambacho hatukuwa na Mradi mkubwa wa Daraja la Busisi na hii ya leo ambapo tumejenga Daraja la Busisi katika kipindi hiki hiki cha miaka mitano huwezi kulinganisha bajeti huwezi kulinganisha deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi pia kulinganisha deni la kipindi hicho cha mwaka 2010 na deni kama lile la India ambalo limetuletea maji ya Ziwa Victoria la bilioni 600 ukalinganisha na leo. Kipindi kile tulikua tuna upatikanaji wa maji pale Nzega Vijijini wa 21% wakati i ninachukua Jimbo kwa mara ya kwanza, leo hii tuna upatikanaji wa maji katika Jimbo la Nzega wa 90%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama lile deni tulilokopa tukajenga Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria umetutoa kwenye kero ya maji katika kiwango cha kutoka 21% ya upatikanaji wa maji mwaka 2010 mpaka 90% Mheshimiwa Dkt. Mwigulu akakope. Sisi tunaishi na Watanzania maskini kule vijijini, ninaishi kijijini mimi siishi Nzega Mjini ninaishi Kijijini Puge kulikuwa na shida kubwa ya maji. Mimi binafsi na uwezo wangu na *influence* yangu tulichimba visima zaidi ya mara tatu katika kiwanja changu ambapo ninaishi na hatukupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukiwa unaenda zako Mwanza ukisimama pale Puge ukasema ngoja niingie kwa Mheshimiwa Mbunge hapa nijisaidie kidogo utapata maji hata

ukitaka kuoga utaoga. Kwa sababu tuna maji masaa 24 yanayotoka Ziwa Victoria. Kwa hivyo, ule mkopo wa bilioni 600 kitu uliyeleta maji katika Mkoa wote wa Tabora, Wilaya za Kahama katika Mkoa wa Singida baadhi ya maeneo yatafaidika ni mradi ambao hutokana na deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwezi kulinganisha faida ya sisi kupata huduma ya kijamii kama maji na uoga wetu wa kukopa. Kwa hiyo, sioni haja kwa nini tuogope kukopa kama tunaenda kuleta mabadiliko makubwa kwenye maisha ya watu kiasi hiki? Puge kulikuwa hakuna maji leo kuna maji ya bomba, maji safi na salama. Kama tunakopa tunawaletea wananchi maji tuendelee kukopa tu, mimi sioni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nikafanya tathmini nyingine nikatazama na majirani zetu hapa. Jirani yetu ambaye watu wengi kwenye mitandao ya kijamii wanapenda kuji-*compare* naye nchi ya jirani ya Kenya yeye deni lake kwenye bajeti ya mwaka huu liko 278% ya pato la Taifa, sisi ya kwetu iko 200% tuko vizuri kama uki-*compare* bajeti *against GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 sisi tulikua 35% uki-*compare* deni la Taifa *against GDP,* lakini wao hao majirani zetu walikuwa 48% leo hii wako 67% uki-*compare*. Kwa hivyo, tunaenda vizuri hatuna haja ya kuogopa kelele za watu kwa sababu kwanza deni letu liko ndani ya *threshold*. *Threshold* ya Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* ni 55% ya *GDP* sisi hatujafika huko sisi deni letu lipo kwenye kati ya 40% mpaka 48% inategemea unapima kwa kutumia vigezo vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo bado ni himilivu na liko vizuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kama anakopa kuleta umeme akope, kama anakopa kuleta barabara akope, kama anakopa kuleta pembejeo kwa ajili ya wakulima wetu akope. Bunge hili tutapitisha na tutawalinda kwa sababu wanakopa katika misingi ambayo inaenda kuleta tija na ufanisi kwenye maisha ya watu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimalizie kwa kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Nzega Vijijini kwa kuendelea kunipa imani. Wakati nikizungumza hapa siku ya leo katika hatua za mwisho mwisho kabla hatujaenda tena kuomba ridhaa, ninawataarifu tu kwamba sijafika Jimboni muda mrefu kuna mchwa wanakulakula hapa na pale, lakini kama atakuwepo mtu ambaye ataweza kushindana na mimi kwa vigezo basi achukue fomu na ashindane. Nzega ni njema na atakaye aje, niko imara nitarudi Jimboni kugombea na nina uhakika kwa kazi kubwa tuliyoifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia miradi aliyotuletea kwenye Jimbo letu basi nina uhakika wataendelea kunipa ridhaa ya kuwawakilisha kwa awamu nyingine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ahsante sana, daktari wa binadamu, lakini leo ameongea kama daktari wa uchumi ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu atakuwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunifanya kitindamimba mchana huu na kitindamimba siku zote huwa anakula na ukoko, kwa hiyo ninaamini nitaongezea vizuri kwa taratibu bila haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Bajeti Kuu, lakini na Wizara ya Mipango ambayo ndiyo inapanga mipango ya nchi yetu, nitaanza na kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwaambia Wanamkalama kwamba Rais sisi hatumdai bali yeye ndiyo anatudai. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tunakwenda kulipa deni siyo muda mrefu mwezi Novemba kwa kumpa kura nyingi za kishindo kwa mema mengi aliyotutendea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema kwa nini tunasema hatumdai Rais huyu kwa jinsi alivyotundea Wanamkalama. Nilipokuwa ninaingia Jimbo la Mkalama hatukuwa hata na Hospitali ya Wilaya, leo tunavyoongea Wanamkalama wana hospitali nzuri ya wilaya ya kisasa na yenye jengo la dharura. Hatukuwa hata na vituo vya kutosha vya afya, leo tuna vituo vya afya vya kisasa pale Bumanga, pale Ilunda na pale Kinyambuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu hapa nimepata fedha shilingi milioni 250 za kwanza za kwenda kujenga Kituo cha Afya cha Kimkakati pale Iguguno. Wanaiguguno kilio chenu kile ambacho nilianza tangu ninaanza kuomba kura, sasa wamepata na ujenzi wa kituo cha afya unaanza. Haya ni mambo ambayo mama ametufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaingia Mkalama hatukuwa hata na *ambulance* tulikuwa na *Landrover* moja iliyotembea kilometa 700,00 ndiyo ilikuwa inategemea kuokoa akinamama. Leo ninavyoongea nina *ambulance* za kisasa tatu ambazo ziko Jimboni kwangu ambapo mama huyu amewatendea Wanamkalama nikisema hatudai tunamaanisha hatudai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi ya kusema kwenye afya, lakini ninaomba niishe hapo niende kwenye elimu; niliingia watoto walikuwa wanakaa chini, watoto walikuwa wanasafiri kilometa nyingi kutoka kata moja kwenda kata nyingine kufuata shule. Hivi ninavyoongea madarasa ya kutosha yamejengwa, madawati yapo, shule mpya ya msingi moja wapo ipo pale Nkindiko Kata ya Kinyangiri watoto wanasoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari madarasa yapo ya kutosha, lakini nimepewa Shule ya Sekondari mpya Kisubihu iko pale Kata ya Iguguno. Nimepewa sekondari mpya inaitwa *Mkalama One* iko pale Nduguti, sekondari mpya iko pale Kidarafa tena ya amali, lakini nyingine iko kwenye *pipeline* inakuja inaenda pale Kata ya Mwangeza. Haya ni mambo ambayo mama huyu ametutendea kwenye elimu, nikisema hatudai ndiyo wananchi

wa Mkalama muelewe kweli hatumdai mama yetu na yeye ndiye anayetudai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda haraka nikienda kwenye maji. Nina vijiji 70, katika vijiji 70 wakati ninaingia hakuna kijiji kilikuwa kinakunywa maji ya mtandao. Leo ninavyoongea katika vijiji 70, vijiji 30 wanakunywa maji ya mtandao maji safi ya bomba, katika vijiji 30 nitataja tu 10 kwa mfano kuthibitisha haya. Ipo Nduguti, Nkungi, Malaja, Milade, Senene, Kinyangiri, Iguguno, Kinampundu, Ibaga, Asanja, Tumuli, Ipuli, Nkinto, na Mbigigi viko 30 maji ya mtandao Mungu atupe nini? Ampe huyu mama maisha ili aendelee kutuneemesha Wanamkalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maji ya *point* source maji ambayo unachimba chini unaweka *solar* ama unaweka umeme, lakini kuna kituo kimoja tu cha maji viko vijiji nane. Maji kwenye vijiji ambavyo kuna pampu ya mkono vijiji 29, katika vijiji 70 ni vijiji vitatu tu ambavyo havina hizi huduma za maji. Kwa hiyo, ndugu zangu nikisema mama hatudai ni kweli hatudai hivi vichache vilivyobaki mimi pekee ndiye ninayejua viporo viko wapi niende kuvipasha. Kwa hivyo, wananchi wa Mkalama hakikisheni mtu anayejua viporo vimebaki wapi wanamrudisha na siyo hao wanaojidai wanawapenda Wanamkalama, lakini leo hawapo Bungeni wameweka kambi huko wanawapa elfu hamsini hamsini kununua Jimbo wakati wanajua anayewapigania yuko Jimboni wapate maendeleo yenu. Kuleni hizo hela Wanamkalama, kuleni hizo ni haki zenu hela za makafara hizo, lakini mimi mkombozi wao niko hapa ninawatetea mpaka dakika ya mwisho ili na wao waendelee kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema mama hatudai ninamaanisha. Wakati ninaingia Mkalama vijiji 24 havikuwa na umeme kati ya vijiji 70, leo ninavyoongea hakuna hata kijiji kimoja hakina umeme, katika vitongoji vyangu 388 takribani vitongoji 200 vina umeme. Wanamkalama mimi ndiye ninayefahamu vitongoji gani 188 vilivyobaki vinahitaji umeme na hapa nipo na-*trot* mwezi wa Novemba nitakuwepo hapa Bungeni ninaanza na hivyo vitongoji kuhakikisha wote wanapata umeme, wanakula matunda ambayo mama huyu ametuletea umeme wa kutosha.

Tuna umeme *megawatts* 4,000, sisi tunatumia 2,000 hizi ni zenu na vitongoji vyote hivyo watapata umeme chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema mama hatudai namaanisha barabara leo Mkalama inapitika kila kona iwe masika iwe kiangazi, vivuko tumejenga, madaraja ya kutosha, daraja kubwa pale Msingi. Hivi ninavyoongea daraja pale Kinyangiri shilingi bilioni 1.5 wakandarasi wako *site*. Mkandarasi mwekezaji yule msimamizi juzi alikuwepo wamemwona, Wanakinyangiri, lakini leo daraja hilo linajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya lami ninajua ndiyo kiu yenu iliyobaki Wanamkalama, lakini ninataka niwaambie kilometa 10 za lami pale Nduguti mazungumzo yanaendelea kati ya wakandarasi na Waziri wa Fedha. Nimwombe kaka yangu (pacha wangu) kabla hujampa mama nafasi ya kutengeneza *cabinet* nyingine, ninajua mama ana nafasi hiyo; na naamini kwa jinsi alivyotenda kwa uzuri na kwa sababu bado mama huyu ni mwema ninaomba Mungu aendelee kukurudisha kwenye hiyo nafasi. Kabla hajakabidhi, kabla hajapata nafasi ya kuunda *cabinet* apeleke zile fedha za kilometa 10 pale Nduguti, lakini pia kilometa 11 pale Ilongero kutokea Igauri mpaka Ilongero, kwa nini ninasema na hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wa Jimbo la Mkalama wana *interests* na hizi barabara mbili: Kata ya Mwanga, Kinampundu na Ilunda tunatumia Barabara ya Ilongero kupita Mtinku. Hata hivyo, kuanzia Iguguno mpaka Siditi kwenda mpaka kule Simiyu tunatumia hii barabara ambayo kilometa 10 zipo kwenye hii bajeti. Kaka yangu (pacha wangu) leo nitoe siri kwa nini hatujabadilisha Jimbo la Iramba Mashariki likaitwa Mkalama ninatoa siri leo sisi ni pacha tuliona tukibadilisha jina upacha wetu utapotea na mapacha siku zote wanavaa sare. Baba yeye ana nguo ya lami nyeusi inapita huku Jimboni kwake huku kwetu tusije tukaonekana pacha wa pili ana kiraka, apeleke fedha upacha upimike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi waliokuwa wanalalamika kwa nini hatujabadili jina niweze kuwajibu kwa vitendo kwamba sikubadili jina kwa sababu sisi ni pacha lazima tupate lami, kwa hiyo ninamwomba sana ndugu yangu. Kwa hiyo, ndugu zangu wananchi wa Mkalama wakae mkao wa kula, kazi waliyonituma nimeifanya kwa miaka mitano chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na bado nina nguvu ninakuja kumalizia viporo vilivyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wako vijana wa CCM ambao wanalitaka Jimbo waambieni wasubiri niwatengenezee Jimbo, nitakapoondoka waje wakae vizuri, lakini wale wakimbizi, wale wavamizi waliokimbia Majimbo yao huko mpaka walishindwa kwa wananchi wao wameweka kambi huko wanaendelea kuwaghilibu kwa vifedha, wale hizo fedha wananchi wangu. Mimi mkombozi wao ninakuja kumalizia kazi chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na hakika Mkalama itapaa. Wanajua jinsi ninavyojua kuwaombea mimi siyo bubu, wao ni mashahidi kwa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu wanasema: "*nzagamba*" dume lile ambalo halijahasiwa. Kwa hiyo, ninataka niwahakikishie ndugu zangu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunakwenda kuitoa Mkalama, tunakwenda kuitoa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kumshauri Waziri wa Mipango, nimwombe sana ndugu yangu. Ninaomba nitoe ushauri tutengeneze Gridi ya Taifa ya Maji, Mungu ametujalia tuna Ziwa Victoria lina maji baridi, tuna Ziwa Nyasa lina maji baridi, tuna Ziwa Tanganyika lina maji baridi. Tunatumia fedha nyingi sana kuchimba visima, kwenye mipango yake ndugu yangu Profesa waweke mipango tutengeneze Gridi ya Taifa ya Maji itakayosambaa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hayo tutayatumia kwa kumwagilia, tutatumia kwa kunywa, tutatumia kwa mifugo na nchi yetu itapaa, maji ya kutosha. Niwaombe sana kwa hilo kama tulivyo na Gridi ya Umeme ambayo inazunguka nchi yote, tuna

Mkongo wa Taifa unapita kote hatuwezi kushindwa kuwa na Gridi ya Maji ambayo Watanzania tunakwenda kumalizia hivi vijiji vidogovidogo katika Majimbo yote ya Wabunge hawa kama tutakuwa na Gridi ya Taifa ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba nitoe ushauri kwenye hilo kama Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwako mipango. Ninakuamini sana Profesa. Mipango ya nchi hii iko Iramba, fedha za nchi hii ziko Iramba siyo kwa sababu tumepeleka kwa sababu tuna vichwa vilivyotulia, tunawaombea waendelee kufanya kazi watuwakilishe, wametuwakilisha vizuri hawajatutia aibu, waendelee kumsaidia mama na sisi tunahakikisha hatutamwangusha na kura za kutosha atazipata. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja na ninawaambia Wanamkalama huu ni mchango wangu wa mwisho ninakwenda kijana wao kuja kumaliza kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtinga, ahsante sana kwa mchango wako huo.

Waheshimiwa Wabunge tumemaliza wachangiaji wa mchana huu na wa asubuhi hii, tutaendelea mchana na tutakaporudi wafuatao wataanza: Ally Juma Makoa, Haji Amour Haji, Nicholaus George Ngassa, Atupele Fredy Mwakibete na wengine tutawataja kadri muda unavyokwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaahirisha Bunge niwatambulishe wageni ambao tumekuwa nao kipindi hiki.

Tuna wageni 69 wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi huyu ni Naibu Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum. Hawa ni Watumishi wa Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo kutoka Mkoa wa Dodoma Makao Makuu; tuwaone. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine 57 wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, hawa ni Wanafunzi na Walimu wa Shule ya Ghati *Memorial* kutoka Babati, Mkoa wa Manyara, karibuni sana Bungeni, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza mchana huu na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye

Bunge hili la Kumi na Mbili. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kujalia kwamba leo ninahitimisha uchangiaji wa Bunge hili la Kumi na Mbili nikiwa na afya salama kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuchangia bajeti hii na nisije nikasahau ninaiunga mkono ili iweze kwenda kufanya kazi za wananchi. Ninaiunga mkono kwa sababu tumeona hata bajeti hii ambayo inaendelea sasa hivi imefanya vizuri. Bajeti zote zilizopita nyuma zilifanya vizuri. Kwa hiyo, nina imani kubwa 100% kwamba hata bajeti hii itaenda kufanya kazi vizuri zaidi ya hata hizi zilizofanya vizuri zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa kuiongoza nchi yetu vizuri, kusimamia rasilimali zetu za nchi vizuri na hatimaye leo wananchi wananufaika na rasilimali za nchi na kila mmoja anafurahia. Nilikuwa kwenye mikutano ya hadhara ninaona namna gani wananchi wana furaha na Awamu ya Sita namna ilivyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa ya kumsaidia Rais na kusimamia rasilimali za nchi pamoja na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na ndugu yetu Mheshimiwa Chande kwa kweli wanafanya kazi nzuri, ndiyo maana leo hata Majimboni kwetu tukienda wananchi wetu wana furaha na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba hakika hatumdai kweli Dkt. Samia Suluhu Hassan na tukisema hatumdai Rais kwa maana kwamba hatumdai si kwamba eti amemaliza kazi zote za nchi hapana, bali kipande ambacho tulimpatia kama wananchi wa Tanzania katika Awamu hii ya Sita akimalizia zao zao wenyewe wakiwa katika Awamu ya Tano, kwa kweli amefanya kwa weledi mkubwa sana. Kwa maana hiyo kipande hiki kakimaliza kwa kufaulu kukubwa tunasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza na kumshukuru na kwa kweli hatumdai, kwa sababu ukiangalia miradi ambayo aliichukua kutoka Awamu ya Tano ambayo yeye alikuwa

Makamu wa Rais; Mradi wa Bwawa la Umeme limekamilika, Treni ya Mwendokasi leo tunaifurahia tunapanda na kwenda Dar es Salam, kesho atazindua Daraja la Busisi na Makao Makuu ya Dodoma inaendelea kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Rais alikuwa akitembelea barabara ya mzunguko wa nje, haya yote ameyafanya. Tumeangalia ununuzi wa ndege na mambo makubwa kama haya. Kwa maana hiyo kipande hiki cha Awamu yake ya Sita ya Miaka minne amekitendea haki, ndiyo maana tunasema kwa kipindi hiki hatumdai. Hatumdai sasa tunakwenda kumkabidhi miaka mitano tena ijayo kwa ajili ya kwenda kuhakikisha na kutimiza bajeti ya kazi na utu na tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo letu la Kondoa Mjini kwa kweli tunashukuru sana miradi iliyofanyika ni mingi na ndiyo maana tunasema hatumdai kwa sababu yale tuliyokuwa tukitarajia yafanyike kwenye jimbo yamefanyika. Tunakwenda sasa kumpatia awamu nyingine tena ya miaka mitano kwenda kumalizia vile ambavyo vimebaki katika awamu hii. Nina uhakika tutampa kura za kishindo kwa sababu tunawapima wananchi namna wanavyoenenda kule katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia kipindi wakati tunaomba kura kuingia katika ubunge, ukiangalia nyuso za wananchi kipindi kile, ukifananisha na nyuso za wananchi wa kipindi cha sasa hivi unaona hata mikutano yetu inakuwa ni mikutano yenye bashasha na wananchi wana furaha maana yake kila mwananchi ana uwezo wa kuelezea maendeleo makubwa yaliyofanyika katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, niwatie moyo wote wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, Mawaziri wote tuliofanya nao kazi katika awamu hii wamefanya kazi vizuri sana, Makatibu Wakuu wamefanya kazi kubwa sana, Wakurugenzi wa sehemu mbalimbali wamefanya kazi kubwa sana. Niwape hongera na niwatakie kila la kheri katika awamu hii ya kwenda kuitekeleza hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiunga mkono bajeti kwa sababu nimeona na kwa sababu nimeshiriki mwenyewe kupitisha bajeti hii katika Wizara mbalimbali. Nimeona namna gani bajeti inaenda tena kuwagusa wananchi wetu. Nimeona namna gani bajeti itaenda kumalizia vile viporo ambavyo vimebaki katika miradi yetu. Hivyo basi, kwa sababu maendeleo haya ni mchakato ninaendelea kuunga mkono na tutaipitisha kwa kura za ndiyo, ili fedha ziweze kwenda kumalizia miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Wizara mbalimbali; umeme, tumepata katika maeneo mengi na nishukuru leo walikwenda wataalam katika Kata ya Mongoroma kwenda kufanya *survey* kwa ajili ya kupeleka umeme ambao ndiyo mitaa nilibakiza, Mongoroma, Chandimo, pamoja na kule Hachwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini bajeti hii itakayopita tutakwenda kumalizia ile mitaa mitatu iliyobaki na tutakwenda kujaziliza maeneo yale ambayo yamebaki. Sina mashaka kwa sababu hata wananchi wenyewe wameona namna kazi zilivyofanyika. Kwa hiyo, tukiwaambia tunakwenda kukamilisha hawatakuwa tena na mashaka juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara ya afya pia tumeboresha sana maana yake kipindi hiki cha Awamu ya Sita kimeboresha sana huduma ya afya kwenye jimbo. Kwa maana hiyo kila mwananchi anaridhika na huduma. Tumeboresha hospitali ya wilaya, hakika wananchi wana-*enjoy* huduma ambazo zinapatikana sasa hivi, kwa maana upatikanaji wa madawa umeongezeka, majengo, miundombinu mbalimbali imeongezeka. Hospitali ya Wilaya ya Kondoa sasa imekuwa ni hospitali ambayo kila mmoja anaona. Tumejengewa majengo ya mama na mtoto, upasuaji, *mortuary*. Vitu hivi havikuwepo, pia tumeboresha wodi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo wananchi wanapata huduma tofauti na huko nyuma palipokuwa na malalamiko mengi kabisa. Kwenye kata tumeweza kujenga vituo vya afya. Tunashukuru sana Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan,

kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na tunaendelea kujenga zahanati kwenye maeneo mbalimbali. Tunaamini bajeti hii ambayo tunaipitisha ndiyo bajeti ambayo inakwenda kukamilisha hii miradi ambayo haikufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumejenga barabara maeneo mengi. Jana nilikuwa kwenye mkutano amesimama Mzee ana miaka 78 akatoa ushuhuda kwamba, toka amezaliwa kwenye mtaa wake, ilikuwa kijiji sasa hivi ni mtaa hakuwahi kuona ma-*grader* yakipita kwenye mitaa yao. Kwenye Awamu ya Sita wamesema wameona vitu hivi na ndiyo maana ninasema kwa hakika hatumdai Mheshimiwa Rais kwa sababu ikienda vijijini wenyewe wanatoa ushuhuda wa kazi ambazo walikuwa hawaamini kama zitafanyika, lakini zimefanyika kwa wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya maji tumefanya kazi kubwa sana. Tunaishukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maana ya kwamba hata vijiji ambavyo vilivyokuwa havifikiki lakini leo wanapata huduma ya maji. Kazi chache zilizobaki kwa ajili ya umaliziaji hapa tunasema mchawi ni muda tu, leo tumebakiza siku zisizopungua saba au nane za Bunge hili lakini ninaamini kabisa wananchi kwa kazi kubwa waliyoiona imefanyika katika kipindi hiki hawana mashaka na Mheshimiwa Rais na Mbunge wao. Ninaamini watat urudisha ili tuweze kumalizia zile kazi ambazo tumeziishia njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kila mmoja amethibitisha kwamba hakika kazi imefanyika kwa sababu leo tumechimba visima kwenye maeneo yote, vijiji, vitongoji pamoja na maeneo ambayo yenye *centres* tumepeleka visima. Tunashukuru sana Wizara ya Maji kwa kweli imefanya kazi kubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga madaraja yasiyopungua 40 makubwa na madogo kwenye jimbo langu. Sasa tumebakiza machache sana ambayo ni makubwa na kazi inaendelea. Hatuna mashaka juu ya Serikali kwa sababu imefanya, inaendelea kufanya ninaamini itamalizia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna daraja letu hili tulikuwa tukilizungumzia la Monguli *"B"* ambalo tulisema Daraja la Mto Bubu lenyewe ndiyo limebaki usemi mkubwa wa wananchi, lakini tunaishukuru Serikali imetoa milioni 660 mpaka hivi sasa katika kuhakikisha wanakamilisha kazi za awali za ujenzi wa daraja lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwa sababu kazi hizi tayari zilishafanyika za *feasibility study,* kwa sababu zilishakamilika na gharama imeshafahamika na tayari *file* limepelekewa wizarani, ninaamini bajeti hizi zinazokuja, hii pamoja na hiyo inayofuta zitaendelea kufanya vizuri kulijenga daraja hilo ambalo ndio kilio kikubwa cha wananchi wa Jimbo la Kondoa Mjini na wananchi wa Hanang' na Kondoa Vijijini. Kwa hiyo, kwa sababu ni daraja ambalo linaunganisha Mikoa ya Dodoma na Singida kwa Wilaya ya Kondoa na Hanang' ninaamini Serikali hii itafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru zaidi kwa sababu kwa kupitia hiyo milioni 600 Serikali imeshafanya pia upembuzi yakinifu wa daraja kubwa ambalo walikuwa wanalitumainia wananchi wa Kondoa la *NBC* ambalo kwa sasa tunatumia daraja dogo la zamani ambalo gari zinasubiriana. Wameshakamilisha hiyo *feasibility study* kwa kupitia mradi uleule wa Mto Bubu. Hivyo tunasubiria tu Serikali ainze kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali mambo yaliyofanyika ni makubwa na ndiyo maana tunaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja ili iweze kwenda kufanya kazi za wananchi katika awamu inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimtamka Mheshimiwa Haji Amour Haji lakini ninamwomba radhi. Mheshimiwa Haji Amour Haji atafuata baada ya Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi na

Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa ajiandae. Mheshimiwa Masaburi, tafadhali.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambazo amefanya katika nchi yetu kwa miaka hii minne tangu amechukua nafasi ya uongozi. Pia, niipongeze Wizara ya Fedha chini ya baba yangu Mheshimiwa *Comrade* Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa *Comrade* Mkumbo na Naibu Waziri wetu wa Fedha Mheshimiwa Chande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana kwa bajeti nzuri ambayo imelenga kuleta unafuu kwenye maisha ya Mtanzania mmoja mmoja, lakini kwa kujipendelea niseme imeenda kulenga kumnyanyua kijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo kwanza nianze na sehemu chache ambazo zimenivutia na zinamlenga kijana moja kwa moja. Kwanza, niwashukuru Wizara ya Fedha kwa kuona kuna sababu kubwa ya kupunguza ongezeko la kutoza kodi ya mapato kwenye kundi la pikipiki na bajaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba vijana wengi ndio wamejiajiri hapa; kuwapunguzia mapato inaenda kuwafanya sasa kila kijana *instead of* kupewa zile pikipiki aidha na tajiri au na mtu yoyote anaweza kujinunulia yeye mwenyewe, akajisimamia yeye mwenyewe na akafanya kazi zake na kujiongezea kipato chake mwenyewe cha maisha ya mmoja mmoja hata kwenye vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niwapongeze Wizara ya Fedha, ninaona wamekuwa kinara wa kusimamia nishati safi na hapa mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Nishati ya Madini, tumekuwa ni wa kwanza kabisa na tumeshauri sana kwenye upande wa sehemu zile za kujazia gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri sana kupunguzwe kodi kwa wale watu ambao wametengeneza vituo. Kwanza, vile vya Serikali hata vya watu binafsi. Kwa hiyo, hapa ninaona wamepunguza na kusamehe kodi kwenye upande huu wa *CNG Station* kwa asilimia kubwa sana. Ninawapongeza Wizara ya Fedha kwa kujali maisha ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ninaomba vilevile nishauri kwenye upande wa *hotel levy*. Ninaomba niishauri Serikali na baba yangu Mheshimiwa Mwigulu hapa ninaomba nimshauri. *Hotel levy* ninaona kwenye bajeti yake amesema anapunguza kodi kwenye *hotel levy* kutoka 10% mpaka asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwelewa, kwa sababu ameenda kulenga kwenye zile hoteli ndogondogo *(lodge au guest house na houses),* lakini baba yangu hapa ninaona kama amesahau kwamba hoteli ndogondogo sasa hivi Mheshimiwa Rais amenyanyua sana uchumi wa nchi yetu, ninaomba wakubaliane nami hilo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hizi hoteli ndogondogo kwa uelewa wangu mdogo ninaziona zipo chache sana na nyingi hazijakua kwenye mfumo sahihi wa kulipa kodi. Sasa hii punguzo la *hotel levy* unaenda sasa kuwapunguzia hizi hoteli kubwa ambazo nyingi zinakuwa kwenye *four-star* mpaka *five-star,* ambazo sioni kama kuna haja ya kufanya hivyo kwenye hili punguzo limekuwa ni kubwa sana kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza; bado tunahitaji mapato. *Hotel levy* kwa miji mikubwa kama London, Dubai, Ujerumani inaitumia *hotel levy* kuwa ni chanzo kikubwa cha mapato hasa kwenye kusimamia mazingira na barabara kwa sababu ni miji ambayo inatumika na watalii mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, anapoenda kuipunguza kwa kiasi hiki ninaona bado anajirundikia mzigo kwenye wizara yake ya kutafuta vyanzo vingine vipya, ili ku-*maintain* hizi barabara na ku-*maintain* na mazingira mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninashauri akae na wizara yake waangalie ni jinsi gani. Ni jambo zuri, lakini ninaomba waangalie ni jinsi gani wataenda kusimamia hili eneo vizuri Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu yeye mwenywe amesema kwenye hotuba yako kwamba inaenda kupunguza kodi *almost* bilioni 9.7 hii ni hela nyingi sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba katika eneo hili wakae waliangalie vizuri kwa sababu watu wengi wanaotumia hoteli ni watalii na nchi yetu watakubaliana nami imeongezeka watalii kwa asilimia kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kama imeongezeka watalii wengi wanaingia, wanatumia hizi barabara na mbuga, kwa nini wasiongeze kiasi fulani ambacho kitaenda basi hata kuwafanya kukitumia hata kwenye kurekebisha barabara za mbugani na miundombinu mingine. Kwenye suala hili wamefikiria vizuri kwa mtu mmoja mmoja, lakini wamemfikiria sana mzawa wa hapa ninawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia walifikirie kwa namna ambavyo nimeshauri kwamba, hiki ni chanzo kikubwa sana cha mapato na wanapoenda kukipunguza wanapunguza kiwango kikubwa sana cha mapato kwenye wizara yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ninawapongeza sana kwa bajeti nzuri na ninawatakia kila la kheri kwenye kutimiza majukumu yenu. Basi ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juliana ninakushukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngassa. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ni kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi aliyetuwezesha kukaa kwenye viti vyetu hivi na

kupata pumzi zake. Pili, nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anatuwezesha na kuweza kufanya kazi zake za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuiwezesha nchi yetu kuwa katika hali ya usalama na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninawapongeza Mawaziri wetu akiwepo Waziri wetu makini, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mawaziri wetu wa Mipango, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Hamad Hassan Chande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika maelezo ya bajeti ambayo tunaichangia hii leo, kwa kweli niseme tu wazi kwamba, hakuna bajeti ambayo imekamilika na iliyokuwa pengine imejaza hasa yale mahitaji ya Watanzania kama bajeti ambayo imewasilishwa kipindi hiki. Bajeti yetu ni bajeti ambayo kwa kweli imeakisi mambo yote ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika suala letu la kiuchumi utakuta kwamba hasa katika suala la ongezeko la mapato ya Taifa kwamba bajeti yetu iko juu sana, imeakisi hasa kwamba safari hii bajeti yetu inaonyesha hasa kwamba pato letu la Taifa limekuwa kwa asilimia 5.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika suala la uimarishaji wa mazingira mazuri ya kisera na sheria, maana yake tutasema kwamba kwa upande wa Mipango na Wizara yenyewe ya Fedha maana yake kule nako kumekamilika kukiwa kuzuri sana, kwamba mazingira yetu inaonekana yanaendelea kuwa ni mazuri sana hasa katika masuala ya kisheria na kwenye uwekezaji wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe na mazingira bora ya kodi na upatikanaji wa nguvu kazi na ujuzi. Ukiangalia hasa bajeti yetu imelenga huko kote, tukizungumzia suala la kikodi maana yake kodi yetu, sasa safari hii maana yake imejaribu kuangalia wananchi wetu na imejaribu kupima na kuangalia namna ya hali ya maisha ya watu. Kuna baadhi ya mahali pengine kwa mujibu

wa ile hali ilivyo, kuna kodi zimepungua au tozo zenyewe maana yake zimepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hali ya kisiasa tukiangalia kwamba hali yetu ya kisiasa kwa upande wa nchi kiujumla, nchi yetu ina utulivu wa hali ya juu, tukizungumzia katika suala la kiujumla upande wa Tanzania Bara au upande wa Visiwani kwetu Zanzibar kule, hali ya kisiasa ni nzuri sana. Kukiwa na utulivu wa kisiasa, kukiwa na utulivu wa amani tuliyonayo, maana yake hata uchumi wetu nao utakuwa katika hali ya utulivu. Maana yake ili uchumi uwe tulivu maana yake lazima tuwe na amani, ni lazima siasa zetu ziwe ni himilivu na tulivu, ukiangalia mpaka sasa hivi pamoja na kelele zote hali ya kisiasa, hali ya usalama wa nchi yetu iko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika suala la kibajeti hasa tukizungumzia suala la Wizara zile mbalimbali, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Utalii, Wizara ya Viwanda, Usafirishaji, Elimu, Afya, pamoja na Madini, ukiziangalia zile bajeti za kila Wizara, ukizichambua utaona hasa kwamba zimeakisi hasa maisha ya Watanzania na hali ambayo tunayotaka kwenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kibajeti mara nyingi hasa tunaangalia ili bajeti yetu na uchumi wetu uwe mzuri, wakati mwingine tunaangalia suala la idadi ya watu. Mara nyingi mtu anakwambia kwamba wakizaliana sana si vema, lakini kuna nchi kadri watakavyokuwa wanazaa, ikiwa kwamba wanazaa lakini nguvu kazi ambayo wanayo, watu wanapata elimu bora, wanapata afya njema na wanapata maisha mazuri, kula nzuri, hiyo itakuwa inajenga kwamba hata katika masuala ya mazingira yale ya uchumi wa ndani, yanakua kwa sababu ya wingi wa idadi ya watu tulionao. Kwa sababu, badala ya kutegemea soko la nje, tutakuwa tunategemea soko letu la ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchumi wetu wa nchi kiujumla, uchumi wetu kwa sasa hivi maana yake unakua kwa hali kubwa sana. Nikizungumzia suala la ushauri katika hali ya uchumi, Serikali lazima iongeze uzalishaji wa bidhaa na huduma wa hali na mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili, kuwe na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye sekta ya madini, kilimo, utalii, na viwanda. Tukiwa kwa mfano kama tutaongeza suala la uzalishaji au uwekezaji katika sekta hizo, maana yake uchumi wetu bila shaka utakua kwa kiasi kikubwa. Sasa, ninaishauri Serikali katika suala la uwekezaji sekta hizo maana yake tuziangalie katika hali nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu katika ushauri, maana yake hili linafanywa, kwa sababu Serikali yetu imejenga shule bora kila mahali sasa hivi kuna shule nzuri, hili maana yake ni nini? Maana yake ni kuwafanya watu wetu kupata elimu bora na yenye ujuzi. Tukiwa tuna watu wenye elimu bora na yenye ujuzi, maana yake uchumi wetu bila shaka utakua kwa kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika kushauri ambalo limeshafanyika kwa upande wa, nilivyoangalia suala la kibajeti upunguzaji wa kodi na tozo, kuna tozo nyingi ambazo nimeziona hasa kwa hawa wawekezaji au wajasiriamali wadogo wadogo kama bodaboda, nadhani wale kuwawezesha kuwapunguzia zile tozo, maana yake pia ni kuwawekea mazingira mazuri ya kuweza kujiwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha miundombinu, hili suala nalo liko katika hali nzuri sana, kwa sababu ukiangalia kwamba kwa nchi yetu kwa sasa hivi miundombinu iko katika hali ya uimara mkubwa sana. Tukiangalia madaraja ambayo yamejengwa, kwa mfano kama Kigongo – Busisi ambapo kule kuna daraja la kisasa, kuna barabara zilzojengwa pamoja na miundombinu mingine, hiyo yote ni kusema kwamba ni njia ya kuweza kuchochea uchumi wetu uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la utoaji wa mikopo na kupunguza riba kwa watu wetu, hilo nalo kama Waziri wa Fedha tuliangalie kwa upana sana. Ingawa kwa mfano mpaka sasa hivi ukitazama kwamba katika upunguzwaji wa hizi riba kwenye mabenki, bado riba zetu zipo kubwa, lakini ili kuwawezesha watu wetu mabenki yetu waweze kupunguza riba zao ili kuwawezesha

watu wetu waweze kujiwekeza na uchumi uweze kukua katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza teknolojia na mbinu mpya za usimamizi wa shughuli zetu. Hilo nalo nadhani kwamba limetajwa katika bajeti zetu, ili kuweza kuwa na usimamizi mzuri lazima kwamba tuwe na teknolojia ya kisasa, tuwe na usimamizi ambao utakuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika hoja yangu ya pili, hasa katika suala la hizi Sheria ya Mapendekezo ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura Namba 30. Pale utakuta kwamba katika sheria ile, katika mabadiliko ambayo yamekusudiwa kufanywa ya Msajili, kuna mapendekezo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha yeye amependekeza baadhi ya hizi fedha ambazo zinazoingia hasa kwenye suala la gawio la 15%, badala ya kwamba kwa yale mashirika kuwa 15% kwa kila baada ya kila kiezi mitatu, alipendekeza gawio lile liwe linafanyika kwa kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala sa sheria hii na tukiangalia suala la Msajili wa Hazina, kwa sababu Msajili wa Hazina ndiye ambaye anabeba taswira nzima ya Mashirika ya Umma. Sasa, kuna kitu ambacho mpaka sasa hivi nitasema kwamba tumekiacha kama kiporo, ile Sheria ya Msajili wa Hazina ambayo sheria ile ingelikuwa ipo maana yake ingelikuwa imetoa mwanya mkubwa sana na haya tunayoyapendekeza, kwa mfano kama Msajili wa Hazina zile fedha zinazokwenda kwenye Mfuko Mkuu au zinazotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, maana yake inawezekana pengine kama ile sheria ingepita maana yake fedha zile zingepitia kwa Msajili wa Hazina ili kuweza kuzi-*control* na kuziangalia namna gani ya mashirika kuweza kwenda nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna shirika kama *TANAPA*, nina hoja nyingi, lakini mwisho nadhani kwamba nipe dakika kama mbili, nimpongeze Msajili wa Hazina kwa namna ambavyo anafanya kazi zake hasa katika gawio la safari hii, kwamba kwa mwaka huu tumepata trilioni moja ambapo kwa

kiasi kikubwa sana tumepiga hatua. Hiyo ni hatua ambayo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa na bilioni 600, mwaka ambao tumeingia sisi mwaka 2020 tulikuwa na bilioni 300, hiyo ni hatua kubwa sana na tuangalie hiki kinachopatikana kwa Mashirika ya Umma hatua imepigwa na kwa kiasi fulani tukiyaendeleza Mashirika ya Umma na ikiwa kwa mfano, kama anatoa gawio namna kama hii, nina uhakika kwamba kodi zetu zitashuka kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja bajeti zetu zote mbili Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Bajeti ya Uwekezaji na Mipango. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Zacharia Issaay, ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali yetu kwa Awamu hii ya Sita, pia na huu Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 Juni juzi baada ya Waziri wa Fedha kuwasilisha taarifa ya bejeti, jalada maarufu Afrika linaitwa *Business Inside Africa* walitoa taarifa yao wakionesha mafaniko katika Mataifa ya Afrika ambayo yanakwenda vizuri kiuchumi, waki-*refer* namna ambavyo bajeti za nchi hizo zinakwenda kusaidia wananchi na namna ambavyo bajeti zilizokwisha zilifanya vizuri. Sasa nina takwimu hapa ya baadhi ya nchi za Afrika ambapo tuweze kuona na sisi namna gani Taifa letu linakwenda, halafu niende kwenye hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walianza wakatoa Afrika Kusini wakasema kwamba bajeti yao ni ya dola bilioni 141.4, *Algeria* dola bilioni 126, Misri dola bilioni 91, Morocco dola bilioni 76, Angola dola bilioni 37.8, Nigeria dola bilioni 36.7, Kenya dola bilioni

32.6, Libya dola bilioni 26, Ivory Coast bilioni 25.2, Tunisia dola bilioni 25.1 na sisi Tanzania dola bilioni 21.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa sana kwa Taifa letu, kutoka kwenye nchi ambazo zilikuwa chini sana, lakini sasa hivi angalau tunaingia mpaka kwenye machapisho ya kidunia na kuonyesha kwamba uchumi unakwenda vizuri. Hongereni sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita, hongera kwa Waheshimiwa Mawaziri ambao wanaomsaidia kazi Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli hakuna namna katika uchumi, namba zinaongea, ili namba ziongee lazima wafanye kazi. Serikali ya Awamu ya Sita wamefanya kazi kubwa sana, hongera sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ambayo tunasema ni miradi ya kielelezo. Ni miradi ya mfano, imefika hatua sasa hivi hata Marais wa Mataifa ya nje mfano wakija, kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma wanatumia treni ya *SGR*, ni mfano mkubwa sana, ni *branding* kubwa ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika hatua sasa hivi tuna *stability* ya umeme, *energy* nchini, kiasi kwamba ile biashara umeme ukikatika watu wanapiga kelele na ukirudi wanasema huoo! Tumeshaanza kuisahau kama Tanzania. Hongera sana kwa Serikali yetu, hongera kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Rais wetu kwa miradi ya huduma za kijamii. Asubuhi nilikuwa nasikiliza taarifa ya Naibu Waziri wa TAMISEMI. Tumejenga zahanati zaidi ya 1,000 nchini, tumejenga vituo vya afya zaidi ya 400, tumejenga majengo kwenye hospitali za rufaa, hospitali za kanda, vifaatiba, vifaa vya kusaidia huduma za uendeshaji wa afya, haya ni mafanikio makubwa. Kwa namna yoyote huwezi kuwa na Taifa linaloendelea bila kujali ustawi wa wananchi wako, hongera sana

kwa Serikali yetu, tunawashukuru na tunawapongeza, wametufanyia kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa miradi ya miundombinu ya kiuchumi. Sasa hivi mawasiliano kila sehemu utakapokwenda ukisafiri, huwezi ukatembea zaidi ya dakika tano kwamba hauko kwenye mtandao wa mawasiliano, hii ni hatua kubwa sana ambayo Mheshimiwa Rais amefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga barabara, tumejenga madaraja. Wamesema Mheshimiwa Makoa na Mheshimiwa Haji. Tumejenga kila aina ya miundombinu kurahisisha uchumi wa nchi na ndiyo namna ambavyo uchumi utapaa. Huwezi eti ukategemea uchumi unapaa, unasafirisha mazao kutoka kijijini kwenda kwenye sehemu ya uzalishaji yanatumia wiki mbili. Sasa hivi unatoka Mwanza, leo mtu anatoka Mwanza jioni kesho yupo Kariakoo anahemea bidhaa, keshokutwa jioni yuko Mwanza amerudi kufanya biashara. Ndiyo uchumi unakwenda hivyo. Hii ndiyo *modern economy* ambayo tunaihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mawaziri wamemsaidia sana Mheshimiwa Rais. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mwalimu wangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Kaka yangu Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, wamemsaidia Mheshimiwa Rais pamoja na Watendaji wao wa Wizara zao, tuwapongeze sana, akiwepo na Mheshimiwa Naibu Waziri Nyongo ambaye ametoka, wamemsaidia Mheshimiwa Rais. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya ziara ya kuelezea taarifa ya utekelezaji Ilani Jimboni mwezi uliopita. Kila Kata unayofika wanakutolea taarifa Mheshimiwa Diwani au Mtendaji wa Kata ni mabilioni yamefika kwenye Kata zao, hili jambo siyo la kubeza na siyo jambo dogo. Wanakwambia tulikuwa hatujawahi kuona hela zinashuka kwa utaratibu huu, lakini ndiyo namna ambavyo wamefanya kazi Serikali ya Awamu ya Sita na wao

kama *cabinet* tunawapongeza sana kwa kazi nzuri. Hongera, waendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo takribani saba ninataka niongee jioni hii, lakini kwa asilimia kubwa ni *success stories* ambazo Serikali imefanya na sehemu ambayo ni ya kutoa ushauri, basi tutatoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ningependa kuchangia ni ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, *(Public-Private Partnership)*. Tumeanzisha kituo cha ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma na kinakwenda vizuri na ndiyo eneo moja ambalo pia litatusaidia sana kwenye uwekezaji wa miradi mikubwa. *Mega project* hatuwezi kuendelea kutumia tu fedha za Serikali, kwa hiyo, ninawapongeza Serikali, katika hili eneo na hiki kituo chenu kinakwenda vizuri, sasa, niwashauri jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo inaonekana, bado taasisi nyingi zinaingia ubia na wawekezaji kwa kutumia sheria za taasisi husika na kwa kutumia utaratibu wa taasisi husika. Kwa kuwa, wameunda kituo kwa ajili ya kuratibu hili zoezi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yako tunaomba waweze kuwasaidia, Mheshimiwa Waziri pia wa Uwekezaji waweze kuwasaidia ili jambo liweze kwenda vizuri, kuwe na *coordination* nzuri ya kuhakikisha tunapata ubia na sekta binafsi na kusaidia katika uendeshaji wa miradi mingi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ningependa kuchangia jioni hii ni uendelezaji wa rasilimali watu, *human capital development*. Kiukweli kama Serikali wamefanya makubwa upande wa sekta ya elimu, afya, pia hata na lishe, ndiyo maana hata kwenye mbio za Mwenge wa Uhuru tumeweka kipengele cha kuangalia suala la lishe. Hakuna namna Taifa litaendelea watu wake ni goigoi, hapa Serikali wamefanya hatua kubwa, tuwapongeze na waendelee kutilia mkazo ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 – 2050. Kiukweli maandilizi ni mazuri na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo tukupongeze katika kulisimamia hili jambo, wamelisimamia vizuri sana. Sasa, kuna jambo ambalo lazima tufanye *branding* ya nchi, mambo mawili. Kwanza ni urasimu. Katika Dira yetu ya 2025 – 2050, tuonyeshe kabisa kama nchi tuko *serious* kwenye suala la urasimu kwa maana ya *bureaucracy*, lakini pia na suala la rushwa, *corruption free zone*. Tuna taasisi yetu ya kupambana na rushwa inafanya kazi vizuri sana, lakini lazima tui-*brand* nchi, tusiwe tunatolewa mfano, Mataifa mengine ya jirani ambayo nisingependa kusema. Wanakwambia mwekezaji akifika, ndani ya masaa 24 ameshapata vibali vya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianzisha hizi *One Stop Centre* kwa lengo la kurahisisha na kupunguza urasimu, ninaomba walisimamie hili ili tuvutie wawekezaji kwa wingi sana ili Taifa letu liweze kukimbia na kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ningependa kuchangia ni suala la nishati, upande wa umeme kama nilivyosema awali *stability* inaonekana, lakini kuna upande wa *petroleum* na kuna upande wa gesi. Kwa upande wa umeme ninawashauri, kwa kuwa sasa hivi mwelekeo wetu ni kwenda kwenye ngazi za vitongoji, Serikali waje na mfumo ambao tungependa wengi tuna ushauri wa namna ya wananchi kuunganishiwa, lakini malipo yapatikane kwenye *tariff* moja kwa moja ili tujikute kwamba umeme, unafika kwenye vitongoji lakini pia wananchi wengi wanaunganishiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi wengine wanashindwa kuunganisha kwa sababu wanakosa hela ya papo kwa papo na ya moja kwa moja. Kwa hiyo, watakapowaunganishia umeme wananchi, lakini ile gharama inaenda kuanza kukatwa kidogo kidogo kwenye gharama ya *tariff* anazokuwa analipia zile bili zake mpaka deni lake linakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *petroleum,* nadhani wana wataalam wa watu wa *risk*. Sasa hivi *Middle East* kuna mgogoro

umeibuka, Iran na Israeli, nadhani hili wanaweza wakalifanyia kazi kwa kuli-*foresee* mapema. Kunaweza kukatokea changamoto ya mafuta mbele ya safari, miezi mitatu ijayo mbeleni, kwa hiyo, kama Serikali waliangalie mapema, waangalie namna ya kulidhibiti. Hata hivyo, ninawapongeza, *stability* ya mafuta pia nchini imetulia, *petroleum* sasa hivi imekuwa siyo usumbufu sana, tunaona tunakwenda vizuri, ile biashara ya kupanga foleni kwenye vituo ya kununua mafuta, ninaona kwa sasa imekatika nchini. Hongera sana kwa hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gesi, kwenye suala la gesi ushauri wangu ni mmoja. Wamefanya vizuri sana katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi na *distribution* imefanyika nchini. Sasa, *refilling* ile pale kwa sasa mwananchi lazima anunue ule mtungi, Serikali waanze kuja na namna waangalie namna ya kuwa na vituo vya hizi gesi za matumizi ya nyumbani kwa ajili ya kufanya *refilling* na mtu auziwe kwa ambaye anataka kilo moja, anayetaka kilo mbili, anayetaka kilo tatu, siyo lazima mpaka mtu anunue mtungi mzima. Ninasema hivi kwa sababu kulingana na hali ya uchumi wa wananchi wengine wanashindwa kununua mtungi mzima kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya barabara za vijijini, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kiukweli katika eneo moja ambalo alitutendea haki Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili ni kuamua kwamba fedha za barabara zije kwenye Majimbo yetu moja kwa moja. Tofauti na awali unakuta zinakwenda Mkoani, Wilayani, kama wana Majimbo mawili au matatu wanaanza kugombania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa unaletewa fedha kwenye jimbo lako, wanapanga vipaumbele kwa kushirikiana na Meneja wa *TARURA* wa wilaya husika. Niwashauri Serikali, kwa kuwa uchumi wetu unaimarika na mapato yanaongezeka, basi tutakapoanza Bunge lijalo angalau kwenye fedha ya barabara *at least* kila jimbo lipate hata shilingi bilioni tano. Hizi zitatusaidia sana kuboresha barabara na tutajenga madaraja mengi na zaidi itasaidia sana katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma la kifedha; *transaction* nyingi kwa sasa zinafanyika kwenye mitandao ya simu. Kuna changamoto moja ambayo bado ninaona wanaweza wakaifanyia kazi Wizara ya Fedha na hii ni kwa ajili ya *financial inclusion*. Mwananchi anapokosea kutuma fedha kwa bahati mbaya au anatuma kwenye namba ambayo siyo, inachukua muda mrefu sana mpaka zile kampuni za simu kurudisha zile fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua hili jambo ni la Wizara ya Mawasiliano, lakini kwa kuwa linahusiana na masuala ya kifedha kwa ajili ya *financial inclusion* ambayo tumekuwa tukiipigia chapuo muda mrefu, basi angalau muda wa fedha mtu akisha-*confirm* kwamba nilituma fedha kimakosa, ndani ya saa moja au mbili awe amerudishiwa fedha zake aweze kuendelea na mambo mengine na siyo kusubiri mpaka saa 24. Wakati mwingine saa 24 zinafika lakini fedha zake hazijarudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la saba ni suala la kilimo, mifugo na uvuvi. Hapa nitaongelea suala la usalama wa chakula *(food security)* na mapinduzi ya kijani. Katika nchi yoyote pia suala la usalama wa chakula ni kipaumbele, kwa maana ya kwamba utulivu wa nchi lazima kuwe na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyoona *trend* inaonesha kwa hii miaka miwili kumekuwa hakuna njaa nchini pamoja na changamoto mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi na hii ni kwa sababu ya mikakati ya kiserikali waliyowekeza katika suala la kilimo. Kilimo cha umwagiliaji kimeweza kusaidia sana na ruzuku zimeweza kusaidia sana wakulima na hatimaye kama Taifa tunakwenda vizuri na utulivu upo kwa sababu kuna chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, mwaka 2000, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, wakati anakamilisha hotuba yake ya kuzindua Dira ya Maendeleo ya Taifa alisema kwamba *"let us get forward building Tanzania a winning Nation"*. Hii ndiyo maana yake kwamba tunapambana kujenga Taifa letu lisonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza nimshukuru *Allah Subhanahu Wa Ta'ala* kwa kutujaalia uzima na salama. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Naibu Waziri na timu yao nzima ya Makatibu Wakuu, hasa dada yangu Bi. Amina Shabani ambaye pia ni Mwalimu wangu wakati anafanya kazi kule Kilimo Zanzibar. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri na kama walivyosema wenzangu sina haja ya kuyarejea, lakini kazi inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mtiririko wa mapato na matumizi upo vizuri na hapa nitangulize ombi langu kwanza, Mheshimiwa Waziri la muhimu zaidi kwa sababu miradi ile mikubwa ya kimkakati umeikamilisha, sasa ningeliomba tu uende katika miradi ya huduma ambayo ndiyo inagusa sana wananchi na ndiyo inatengeneza utu wao. Sasa akaziangalie Wizara ya Afya na Wizara ya Maji. Hizi ni wizara muhimu kwa sababu zinagusa utu wa mtu na vijana wetu au wazee wetu wanapata shida hasa wale wanyonge kutokana na matatizo ya kihuduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu sasa hivi ukienda kwenye hospitali za Serikali hazina tofauti na hospitali za *private*. Gharama zipo vilevile na wananchi wetu wale wa kipato cha chini wanasumbuka sana. Kwa hiyo, ningeliomba tu, tumefanya kazi vizuri katika miradi ya kimkakati ikiwemo *SGR*, Bwawa la Mwalimu Nyerere, daraja lile ambalo kesho au ni leo Mheshimiwa Rais anaenda kulifungua. Sasa tuhamie kwenye huduma za wananchi ili tupunguze makali ya maisha ambayo yanawasumbua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye uchumi wenzangu wachumi wamezungumza vizuri sana. Sasa kwa harakaharaka niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais (mhifadhi nambari moja) kwa kazi kubwa ambayo ameifanya hasa katika Sekta ya Utalii, Sekta za Uhifadhi na Sekta za Kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kwenye Sekta ya Utalii na Uhifadhi wa Mazingira tutaona kuwa Mheshimiwa Waziri, katika Awamu hii ya Sita amefanya mambo makubwa sana. Jambo la kwanza, tumeona kwamba wakati hata mimi nilikuwa ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii, nilipochungulia Ilani ambayo akina Mheshimiwa Dkt. Bashiru hapa walikuwa wameitayarisha vizuri, wakawa wameweka lengo la watalii wafikie milioni tano kutoka milioni moja mwaka 2020, nilisema hili haliwezekani. Leo tunavyozungumza hapa watalii wameongezeka kutoka 1,100,000 mwaka 2020 na kufikia 5,360,000 mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ongezeko kubwa sana ambalo halikutegemewa. Pia, mapato yameongezeka kutoka dola milioni 715 hadi dola bilioni 3.9. Haya ni mabadiliko makubwa ambayo hatukuyatarajia. Kwa hiyo, tuwapongeze sana hasa Mheshimiwa Rais, kwa sababu haya hayakuja kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika tumeona mabadiliko makubwa kama tunavyojua kwamba sasa hivi Mbuga yetu au Hifadhi yetu ya Taifa ya Serengeti kwa mwaka wa tano mfululizo kuanzia mwaka 2019 mpaka huu mwaka 2024 imeendelea kuwa ni kinara na mshindi wa Hifadhi bora duniani kwa miaka mitano mfululizo. Hili huko nyuma hatukulitegemea lakini halikuja kwa bahati mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania pia imekuwa ni nchi ya tisa duniani kwa vivutio na nchi ya tatu Afrika na imekuwa ni miongoni mwa nchi ambayo ina vivutio muhimu zaidi au vizuri zaidi *(Africa leading destination)* ukiangalia katika nchi za Afrika ambapo Tanzania ndiyo inaongoza. Hii haikuja kwa bahati mbaya na nimeanza haya kwa sababu kama tunavyojua kwamba haya yamekuja kwa sababu ya utayari wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amehudhuria yale makongamano ya kimataifa, lakini pia ameshiriki mwenyewe katika filamu ya *Royal Tour* na *Amazing Tanzania*. Pia, fedha za UVIKO-19 zimepelekwa nyingi katika hifadhi zetu kwenda kutengeneza miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege pamoja na makazi kwa ajili ya watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ndiyo sababu kubwa kwa nini Sekta ya Utalii na Maliasili imeweza kuimarika vizuri na kuleta mapato haya ambayo tumeyaona hapa. Sasa mawazo yangu au ushauri wangu Mheshimiwa Waziri, twende tukaisaidie Sekta ya Utalii na Sekta za Uhifadhi kwa kujenga *capacity* na kuwa na taasisi bora ambazo zitaweza kufanya kazi vizuri zaidi pamoja na fedha. Kama tunavyojua kwamba hifadhi zimekuwa zikilalamika kwamba mtiririko wa fedha kwenye hifadhi zetu sio mzuri toka tulivyofanya mabadiliko ya kifedha na kuondosha *retention* katika hifadhi zetu. Hifadhi kidogo zinasuasua na hazifanyi kazi vizuri kama ilivyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika *capacity* ya *institution* zetu au taasisi zetu. Tumekuwa tukilalamika hapa au tukishauri mara nyingi kwamba ni vyema kama ingewezekana Taasisi kama ya Misitu ile ilikuwa ikiitwa Wakala wa Misitu Tanzania tungeweza kuipandisha hadhi na kuwa mamlaka na ingeweza kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAWA* pia tungeweza kuipandisha hadhi na kuijengea uwezo na kuipa nguvu zaidi kukusanya mapato basi pia ninafikiri zingefanya kazi vizuri zaidi. Hii ni kwa sababu kama tunavyoona ukiangalia makusanyo *TRA* wamekusanya 91%, lakini hizi sekta kama taasisi zetu hizi wao wana 77%. Maana yake ni kwamba uwezo wao wa ukusanyaji haupo vizuri. Sasa kama tutazijengea uwezo, zitakuwa na *capacity* kubwa ya kuweza kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka huko nije sasa moja kwa moja kwenye suala zima la mabadiliko ya tabianchi. Wakati Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, anawasilisha bajeti hapa alizungumza kwamba changamoto kubwa ya sekta zetu za kiuchumi na za

kihuduma ni masuala ya mabadiliko ya tabianchi na mkakati wa mabadiliko ya tabianchi amezionesha zile *vulnerable sectors* ni miongoni mwa Sekta za Miundombinu, Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni sekta ambazo zitapata shida sana kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Sasa tufanye nini? Lazima twende tukajenge wigo mpana wa kuzijengea uwezo. Kwanza sheria tumebadilisha majuzi lakini zile sheria kama tulivyozungumza kwamba mabadiliko yalikuwa ni madogo sana. Sasa ni vyema tukakaa kitako na tukamshauri Mheshimiwa Waziri, ambaye anashughulika na masuala ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi akaja akaleta Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge hili hakufanikiwa, alete Bunge linalokuja sheria ambayo itakuwa ni *comprehensive* ambayo itaonesha hasa masuala ya fedha za mabadiliko ya tabianchi kwa sababu mpaka sasa hivi sheria inazungumza kwamba uwepo wa Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi lakini Mfuko ule hauna pesa, upo tu jina. Sasa ni vyema tukaujengea uwezo ule mfuko ili ukaweza ku-*attract funds* zaidi kuliko ilivyo hivi sasa ambayo inategemea zaidi Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fursa pia ambazo zingeweza kupatikana kama tungekuwa na taasisi madhubuti. Mfano taasisi kama *NEMC* tungeijengea uwezo tukaipandisha hadhi na kuwa mamlaka ingeweza kuwa na nguvu zaidi ya kuweza kukusanya fedha na kuweza kushauri kusimamia Sekta za Uhifadhi kuweza kuzalisha zaidi nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeliomba tu kwamba tuijengee uwezo *NEMC,* tuibadilishe iwe mamlaka ili iweze kuwa na nguvu zaidi za kuweza kutengeneza au kuzalisha fedha zaidi hasa kuzishughulikia fedha za mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano, sasa hivi Tanzania kuna huu Mfuko wa *Green Climate Change Funds*. Huu Mfuko kuna nchi kama Kenya wanaratibu *institution* tatu ambazo tayari zimeshakuwa *accredited*. Ukienda Nchi kama Senegal wana karibu *institution* mbili ambazo tayari zimeshapata *accreditation* ya *Green Climate Fund*. Pia, ukienda

Nchi kama Afrika Kusini wana *institution* au taasisi karibu mbili ambazo tayari zimeshapata *accreditation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Tanzania tuna taasisi moja na hii tumshukuru sana tumpongeze Mheshimiwa Muyungi kwa jitihada zake binafsi za kuweza kupata *accreditation* kwa taasisi ya *CRDB* angalau miaka mitano iliyopita. Sasa ningeliomba sana tuijengee uwezo *NEMC* iwe na uwezo mkubwa iweze ku-*compete* na kuweza kutengeneza uwezekano wa kushughulikia hii Mifuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mifuko mingi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo sidhani kama Tanzania tumeishughulikia vizuri. Kuna hiyo *adaptation fund*, kuna *Green Climate Fund*, kuna *window* hii ya *IMF* ambayo inahusika na masuala mazima ya *resilience and sustainability facility* na kuna *funds* nyingi ambazo kama tutakaa vyema kuweza kuzishughulikia hizi *funds,* basi tutaweza kupata fedha za ziada kushughulikia katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *institution* ambazo tayari zilishaanza *accreditation* kama TAMISEMI, *NEMC*, Wizara ya Fedha na kule Zanzibar *(People's Bank of Zanzibar),* lakini hakuna hata moja huu mwaka wa 10 ambayo imefanikisha hili; kwa sababu gani? Hatuna taasisi madhubuti ya kuzisimamia hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeliomba na hili tukasaidie kuzisimamia taasisi zetu hizi za Uhifadhi wa Mazingira ili ziweze kuwa *serious* na kuweza kushughulikia hizi fursa za fedha za mabadiliko ya tabianchi. Halikadhalika .... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa muda. Nilikuwa nina mengi lakini ningependa kumalizia tu kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Donge kwa kuweza kushirikiana na katika miaka mitano iliyopita na ni mategemeo yangu *Insha Allah* kwa mambo ambayo tumefanya pamoja na wao watanipa muda zaidi tuweze

kuendeleza jitihada zile ambazo tumezifanya katika mitano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kheri ambayo ametupa muda huu wa kuweza kujadiliana bajeti yetu hii, lakini pia kwa kumaliza hii miaka mitano mingine ambako sisi Wabunge sasa tunafikia hatua ya mwisho ya miaka mitano ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa iliyofanyika katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kazi imefanyika. Kila Mbunge ni shahidi kwenye eneo lake kwani miradi mingi ya maendeleo imepelekwa lakini hata utulivu wa nchi upo kwa sababu maendeleo yanatokana na amani, mshikamano na mtangamano wa kisiasa katika nchi yoyote kwa maana ya kukubaliana na nchi inakuwa tulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pia pongezi nyingi kwa Serikali kuanzia Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri pamoja na vyombo vingine vyote vya dola kuanzia ngazi ya Taifa, ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya kwani kazi kubwa imefanyika. Nchi hii ni kubwa sana kwa jinsi ambavyo mahitaji yanakuwa makubwa. Yaliyofanyika katika miaka mitano hii ya awamu ya pili kwa kweli ni makubwa na kwamba hatukutarajia. Mimi ni mfano, katika Jimbo la Mbulu Mjini kuna miradi ilikuwa tunashindwa hata kuahidi wakati wa Ilani, lakini sasa imetekelezwa na kazi kubwa imefanyika kwa kila jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Kamati zetu zinatembea mikoani zinaona miradi mingi inayotekelezwa na mafanikio yanayoonekana, kwa vyovyote vile nchi inahitaji mahitaji makubwa na kila mwaka yanaongezeka kwa sababu bado tunaongezeka, lakini pia na kadri ambavyo uwezo wa Serikali unakuwa mdogo kulingana na mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kwa namna ya pekee kuona kwamba mafanikio haya yaliyopatikana yamechochea mahitaji mengine mapya. Kwa mfano, tulipojenga miundombinu ya afya (tumejenga miundombinu ya afya nchi nzima), tumepeleka rasilimali nyingi nchi nzima ikiwemo miundombinu ya majengo lakini pia rasilimalifedha, rasilimali watumishi na vitendea kazi. Hata hivyo, kwenye Sekta hii ya Afya mimi mchango wangu ulikuwa sehemu hii ya huduma ya makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo langu nimekuta mambo mengi ikiwemo kundi la akinamama wajawazito na watoto, kundi la wazee na kundi la walemavu. Eneo hili Serikali itazame upya namna ambavyo huduma ya afya kwao itapatikana kwa sababu unaweza kukuta huduma ya afya ya mama na mtoto au mama mjamzito inahitaji gharama kubwa hailingani na uwezo wa yule mama au yule mzazi ambaye amefika kwenye huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu hiyo kubwa ni kwamba uwezo wa Serikali ni mdogo. Tukitazama upya eneo hili litasaidia. Pia, hata tukizungumza eneo la kuzungumza kwamba labda tutegemee bima ya afya kwa wote, bado Watanzania wa chini waliowengi, uwezo wao utashindwa kufika hapo. Kwa hiyo, eneo hili Serikali itazame upya, lakini pia tuone namna ambavyo huduma hii inaboreshwa kwa makundi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni miradi ya maendeleo. Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Jimbo la Mbulu Mjini tumenufaika sana, lakini Mradi wa *TACTIC* una miaka minne tukiusubiri (kwa hali na mali tunategemea huo mradi wa soko, stendi, dampo na machinjio). Fedha zake ni nyingi sawa, lakini

kwa sababu tulipokuwa tumetembea kamati zetu mikoani tulikuta baadhi ya Miradi hiyo ya *TACTIC* katika miji mikubwa imechelewa sana katika utekelezaji kwa maana ya wakandarasi tunaowaweka hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokwenda Shinyanga Mkandarasi yupo nyuma ya muda kwa muda mrefu katika Mji wa Kahama, lakini fedha zipo, ni yeye tu hatekelezi kwa wakati. Hali hiyo inasababisha mwisho wa siku miradi inayofuata kwenye awamu nyingine inakwama na kwa sababu hiyo uteuzi ule wa wakandarasi ungetazamwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyokuwa tumeikuta kule Kahama na maeneo mengine wanayofanya wazungu au wachina tulikuwa na uwezo wa wakandarasi wetu kufanya. Ninadhani ifike mahali tuangalie miradi ambayo wakandarasi wazawa watafanya na yale ambayo mkandarasi wa nje atafanya kulingana na uwezo ulivyo ili walau miradi hiyo ya maendeleo na mpango huu wa maendeleo uweze kufanikiwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa hasa *World Bank* wanapotoa fedha, wakiona fedha za miradi ya awamu ya kwanza haijaweza kukamilika kwa wakati basi miradi ya nyuma inachukua muda mwingine tena. Kwa hivyo, wale wahisani na wafadhili wa miradi hiyo ya maendeleo wanakuwa wanasuasua kutoa zile fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo pia nilichojifunza ni kwamba huu mradi wa maboresho ya miji Tanzania ambapo Mbulu tunatarajia kupata soko, stendi, dampo na machinjio pamoja na lami kilometa 12 katika Mji wa Mbulu, inaonekana hata sasa ilikuwa muda wa manunuzi ni muda huu wa kwamba kazi za manunuzi zitafanyika lakini bado mpaka sasa haijaanza. Ninaomba kipindi hiki cha manunuzi kianze katika mwaka huu wa bajeti shughuli ianze mwezi Julai kama tulivyotarajia ili miradi hii itekelezwe kwa wakati na iweze kuleta tija kwa Wanambulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi viporo na kwa sababu hiyo miradi viporo inavuruga bajeti yetu kadri tunavyopitisha

hapa. Kwa mfano, mradi usipokamilika mwaka ule wa kwanza tukaingia mwaka wa pili wa mradi, kwa vyovyote vile ile bajeti tuliyopitisha inaenda kukamilisha ule mradi kwa sehemu na mradi ule ambao tunatekeleza kwa wakati huo wa mwaka wa bajeti utakuwa umerudi nyuma tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini? Ni kwamba Serikali iangalie utaratibu wa miradi yote iliyowekezwa iwe Serikali na ama iwe wananchi kwa maana hata yale maboma tuliyoomba tunaomba sana Serikali itusaidie katika eneo hilo. Pia, miradi hii viporo inagusa miradi midogo ya fedha kidogo na miradi ya fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu. Yule Mkandarasi wa Mbulu - Garbabi amerudi sasa hivi yupo *site,* lakini tunamwomba sana ajitahidi namna ya kumalizia ile hela ili tuweze kumsimamia vizuri aweze kukamilisha ule mradi kwani sasa hivi anajenga makalavati na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi alitelekeza ule mradi kwa mwaka mzima. Sasa kadri ambavyo ametelekeza kwa mwaka mzima zipo athari zimejitokeza (ama athari kwa upande wa Serikali na athari kwa upande wake pia). Ninashauri kama itawezekana fedha zile alipwe halafu aandikiwe barua mahususi ya kukamilisha huo mradi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa sababu hawa wastaafu waliokuwa wanapokea shilingi 100,000 na kitu Serikali imeongeza mpaka shilingi 250,000. Hatua hiyo ni kubwa kwa sababu hao wazee wana mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho pia za Wenyeviti wa Mitaa ambazo wanaelekeza zilipwe na Halmashauri. Halmashauri nyingine hazitaweza, wala tusifichane hapa. Halmashauri ya Mbulu Mjini kulipa posho za Wenyeviti wa Mitaa, wa Vijiji na hata Vitongoji haitaweza. Ninaomba Serikali itazame mapato ya Halmashauri ili iweze kuona namna ambavyo malipo haya ya viongozi wa ngazi za chini yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Jimbo kwa upande wa barabara pia kwa sasa zimesimama, hatujapata, lakini fedha hizi za Mfuko wa Jimbo tulikwenda sisi Wabunge tukaahidi barabara kwenye maeneo yetu, hadi sasa wala hazijapatikana. Ninaomba fedha hizi zipatikane, ili ahadi zetu zitekelezwe, ili maeneo yale ambayo yalilengwa yaweze kupata huduma, kadri ambavyo inawezekana kwa jinsi ambavyo fedha hizi zitapatikana kwa sababu, tulishaahidi. Zile barabara bado ni madeni kwetu sisi kwa kuwa, awali ilikuwa ni fedha ziko za Mfuko wa Barabara, kwa ajili ya kutusaidia sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua jukumu kubwa sana, fedha hizi zinagusa *TARURA* kwa maana ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini. Kwa namna ya pekee *TARURA* wamefanya kazi kubwa sana nchini, barabara zilizofunguliwa kwenye majimbo yetu ni nyingi. Ombi langu kwa Serikali ni fedha ya *TARURA* ya miradi ya maendeleo iongezwe na pia, zile za Mfuko wa Jimbo zipatikane, ili walau Mbunge akienda mahali, kuna jambo ambalo ni gumu sana, basi ile hela atakapoahidi mradi ule utekelezwe na uweze kuleta tija. Barabara ambazo zimefunguliwa na *TARURA* ni zaidi ya 70% ya zilizokuwepo. Sasa kwa sababu bajeti yao ni ndogo wanashindwa kutekeleza kwa jinsi ambavyo inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya viongozi wa Serikali. Wakati Mheshimiwa Makamu wa Rais alipofungua Daraja la Magara kule Mbulu, katikati ya Babati na Mbulu, aliahidi Barabara ile ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu. Hatua kubwa imechukuliwa, ninaipongeza Serikali imejenga sehemu kubwa ya mlima kwa zege, lakini pia, mchakato wa kutafuta fedha za usanifu wa awali tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Mlima Magara katika Jimbo la Mbulu Mjini, kwa Mawaziri tulioenda kwenye ziara walikuwa wananiuliza Mheshimiwa hakuna njia nyingine ya kupita? Njia yako ni hii? Nikawaambia kwa kweli, njia yangu ni hii na ndiyo barabara yetu. Serikali imefanya kazi kubwa, wakati inaingia hapakuwa na daraja, hapakuwa na zege, barabara ile mvua moja tu ikinyesha inaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba, kwa kuwa, usanifu na kazi za awali tayari, zinazotafutwa ni fedha, ili *tender* itangazwe, barabara hiyo ijengwe kutoka Mbuyu wa Mjerumani kwenda Mbulu. Ninaomba, kama itawezekana, utekelezaji wa barabara hii Serikali iweze kuusogelea kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Kwa hivyo, hatua ile iliyochukuliwa ninaishukuru Serikali kwa sababu, bado ni kubwa, sehemu kubwa ya zege imekamilika na miradi inaweza ikachochea uchumi wa wananchi. Barabara hiyo inatuunganisha sisi na Mikoa mingine ya Kanda ya Kaskazini pamoja na Mji wa Babati ambako ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa maji, asubuhi niliuliza swali hapa. Huu mradi ni wa fedha nyingi, ninashukuru Serikali imeuweka kwenye mpango. Ni mpango ambao unaweza ukatekelezeka kwa sababu, bado uwezekano wa kupatikana kwa fedha upo na Mheshimiwa Waziri wa Maji alishaniambia atapata fedha. Kwa hivyo, kwa Mwaka huu wa Bajeti 2025/2026, utekelezaji wake uweze kuanza, huu Mradi wa Nambis, Tarafa nzima haina maji, lakini walikuwa na maji ya asili ambapo, kwa sasa vyanzo vile vimeanza kupotea na wananchi wanatafuta maji, kwa hivyo mradi huu utatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache ninasema pia, tumejenga *VETA* nyingi na *FDCs,* lakini ninadhani hao vijana wanaosoma kwenye vyuo vya ufundi na shule za amali hebu tutazame maeneo hayo ya vyuo. Wanafunzi wanapomaliza tutafute namna ambavyo wanaweza kuwa na mtaji na vifaa kwa fani waliyosoma, ili walau wakishamaliza wasirudi tena mitaani. Kujenga Vyuo vya *VETA* na *FDC* ni jambo jema, lakini pia, kuwatafutia namna ambavyo wanakuwa na vifaa ni jambo jema. *(Makofi)*

Meshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwa uchache, niseme tu kwamba, kwenye eneo hili nizungumzie suala la umeme. Alizungumza mchangiaji wa awali, katika Jimbo la Mbulu wanakosema ni mji wetu eneo kubwa ni vijiji kwa hiyo, wananchi wengi hawawezi kuingiza umeme kwa shilingi 300,000 na *wiring* shilingi 300,000 jumla shilingi 600,000. Ninaona Serikali itazame

eneo hili kwa majimbo yote nchini, ili ione namna ya kuweka utaratibu mzuri wa umeme kupokelewa na wananchi, sasa hivi maeneo mengi wananchi wanaangalia tu umeme upo, lakini uwezekano wa kupata shilingi 700,000 unakuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii kwa kweli, tukiweka utaratibu ambao watalipia kidogo kidogo ama kwa namna ya kuweka kwenye… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha. Muda wako umeisha, tafadhali.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mengine nitachangia kwa maandishi siku zijazo. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuiendeleza, kusimamia na kuiongoza nchi yetu. Ameonesha maono makubwa sana, ameonesha hekima na busara, lakini ile falsafa yake ya *4R* kwa kweli, imeiweka nchi katika nafasi nzuri sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninampongeza sana kwa miradi ya kimkakati kwa namna ambavyo ameweza kuitekeleza. Ni miradi ambayo imechangia kwa kiwango kikubwa kuinua uchumi wa nchi yetu; tumeona jinsi *SGR* ambavyo imepokelewa na wananchi na mchango wake katika uchumi wetu. Tumeona Bwawa la Nyerere, lakini kesho atakuwa anafungua lile daraja kubwa la Busisi kule Mwanza ambalo kwa kweli, nalo linaunganisha ile mikoa, linatoa mchango mkubwa sana na miradi mingine mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, amefanya na anaendelea kufanya kazi kubwa sana. Ndiyo maana naamini Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), walipokutana Mwezi Januari wakaamua kwa kauli moja kwamba, awe ni Mgombea pekee wa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu ya kazi nzuri ambayo ameifanya. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia kwa kutuletea miradi mingi mizuri kwenye Jimbo langu la Vwawa. Ameleta miradi mingi sana, kwenye upande wa elimu tumeona shule kadhaa zimejengwa, zaidi ya sita ni mpya, zikiwepo za kidato cha tano na sita, Pamoja na shule ya mfano ambayo ametupa shilingi bilioni nne inafanya kazi, kwa kweli, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametuletea Chuo cha Mkoa cha *VETA*, kinajengwa na karibu kinakamilika. Nina imani kabisa kwamba, hela zikitolewa kikakamilika, kitatoa mchango mkubwa sana katika kuwaandaa vijana wetu kupata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kujitegemea na kuchangia katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi ametupatia tena fedha shilingi milioni 250, kwa ajili ya kujenga kituo cha afya na katika vituo vingine vya afya ametupatia magari ya wagonjwa, tunampongeza sana. Zaidi ya hapo barabara ile ambayo ilichaguliwa, kwa ajili ya kujengwa na wakandarasi wanawake, ili kuhakikisha kwamba, wanajengewa uwezo kwa kweli, ameridhia na mikataba imesainiwa juzi. Tunamshukuru sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ninaamini atai-*support* sana hii Barabara, wale wakandarasi wanawake waijenge kwa wakati, waoneshe uwezo wao, ili kusudi iweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ya umeme na mambo mengine, ninawapongeza Mawaziri wote wawili; Waziri wa Fedha ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Profesa Kitila, Manaibu wenu na Watendaji walioko kwenye Wizara zenu kwa ujumla wake. Wanafanya kazi nzuri sana na sisi tunaziona, wameisimamia bajeti vizuri na mipango

mizuri sana ya maendeleo wameitengeza. Kwa kweli, sisi kazi yetu ni kuwapongeza kwa kazi wanayoendelea kuifanya na kuwaombea kule wakatakakokwenda, wakati wanaenda kugombea, basi wale wananchi wawarudishe kwa kura nyingi za kishindo na wampe Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia kwenye suala la mfumo jumuifu wa masuala ya fedha. Ni muhimu sana kuhakikisha kwamba, Watanzania wote wanakuwa na akaunti za benki au kwenye mitandao ya simu au kwenye *SACCOS* na maeneo mengine, ni kitu muhimu sana kwa sababu, sasa hivi asilimia kubwa ya Watanzania wamekuwa na simu za mikononi. Ni lazima tuweke mkazo katika kuhakikisha kwamba, wanapopokea fedha, wanapofanya malipo makubwa makubwa, malipo ya kawaida, basi yafanyike kwenye mitandao ya simu na hiyo ndiyo itakayofanya sasa uchumi wetu uweze kuwa ni wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi uchumi wetu kwa maeneo mengi ni ambao ni *informal,* watu wengi wako nje ya mfumo wa fedha. Sasa wakiwa nje ya mfumo wa fedha kwa kweli, namna ya ku-*manage* kuchangia uchumi inakuwa ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pia waangalie zile gharama zinazotozwa na mitandao ya simu na zinazotozwa na benki wakati mtu anapofanya *transaction,* zile gharama zikiwa kubwa zinawafanya watu wengi wasiweke fedha benki wala wasitumie mitandao ya simu na wasiwe katika huu mfumo jumuifu. Kwa hiyo, wakiliangalia vizuri, nimeiona hotuba yako Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amelisemea hilo na ameweka mkazo kwamba, sasa tunapokwenda ni lazima tutilie mkazo katika kuhakikisha watu wengi wanakuwa kwenye mfumo jumuifu wa masuala la fedha, nafikiri litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linaloendana na hilo ni sera ya bima. Tumetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote hiki ni kitu muhimu na tunatoa pongezi kubwa sana kwa sababu, sasa hivi matibabu yamekuwa ni gharama kubwa. Tumefanya

uwekezaji mkubwa wa majengo katika hospitali mbalimbali, vituo vya afya, zahanati na gharama za matibabu ni kubwa. Sasa, ili wananchi waweze kumudu matibabu ni vizuri sasa hii sera, hii Sheria ya Bima ya Afya ianze kufanya kazi mapema iwezekanavyo. Kwa hiyo, tunaomba zile kanuni zinazotakiwa, ili kuhakikisha hii sheria inaanza kufanya kazi zitolewe mapema, kusudi iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya bima ya masuala mengine. Kwa mfano, tulipitisha miaka miwili iliyopita kwamba, mali za Serikali zile za kibiashara ziwe zinakatiwa bima, baadhi ya magari yawe yanakatiwa bima pamoja na baadhi ya mitambo ikatiwe bima. Mheshimiwa Waziri, basi tunaomba ile sera, kama wanaweza wakatuletea zile kanuni zikaja kwa wakati, ili ziweze kusaidia kuhakikisha kwamba, hii sheria sasa inatekelezeka vizuri. Litakuwa ni suala la msingi sana na hii itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu linaloendana na masuala jumuifu ni masuala ya mikopo. Bado kazi ya utoaji wa mikopo kwenye sekta binafsi siyo nzuri sana, kwa hiyo, ninapendekeza mikopo kwenye benki, mikopo ya taasisi mbalimbali, tuielekeze katika sekta binafsi ambayo ndio *engine* ya ujenzi wa uchumi wetu. Sekta binafsi ikipata mikopo itaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuleta uchumi imara katika kujenga mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia, kuchangia suala la umasikini. Watanzania wengi ni masikini na nimeona kwenye hotuba wanasema karibu 26% ya Watanzania bado ni masikini, wapo kwenye umaskini mkubwa, yaani ina maana robo ya Watanzania bado tuko kwenye hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapenda nikumbushe, kule nyuma tulikuwa na mikakati ya kupambana na umasikini huu. Tulikuwa na MKUKUTA namba moja, tukawa na MKUKUTA namba mbili, lakini sasahivi sijaona tena MKUKUTA. Mimi ninashauri tungekuja na mpango mkakati wa kushusha hiki kiwango, 26% bado ni kubwa. Tushushe hiki kiwango, ili kuhakikisha watu wengi wanatoka katika hili dimbwi la umasikini kusudi waweze kuingia

katika hali ambayo ni nzuri, tuweze kuchangia katika uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezikani tuendelee kuwa maskini, Tanzania ni nchi iliyobarikiwa, yenye rasilimali nyingi, yenye ardhi nzuri sana ambayo imetapakaa, yenye madini, yenye kila aina ya maliasili kwa hiyo, hatustahili kuendelea kuwa masikini. Kwa hiyo, ninafikiri Waheshimiwa Mawaziri wangu wawili walete mkakati wa namna ya kupunguza hiki kiwango cha umaskini, ili watu hawa watoke kwenye umaskini na wote tuweze sasa kufurahi kwamba, tuna maendeleo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kukabiliana na hili hebu tujifunze kutoka katika nchi mbalimbali. Kuna baadhi ya nchi ambazo zilikuwa ni maskini kuliko hata sisi, kuna nchi ambazo zimepambana na umaskini na zimefikia kuwa ni nchi zilizoendelea. Sasa hebu tuangalie walitumia mbinu gani kutoka katika ule umaskini mpaka wakafika mahali ambapo ni pazuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukijifunza kutoka kule kwao tunaweza na sisi kuongeza uwezo na mawazo yetu tukaondokana na huu umaskini, tukapunguza kile kiwango cha 26% tukaja labda 20% na mpaka mwisho tukawa na asilimia sifuri ya watu kuwa maskini katika nchi yetu. Kwa sababu, sikubaliani kabisa Watanzania kuendelea kuwa maskini na umaskini isiwe sifa ya kujitetea au ya kujivunia, ni lazima tuone kwamba, hili ni janga. Kila Mtanzania aondokane na umaskini na afanye kazi, ili kuhakikisha kwamba, umaskini huu tunautokomeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza hotuba za Mawaziri wote wawili. Nimeona kipaumbele kikubwa kimewekwa katika sekta za uzalishaji ni kitu muhimu sana, lakini ninafikiri ni muhimu labda kabla sijachangia hilo, kuna suala hili la madai ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais, ameongeza mishahara kwa watumishi wa umma, haijawahi kutokea. Ameongeza kwa kiwango kikubwa, ameboresha maslahi, tunaona madaraja yanapanda kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado kuna tatizo katika mfumo wetu, zile stahiki za watumishi wanapoenda likizo zimekuwa zikichelewa sana. Kwa mfumo, wale wanatakiwa kulipiwa na Serikali zao zile za Mitaa, lakini ni wazi kabisa, kwa mfano nichukulie Halmashauri kama ya kwetu ya Wilaya ya Mbozi ina watumishi, walimu pekee yake wapo zaidi ya 400, sasa wale karibu 200 wote wakienda likizo ya mwaka waka-*qualify* malipo kwa kweli, uwezo wa halmashauri unakuwa ni mdogo sana kuweza kugharamia zile stahiki kuwalipia nauli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasababisha sasa deni lile la watumishi liendelee kukua. Wanasema nenda likizo halafu tutaendelea kudai kwa hiyo, tunakuwa na madeni. Ninafikiri, tuliangalie vizuri ule mfumo wa stahiki za watumishi wanapoenda likizo, namna ya kubaliana nao, itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niongelee miundombinu mizuri katika kipaumbele cha Waziri wa Mipango; tuweke kipaumbele katika maeneo yafuatayo, ameyataja na ameyaweka vizuri sana. Ninachukua neno uzalishaji na kuligawanya katika maeneo matatu, eneo la kwanza ni viwanda, eneo la pili ni biashara na eneo la tatu ni huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale kwenye biashara na viwanda ndio pana kilimo. Kwenye *extractive industry* tuna kilimo, tuna uvuvi, tuna ufugaji, tuna madini na kadhalika. Zile ndiyo sekta za uzalishaji, tuwekeze, tuendelee kuwekeza zaidi itatusaidia sana kuondokana na huu umaskini, itatusaidia sana kuongeza uzalishaji wa malighafi na katika kuongeza vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoka hapo tutakwenda sasa kwenye viwanda mama, *manufacturing industry,* tukitoka pale tutaenda kwenye *constructive industry,* tutaenda kwenye biashara. Nchi yetu kwa sababu, iko *strategically located* lazima tutilie mkazo biashara za ndani na nje, zitatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili kilimo kiweze kuendelea ni lazima tuwekeze kwenye…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Tafadhali hitimisha.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kilimo kiweze kuendelea tunahitaji hii malighafi inayozalishwa basi sasa iongezewe thamani. Ndiyo maana ninatilia mkazo kwamba, viwanda ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, bila kuongeza thamani, tukiendelea ku-*export raw materials* nje, kuuza malighafi ambazo hazijakamilika, hali inakuwa siyo zuri na uchumi hauwezi kukua, ili tukue tuwekeze, tuongeze thamani, nina imani itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja na ninawapongeza Mawaziri. Nina imani kazi waliyofanya, hizi bajeti na mipango waliyoileta ni mizuri sana na sisi tunaiunga mkono, tuna imani tutapiga hatua kubwa sana. Mungu awabariki. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwatambue kwanza Wageni ambao tunao leo. Tunao Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni 20 wa Mheshimiwa Venant Daud Protas, ambao ni watoto wake na rafiki zao kutoka Jijini Dodoma. Tunaomba msimame tuwatambue, karibuni sana vijana wetu. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya Mafunzo; hawa ni wanawake 90 ambao wanatambulika kama, Walioitwa na Mungu kutoka Kanisa la *Redeemed Assemblies of*

*God* la Jijini Dodoma. Karibuni, tunaomba tuwatambue. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ninaomba nimwite Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris na Mheshimiwa Stephen Byabato, wajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii jioni ya leo kuchangia Bajeti Kuu na Mpango wa Taifa. Awali ya yote ninaomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nimshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwahudumia wananchi wa nchi hii na kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninaomba niwashukuru sana viongozi wetu, Waziri wetu wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa. Dkt. Mwigulu, Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Mkumbo, Naibu Mawaziri na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zote ambao ninaamini kwa kipindi kirefu, hadi leo hii, walikuwa hawalali kushughulikia shughuli. Kwa hiyo, ninawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mkuu wangu wa Mkoa ndugu yangu Patrick Sawala kwa kazi nzuri anayofanya ndani ya Mkoa wetu wa Mtwara. Tangu amewasili ndani ya Mkoa wetu wa Mtwara tumeona mabadiliko makubwa ya usimamiaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Amekuwa akizunguka huku na huku kuhakikisha kwamba miradi mbalimbali ya maendeleo inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ndani ya wilaya yangu ninaomba nitoe shukrani zangu kubwa kabisa kwa uongozi mzima wa wilaya, kwa maana ya *DC* wangu bwana Christopher Edward

Magala na ndugu yangu *DAS* bwana Juma Kanyinda, kwa kweli kwa usimamizi mzuri wa shughuli za maendeleo tangu amewasili ndani ya jimbo letu. Tangu amewasili ndani ya jimbo letu tumeona mapinduzi makubwa ya kupunguza migogoro ya wafugaji na wakulima ambapo hapo mwanzo ilikuwa ni kero kubwa. Tangu amewasili tumeona ustawi wa ushirika, tangu amewasili tumeona wananchi wamepunguziwa kero nyingi sana. Kwa hiyo, ninasema Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu ili waendelee kuwatumikia wananchi wa jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze katika mchango ufuatao. Ninaamini kwamba Rais wetu, mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya na anafanya kazi kubwa sana. Sisi watu wa Wilaya ya Nanyumbu tunaahidi kwamba kwa kweli mama hatumdai chochote. Mama amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya ile ilianzishwa mwaka 2005, leo ina miaka 20 tangu imeanzishwa. Ninaomba nieleze mambo ambayo ndani ya miaka minne mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amewafanyia watu wa Wilaya ya Nanyumbu ambao kwa kweli hawakuyategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wazalishaji wakubwa sana wa zao la korosho, lakini zao la korosho lilikuwa linakufa. Mara baada ya mama kuingia madarakani zao la korosho tulikuwa tunazalisha tani 11,000; mara baada ya mama kuingia madarakani amefanya mapinduzi makubwa. Mapinduzi ya kuhakikisha kwamba analiamsha na kuhakikisha kwamba zao la korosho linakuwa ni injini ya Wilaya ya Nanyumbu. Amefanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza amehakikisha kutoa pembejeo na viuatilifu bure kwa wakulima katika kilimo; jambo ambalo huko nyuma halikuwepo. Ametoa pembejeo kwa wakulima wote, na mpaka leo ninavyozungumza pembejeo zinazidi kumwagwa ndani ya jimbo langu. Jambo hili limeleta mapinduzi makubwa sana ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kutoka tani 11,000 mwaka huu tumevuna tani 21,000. Wananchi wa jimbo langu wameingiza bilioni 83, zipo ndani ya jimbo. Ustawi wa wananchi tunawaona, wananchi wametulia, wanaifurahia nchi yao. Kwa hiyo ninasema, kwamba mama anatudai sisi, ametufanyia mambo makubwa kwa kweli tuna kila sababu ya kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuweka pembejeo amehakikisha kunakuwa na bei nzuri ya mazao yetu. Bei nzuri ya mazao ya korosho, bei nzuri ya mazao ya ufuta, tumeanza ufuta bei kidogo inayumbayumba, lakini ninaamini katika misimu ijayo bei ya ufuta itaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ame-*introduce* pia mazao mengine katika soko na stakabadhi ghalani. Hapo awali mbaazi tulikuwa tunauza shilingi 150 kwa kilo moja. Leo tunafikia kilo moja inauzwa mpaka shilingi 2,000; mama amefanya mapinduzi makubwa. Sisi wananchi wa jimbo langu tunasema mama kwa kweli shukrani zetu utaziona mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye umeme. Kabla mama hajaingia madarakani Jimbo langu la Nanyumbu tuna vijiji 93, lakini vijiji vyenye umeme vilikuwa ni vijiji 42. Hivi ninavyozungumza vijiji vyote 93 vimepata umeme. Tuna vitongoji 526 hivi ninavyozungumza vitongoji 310 vina umeme, vitongoji 111 wakandarasi wapo kazini, vitongoji 37 vilitangazwa tenda. Kwa hiyo kwa kweli tunamshukuru sana Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu, sisi ni watu wa vijijini, tunatambua kuwa uchumi wetu bado unategemea kilimo. Ninaomba Wizara iangalie namna ya kuwapatia wananchi hawa umeme ambao umeshafika vijijini halafu wao wakawakata kwenye bili za umeme. Kwa sababu, kama tunaweza kuwakata kodi ya majengo kwenye umeme kwa nini tusiwawekee umeme tukawa tunawakata kidogo kidogo kwenye hizi gharama za kufanya *installation* ya umeme ninakulipia hizo gharama. Kwa kufanya hivyo tutahakikisha kwamba ile dhana nzima ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata umeme inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya lile jimbo kuna tatizo kubwa sana la kukatikakatika kwa umeme. Kuna kitu kinaitwa *high voltage* hasa nyakati za usiku. Wananchi nyakati za usiku wanapata shida sana ya umeme. Ninatambua kazi kubwa inayofanywa na Serikali, na ninatambua kazi kubwa inayofanywa na ndugu zetu wa *TANESCO*. Wanafanya *study* kuhakikisha kwamba kutatua changamoto hii. Ninawaomba ndugu zangu wa *TANESCO* waharakishe, waharakishe sana kuondoa tatizo kwenye jambo hilo, kwa kweli limekuwa kero kwa kipindi kirefu, lakini ninaamini kwa kazi kubwa na meneja mpya aliyekuja na uongozi mpya wa *TANESCO* watalipatia ufumbuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana pia Rais wetu. Sisi Watu wa Mkoa wa Mtwara Wilaya ya Masasi, Nanyumbu tulikuwa bado hatujaunganishwa na *Grid* ya Taifa, lakini sasa hivi mpango madhubuti umekwishaandaliwa, mkandarasi yupo kazini, na dhamira ya Serikali inaonekana. Mama wiki iliyopita alitoa bilioni nne na milioni mia tano ili kuwalipa fidia wananchi wote ambao watapitiwa na *Grid* hii ya Taifa. Kwa hiyo jambo hili limetupa faraja sana sisi wananchi wa Jimbo la Nanyumbu. Tunaamini kwamba shida itakwisha hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo ni kubwa sana kwa Wilaya ya Nanyumbu, kuna shida sana ya maji. Ndani ya miaka yote 20 wananchi wa Makao Makuu ya Kata walikuwa hawajui maji ya bomba. Sasa hivi kuna mradi mkubwa ambao mama ameuleta, wa bilioni 38, wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma, kilometa 100 na zaidi. Hivi ninavyozungumza mkandarasi yupo kazini na 80% ya mradi upo karibu kumalizika. Kwa hiyo tunamshukuru sana mama yetu, tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema ili aendelee kutuhudumia sisi wananchi. Kuna miradi mingi ya maji huko vijijini inaendelea kufanyika. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye upande wa miundombinu ya barabara. Unaweza ukashangaa, ndani ya miaka 20, makao makuu ya wilaya yalikuwa hayana barabara ya lami wala taa, lakini ndani ya miaka minne ya mama ametuwekea barabara za lami ndani ya makao makuu yetu ya

wilaya na taa za barabarani, wananchi wanafurahia maisha. Tunamshukuru sana mama yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba huduma za afya na elimu zinaimarika ndani ya jimbo langu. Hivi ninavyozungumza ndani ya miaka yake minne ametujengea zahanati 15, ametujengea vituo vya afya vitatu, ameniletea milioni 250 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Nanyumbu, na ameniletea magari ya *ambulance*. Kwa kweli tunamshukuru sana Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Waheshimiwa Mawaziri, tunaomba bajeti hii ambayo wametuletea, ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja, iende ikatekeleze yale ambayo wananchi wanayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninaomba nimwombe Waziri wa Mawasiliano. Wilaya ya Nanyumbu ina changamoto ya mawasiliano ya *TBC*, hivi ninavyozungumza *TBC* haisikiki ndani ya jimbo langu. Tunakwenda kwenye uchaguzi wananchi wanategemea *TBC* ili wapate taarifa. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo alifanyie mkazo ili wananchi waweze kupata mawasiliano ya *TBC,* ambacho ni chombo cha uhakika kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhata, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu ya bajeti kuu ya Serikali na mpango wa maendeleo. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwanza mwenye wingi wa huruma na rehema kwa kunipa nafasi ya kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini katika kipindi hiki cha miaka mitano ambayo tunaelekea kuimaliza katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu kwa imani walionionesha, lakini kwa ushirikiano ambao wamenipa. Ni uhalisia usiopingika kwamba yale yaliyofanyika jimboni, kama mwakilishi wao nimewawakilisha Bungeni na Mheshimiwa Rais ameyatekeleza, kiuhalisia huko mbele nitatakokwenda nitaeleza yapi yaliyofanyika. Ndiyo maana tunasema mama Samia Suluhu Hassan sisi wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini hatumdai bali yeye anatudai sisi na tunakwenda kukamilisha kazi hiyo kwenye uchaguzi Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuwatumikia Watanzania. Kiuhakika Mama Samia Suluhu Hassan ametenda utumishi uliotukuka katika kipindi hiki cha uongozi wake wa miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha; msaidizi wake ndugu yangu Chande, Mjumbe wa Kamati Kuu; Profesa Kitila, Waziri wa Mipango na Uwekezaji na wasaidizi wake, pamoja na watumishi wote walioko chini ya taasisi ambazo wanaziongoza kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutimiza maono yake ya kuwafanya Watanzania wafike kwenye nchi ya asali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza *RC* wangu ndugu yangu Malima kwa kazi kubwa ya usimamizi wa fedha za Serikali ambazo tunazipeleka kutoka Bungeni na kwenye Serikali kuu katika kusimamia miradi ya maendeleo ambayo imepelekwa na Serikali kwa ajili ya faida ya wananchi wa Morogoro. Pia, nitumie nafasi hii kumpongeza *DC* wangu ndugu yangu Said Kilakala kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, hasa katika kusimamia migogoro ya wakulima na wafugaji katika Wilaya na Halmashauri ya Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi nitumie nafasi hii; nianze na kumpongeza kwa dhati ya moyo ndugu yangu Mwigulu. Ninachokumbuka, wakati Mheshimiwa Rais anafungua Bunge alizungumzia mambo mawili matatu. Kwanza

alizungumzia suala la *TRA* kutokufunga biashara za wafanyabiashara na maduka ya wafanyabiashara. Alizungumzia pia suala la kutokurudia nyuma kodi za miaka ya nyuma na vilevile kufunga akaunti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Fedha kwa kuweza kusikiliza kilio cha Mheshimiwa Rais. Hata mimi kama Mheshimiwa Mbunge nilizungumzaa mara mbili mara tatu Bungeni. Kongole kwa Mheshimiwa Mwigulu kwa kuruhusu kwamba sasa hivi *TRA* hawatofunga biashara za wafanyabiashara ili wafanyabiashara waendelee kufanya biashara na kuweza kulipa fedha za Serikali katika maeneo yale ambayo wanadaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lile la kurudi nyuma kama Mheshimiwa Rais alivyosema, nimwombe Mheshimiwa Waziri akaliangalie. Kiuhalisia katika kipindi tulichokuwa nacho sasa hivi ni ukweli usiopingika kwamba *TRA* wana uwezo kabisa wa dhati wa kufanya biashara, *I mean* wa kufanya ukaguzi na kuweza kufanya mahesabu na kumfanya mfanyabiashara akalipa na tusirudie tena katika kipindi cha miaka mitano nyuma au minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la miaka mitano au minne linawaumiza sana wafanyabiashara, lakini vilevile watumishi wa *TRA* wasipokuwa waaminifu wanawatumia katika kujinufaisha wao. Kwa hivyo nimwombe akaliangalie hili; vilevile na ufungaji wa akaunti ili wafanyabiashara wawe na utulivu katika kufanya biashara zao na pia waweze kulipa kodi na kuweza kusaidia kusukuma maendeleo ya nchi. Sisi Wanamorogoro Kusini nimeshasema hatuna sababu yoyote ya kumnyima Kura Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu *TRA* vilevile. Nimwombe Mheshimiwa Mwigulu, kuna eneo moja ambalo tumekuwa mafundi *TRA* katika elimu ya mlipakodi. Niombe tungetengeneza kitengo ambacho kitawasaidia wafanyabiashara katika kujua elimu ya utunzaji wa vitabu vyao vya biashara ili kusiwe na mgongano tunapokwenda kwenye

kulipa kodi. Kwa hiyo ninadhani hii inawezekana na akisaidia italeta tija kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiongozi wa kiroho aliwahi kusema kwamba, Wabunge muda wote wanampongeza mama wanasema mama kafanya, mama kafanya sijui itakapofika wakati wa kuja kuomba kura watasema wao wamefanya nini. Ninaomba niseme, kiuhalisia mama amefanya, lakini sisi tumemweleza mama kwa kulilia katika Bunge hili yale matakwa ya wananchi wetu na shida za wananchi wetu. Kwa hiyo hivi tutakavyokwenda, sisi na Mama Samia, nina uhakika kwamba tutarudi tena Bungeni, kwa sababu tumeyatekeleza yale ambayo wananchi wetu wametuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa Morogoro, kuna suala la shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaingia Bungeni kwa mara ya kwanza kuna kazi ilifanyika, lakini nikatoka, nilipata likizo ya miaka mitano. Niliporudi miaka minne hii kwenye upande wa elimu, zimejengwa shule za sekondari tano mpya. Kati ya shule hizo tano mpya tatu za kawaida, moja ya ufundi na moja maalum ya wasichana ya sayansi. Sisi Wanamorogoro tuna kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan; na kwa ukweli yeye anamdai na tarehe 25 tutafanya kazi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu ya msingi tumejenga shule mbili mpya, tumejenga madarasa 107 kwenye jimbo langu tu, nyumba za walimu na kila kitu. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan, tunataka tuwaambie kwamba itakapofika wakati wa kumlipa yeye, tarehe 25, tutakwenda kutia tiki kwenye jina lake na Chama Cha Mapinduzi ili kiendelee kutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya, zahanati 12 zimejengwa, katika kuwasaidia wananchi kwenye maboma milioni 50 zimepelekwa, tumekamilisha na zinafanya kazi kwa sasa hivi. Vituo vya afya vitatu vimejengwa maeneo ya Kisaki, Kisemu

na Kasanga. Juzi tu huku nimepata milioni 250; tunakwenda kujenga kituo kingine cha mkakati kwenye Kata ya Singisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata *ambulance*, tumepata hospitali ya wilaya ambayo imekamilika na inafanya kazi. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na wasimamizi wake; na hasa huyu ndugu yangu Mwigulu kwa kutoa fedha nyingi kwenye miradi hiyo ya maendeleo ambayo leo tunajivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara nina kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan. Sisi Wanamorogoro ndani ya kipindi cha awamu zote barabara ya Bigwa – Kisaki imekuwa ni kero na tumeipigia kelele na hata leo Mheshimiwa Ishengoma wakati anachangia ameizungumza. Wamepita Wabunge na katika Wabunge waliofika mmoja alifika mahali amekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi lakini yote imeshindikana. Ndani ya kipindi hiki cha Mama Samia Suluhu Hassan cha miaka minne ameweza kuruhusu ujenzi uanze kwa kusaini mkataba wa bilioni 132.4 ambayo tayari imeshasainiwa, tunachosubiri ni *advance payment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Mwigulu, kwa utaalam wake wa kutoa fedha kwenye miradi; hii bilioni 13 ambayo anahitaji mkandarasi apewe ili aanze kazi mara moja ili wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki wafurahie matunda ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru kwa ajili ya Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere, ameweza kutoa fedha na mkandarasi anafanya kazi. Tunampongeza kwa kutoa fedha milioni 780 ambayo imefanya upembuzi yakinifu kutoka Ngerengere, tunakwenda Mvuha, tunakwenda mpaka Kisaki ili tuweze kujua gharama ya mradi na tuweze kuujenga. Ni imani yangu kwmaba tutakaporudi tena Bungeni mwakani, Mungu akipenda, miaka mitano ijayo tutafika kisaki kwa ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la umeme, nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan; ndani ya jimbo langu bilioni 27 kulikuwa na vijiji 50 na havina umeme katika vijiji 85. Leo ninapozungumza vijiji vyote 85 vya Jimbo la Morogoro Kusini vinawaka moto. Kulikuwa na vitongoji 434 leo ninapozungumza umeme upo kwenye vitongoji 295, bado vitongoji 141. Kuna vitongoji 90 nimepewa ambavyo ninategemea katika kipindi tunapokwenda kwenye bajeti tunayoipitisha vitakwenda kufanya kazi. Tuna kila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu vilevile kama walivyosema Wabunge wengine umeme unakwenda lakini wananchi wetu wanashindwa kuunganisha. Hebu twende kwenye utaratibu alioupendekeza Mheshimiwa Hasunga; na kuna Mheshimiwa mwingine hapo; tuingize kwenye *tariff* tuwapatie umeme ili wananchi waweze kufurahia matunda ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji tumefanya vizuri sana. Ndani ya jimbo langu kuna miradi mikubwa, zaidi ya bilioni 20 zimetumika kwa ajili ya kupelekea wananchi maji. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mawasiliano ndani ya kipindi cha miaka mitano nimepata minara zaidi ya 14 ambayo wananchi wetu kwenye Kata ya Kolelo, kwenye Kata ya Kasanga, kwenye Kata ya Bungu, kwenye Kata ya Kibogwa, kwenye Kata ya Singisa, Bwakila Juu, Kibungo Juu, Selembala na Kitongoji cha Kilengezi ilikuwa ni hadithi. Leo wakiwa nyumbani wanazungumza na ndugu zao na wapenzi wao katika kufurahia matunda ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina kila sababu ya kuipongeza bajeti hii na pia kumpongeza Mama na kumwomba Mheshimiwa Mwigulu; sisi jumanne tutapitisha kwa kishindo bajeti hii na fedha zitakapotoka ziende zikatekeleze yale maelekezo na maono ya mama ili Tanzania iendelee kung'aa, Morogoro Kusini

iendelee kupaa na Watanzania tuendelee kufurahia matunda ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja na kazi iendelee. CCM Hoyee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent. Mheshimiwa Stephen Byabato.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuendelea kuwatumikia wananchi tukiwa wawakilishi wao humu Bungeni na tukiwa na afya tele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa uzalendo na upendo kwetu sisi Watanzania kwa kazi ambazo anaendelea kuzifanya. Kila mmoja anayesimama anasema *story* nzuri ambazo zipo katika eneo lake la uwakilishi na sisi tunasema hiyo ni vyema na ni sauti zetu kwa mungu kwamba aendelee kumbariki kumpa afya na uhai ili hii mitano tena tunayoisema aikamilishe kwa spidi nzuri ambayo inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri; kaka yangu Dkt. Mwigulu na kaka yangu Profesa Mkumbo, lakini na Naibu Mawaziri na watumishi wengine wote wanaofanya nao kazi kwa sababu wametafsiri kwa uhakika yale maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wakati huu ambapo nataka kuchangia, nianze kwa kusema, hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri Mwigulu aliiwasilisha kimsingi siyo hotuba yake ni Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwenyewe. Mambo yote yaliyoko humu ni ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niki-*quote* hapa mwanzo kwenye utangulizi anasema: "Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2025/2026." Sasa

mwenye Serikali tunajua ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sasa nimpongeze kaka yangu Mwigulu, yale mambo yote tunayoyasema humu yaliyofanyika vizuri kwenye bajeti hii ni kutafsiri kwa usahihi maono na mapenzi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwetu. Kwa hiyo, ninampa pongezi hizo kaka yangu na tunatarajia aendelee kufanya vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yenyewe na bajeti yenyewe ni ya mfano. Kwa mara ya kwanza tangu nimekuwa na uelewa nimeona bajeti ambayo inaungwa mkono na kila mtu na kila kona. Hata wale wenye *negative attitude* sijawasikia wakisema mambo ya msingi kwenye ku-*criticize* hotuba ambayo ilisomwa hapa juzi. Kila mmoja kwa nafasi yake anaisema vyema. Yule ambaye hataki kusema ananyamaza kimya, lakini kwa kuashiria kwamba mzigo umekaa sawa na kwa kweli utatuvusha katika kipindi tunachokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina maeneo matatu ninataka kutoa ushauri kwa sababu ya muda na kidogo nitazungumzia kuhusu ndugu zangu kule Bukoba ambao wamenituma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ninalotaka kushauri ni kwenye eneo la *local content*. Imesemwa, imekuwa *addressed* kwa kiasi fulani kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumeanza ku-*establish* mambo ya *local content* tangu mwaka 1979 kwenye sheria zetu na ziko sheria kadhaa ambazo zina-*address* mambo ya *local content*. Kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma imeelekezwa kwamba kazi zisizozidi bilioni 50 zifanywe na wakandarasi au na wazawa, lakini *local content regulations* zimeeleza na Mheshimiwa Waziri hapa katika ukurasa wa 159 nimeona anaanzisha utaratibu wa kutengeneza kanuni ambazo zitamruhusu kusema ni kazi gani zinazoweza kufanywa na wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano halisi, kipindi tumeanza utekelezaji wa bomba la mafuta, tuliweka mkakati mahsusi wa kuhakikisha wazawa wanapata kazi zile na hivyo tuliziainisha, kazi hii na hii na hii na hii, zifanywe na wazawa. Jitihada hizi ninaomba

niziongezee ufanisi. Mheshimiwa Waziri tumekuwa tuna tatizo la watu kuweka sura za wazawa lakini kiukweli na kiuhalisia wanaonufaika siyo wazawa. Wako Watanzania wenzetu wachache ambao wamekuwa wakisaidia watu wa nje ambao tunatafuta mbinu mbalimbali za kuwazuia kuchukua fursa zetu kuwasaidia wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeshauri wenzetu wa *BRELA* wahakikishe zile kampuni zinazosemwa ni za wazawa ziwe zina wazawa na wanapata hisa zaidi ya 51% ili tuweze kutambua kweli kampuni hii ni ya wazawa na itaweza kutunufaisha sisi hapa nyumbani. Pia, mifumo yao *BRELA* iungwe na wengine; iungwe na *PPRA,* iungwe na halmashauri zetu na iungwe na kila mtu ili tunapoambiwa huyu ni mzawa, tukiingia kwenye mfumo wa *BRELA* kwa *single click,* tunaweza kuona kwamba kweli huyu ni mzawa ili tuweze kujua ni nani ambaye atanufaika na hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tutakapokuwa tuna wasiwasi, tufanye kitu ambacho kwenye sheria za biashara za kampuni tunakifanya, *to lift up the corporate veil;* kujua humu ndani huyu kweli ni mzawa au siyo mzawa anakuja kujinufaisha, lakini vinginevyo ninapongeza hatua ambayo tumeanza nayo ya Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba anapelekewa kutengeneza kanuni...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** …ambazo zitaweza kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha kwamba wazawa wanapata vitu vinavyostahili...

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Saashisha.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka kumpa taarifa mchangiaji mzuri anayeendelea kwamba, pamoja na kwamba tunaweza tukaweka masharti

kwamba wawe wazawa, sasa hivi kinachofanyika ni kweli unakuta yule ni mzawa, mtu anakuja anaanzisha kampuni ya madini anaweka jina la mtu ambaye ni Mtanzania, pengine hata hiyo biashara ya madini haijui na hajawahi kufanya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa *registrar* utakuta kweli kuna Mtanzania mwenye *share,* lakini hajui kinachoendelea. Kwa hiyo, ninafikiri waende mbali zaidi pamoja na kuangalia *NIDA* na kwenda wapi kuchunguza, huyu ambaye anapewa *share* kwenye hizi kampuni na kuonekana ni mzawa, je, anajua kinachoendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Byabato, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Saashisha?

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninaipokea vyema kabisa. Niseme nilipozungumzia *to lift up the corporate veil,* nilichukua ninakimaanisha ndiyo hicho. Kwenye Sheria za Kampuni, kampuni inapoonekana imefanya kosa la jinai, tunaachana na kampuni, tunafunua kuangalia kwenye kampuni wamiliki ni akina nani. Ni Stephen Byabato, Stephen Byabato ni nani? Ni wa wapi? Amezaliwa wapi? Historia yake ya jinai ikoje na vitu kama hivyo ili tuweze kwenda huko. Kwa hiyo, ninaungana na yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini muda wangu utautunza na mimi najimwayamwaya kwa sababu nimekuwa *lastborn*, hata nyumbani kwetu ni wa mwisho kuzaliwa, ninaamini ninao muda kidogo wa kutosha kuendelea kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ningependa kuchangia kwenye eneo la *service levy* na kutoa ushauri wangu kidogo. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hilo la kuamua kupunguza kiwango cha *service levy* inayolipwa kutoka 0.3 kuja 0.25 *percent* ambayo nimeiona ipo katika ukurasa wa 106 wa hotuba hii. Huu ni mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu ambao tunaishi mijini biashara yetu kubwa inayotuingizia mapato ni ushuru wa huduma

pamoja na leseni za biashara. Sasa ninapongeza kwamba tunaanza sasa kuona namna ya kuli-*address*. Sasa nina ushauri kwenye eneo hili. Shida kubwa hasa siyo kwamba wafanyabiashara wetu hawapendi kulipa. Shida moja kubwa ni ku-*calculate service levy* kwa uhakika na usahihi ili mtu aweze kuilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri, Wizara ya Fedha wakae chini na wataalam wao kwa sababu wanajua namna ya ku-*calculate*. Wa-*calculate* watuambie kiwango hiki ndiyo *0.2 percent* ya jambo fulani. Halafu wazitoe hizo kama *figure* ili wenzetu wa halmashauri waende wakatunge sheria ndogo ambazo zitakuwa zinaeleza kwa ma-*group* kwamba, kuanzia sehemu fulani mpaka sehemu fulani kiwango chako cha kulipa ni hiki. Kiasi fulani mpaka kiasi fulani kiwango chako cha kulipa ni hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi kwenda ku-*calculate service levy* kutoka kwenye *turnover* na kutoa gharama za bandarini ni kitu ambacho kwa kweli uhalisia wake ni mdogo kwa wenzetu wale ambao wanafanya *calculation* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu hapa Mheshimiwa Gekul wakati anachangia asubuhi alisema kwamba tuwape elimu wenzetu wa kwenye halmashauri. Ninaboresha zaidi, tutengeneze kabisa viwango viende vimetafsiriwa kwamba wawe wana uwezo wa kujua, sisi huyu tunamkadiria kwa kiwango hiki kwa sababu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze, kadri tunavyosogea mbele, tuache ku-*charge service levy* kwenye *turnover*, tu-*charge* kwenye *profit,* kwa sababu kwenye *turnover* ni pesa ambayo mfanyabiashara kimsingi siyo yake. Tum-*charge* kwenye ile faida ambayo amepata kwa ajili ya kuweza kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ninalopenda kushauri, ni kwenye ukusanyaji wa kodi. Ninapongeza kwa sababu tumependekeza hapa elimu ianze kutolewa kuanzia kwenye shule na imekubalika, lakini tumependekeza na maeneo

mengine. Sasa ningependa kupendekeza jambo moja ambalo limefanywa kwenye *VAT,* kupunguzwa kutoka *18 percent* kuja 16 *percent*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mbele zaidi, tunao vijana wetu wengi mtaani wanaweza kutubunia *startups companies*. Watubunie mifumo ya kutoa *bonus* kwa wale watu wanaolipa na wakalipa na kodi waweze kupata *bonus* na wakishapewa *bonus* kila mtu atapenda kulipa kodi ili aweze kupata hiyo *bonus* ambayo anaipata kwa kuhakikisha kodi imelipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwenye mitandao ya simu wenzetu wa *Vodacom* wana Mfumo unaitwa Tuzo; ukiwa unanunua vocha kwa kutumia *M-Pesa*, unapata tuzo na zile tuzo baadaye unaweza ukazi-*convert* ukanunua vocha, ukalipa vitu mbalimbali, ukazibadilisha kwenye pesa. Tunaona kwenye maduka kama *Shoppers*, ukienda unaulizwa kama una kadi ili u-*credit* zile unit zako kule kwingine na maeneo mengine kama hayo. Kwa hiyo, tuanzishe mfumo huo na mtu aweze kupata hiyo pesa na kuitumia. Tutapunguza tatizo kubwa sana la kuweza kukusanya kodi ambazo zinatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Bukoba Mjini wamenituma niseme hivi, miundombinu inayojengwa kutoka kule Bukoba Mjini, Kagera kwa ujumla kuja mjini itarahisisha upelekeaji na uletaji wa mizigo na bidhaa mbalimbali. Mikoa ya pembezoni mwa nchi tunapata tatizo la kuwa na gharama kubwa za usafirishaji na hivyo bidhaa zetu nyingi haziuziki na uwekezaji kwenye viwanda unakuwa ni mgumu. Sasa wanaomba *SGR* ambayo inakwenda mpaka Mwanza ikamilike ili waweze kutoa ndizi zao ambayo ni mazao sasa ya biashara kutoka Bukoba kwa meli kuja Mwanza na baada ya hapo Mwanza, ndizi zije Dodoma ziende Dar es Salaam; watu wauze na waweze kununua na kufanya biashara kubwa kwa sababu ni zao la kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanikiwa kwa miundombinu hii ndiyo kutakakotufanya sisi sasa tuanze kujiona ni sehemu nzuri zaidi ya uwekezaji kwa zile malighafi na *resources* ambazo tuko

nazo maeneo ya pembezoni. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuanzia na hiyo, lakini na mengine ya kiuchumi na kimageuzi ambayo ameyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Bukoba hatuna la kusema. Miradi ya kimkakati ambayo ilishindikana na kwa miaka mingi, Dkt. Samia amesema safari hii soko litajengwa na tayari mkandarasi ameshapatikana; stendi itajengwa, mkandarasi ameshapatikana; Kingo za Mto Kanoni ambao umekuwa ukiathiri wananchi zitajengwa, mkandarasi ameshapatikana lakini na barabara zaidi ya kilometa 10 katikati ya mji zitajengwa kwa sababu ya mageuzi ambayo tunakuja nayo. Bukoba Mjini tunasema, hatumdai Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ya mambo makubwa aliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema katika elimu, afya, maendeleo ya jamii na maeneo mengine yote tumefanikiwa na tumepiga hatua kubwa. Sasa kwa sababu ya muda sitaweza kuyataja yote, lakini tunamuahidi kwamba tumeyaona na tunamhakikishia kwamba kule kwetu kura zipo za kutosha. Pia, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuhakikishia usalama na utulivu wa wananchi. Moja, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amesema, ni marufuku kufunga maduka ya biashara ya wafanyabiashara na sisi watu wa mijini ndiyo vyanzo vyetu vikubwa vya mapato, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia ameenda mbali zaidi amesema na akaunti zao tuziache. Tusiwa-*harass* na kuwafanya washindwe kufanya biashara kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wamenituma niseme hivi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Dkt. Samia tulimaliza Januari; na mimi ndiyo kijana wao ambaye wamenituma nije kuyasema hayo. Wanasema wale wote wanaotaka kuja Bukoba Mjini kugombea wanaulizwa, unataka kuja kufanya miujiza gani ambayo Byabato na Dkt. Samia

hawajafanya? Kama huna miujiza mipya kule upaache kwa sababu siyo pa kuchezea chezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tulitamani kusonga mbele na njia inaonekana na wamesema umri unaruhusu, ninatosha na ninamini wataendekea kunipa nafasi tena ya kunituma kuja kuwawakilisha na ninawatakia heri wenzangu wote. Twende tukakamilishe hayo machache ambayo tuko nayo. Mheshimiwa Dkt. Samia lake limeshaisha, Oktoba Bukoba Mjini tuna-*tick,* tunamsubiria aje kuzichukua halafu turudi hapa Novemba kwa ajili ya kwenda kuendelea na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninawashukuru wote na ninawatakia heri na Mwenyezi Mungu atubariki na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Byabato.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumepata nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Serikali. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Waziri ambao mmeendelea kupokea hoja za Waheshimiwa Wabunge ili siku ya tarehe 24 tuweze kuhitimisha kwa mafanikio makubwa.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza shughuli zetu za leo na ninaomba niahirishe Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.52 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 19 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*